**Kikao cha Saba - Tarehe 19 Machi, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora):** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji ya Maagizo ya Baraza yaliyotokana na ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2013/2014.

Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2013/2014.

Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi (O) Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako nawasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2013/2014.

Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha mezani ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Mhe. Mohamed Mbwana Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma):** - Aliuliza:

JKU ni miongoni mwa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vilivyoanzishwa kisheria hapa Zanzibar, lengo lake kubwa ni kuwajenga vijana wetu kiuzalendo pamoja na kuwatayarisha katika masuala ya ulinzi wa nchi pamoja na kuinua uchumi wao na Taifa kwa ujumla. Na kwa kuwa upande wa Tanzania Bara JKT wameweza kufanya mambo makubwa ya kiuchumi kama

vile kumiliki Shirika la Biashara (*SUMA JKT*) pamoja na kumiliki kampuni za ujenzi wa majumba.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawapatia nyenzo za kutosha vijana wetu hawa wa JKU ili angalau waweze kufanya kama vile wenzao wa JKT.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kabla ya kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake Na. 10, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyosomeka jina lake jeshi hili ni Jeshi la Kujenga Uchumi. Hivyo vijana wengi wanaopitia katika jeshi hili, ukiondoa wale wanaoajiriwa ni kwa ajili ya kuwapa mafunzo ya kiuzalendo na kujifunza mbinu za utendaji kazi ikiwemo ufundi, kilimo na ujasiriamali.

Serikali imekuwa ikiwapatia nyenzo za kufanyia kazi kwa kadri hali ya uchumi inavyoruhusu. Na kwa mfano, Serikali imewapatia vifaa vya kilimo ikiwemo trekta, vifaa vya ufundi, vifaa vya shughuli za mifugo na kwa sasa tunaendelea na utaratibu wa kutoa mafunzo ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, pia Baraza limepitisha sheria ya Uwakala wa Ulinzi, jambo ambalo litakiimarisha kikosi hichi kiuchumi kama wanavyofanya wenzao wa *SUMA JKT*. Aidha, mashirikiano baina ya JKT na JKU yameimarishwa, na hivi karibuni tunategemea kuwa na miradi ya pamoja na kubadilishana uzoefu, hali ambayo itasaidia sana kikosi chetu kujiimarisha kitaaluma na kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Serikali imeanza kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi na itaendelea kuwapatia nyenzo hizo kadri mahitaji yatakavyojitokeza kwa kuzingatia uwezo wa Serikali.

**Mhe. Mohamed Mbwana Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe.Waziri.

Kwa kuwa Kikosi cha JKU kama alivyosema ni Jeshi la Kujenga Uchumi, na kwa kuwa hivi sasa Mhe. Waziri amesema kwamba wanakiimarisha kikosi hichi kwa kukipatia nyenzo mbali mbali ikiwa ni pamoja na ufundi pamoja na kuanzisha vile vile suala zima la uvuvi katika kikosi hichi.

a) Je, Mhe. Mwenyekiti, ni zana gani za uvuvi ambazo mumezitayarisha katika kikosi hichi ili vijana wanapotoka pale waweze kujiajiri.

b) Kwa kuwa kikosi hichi kinatoa mafunzo ya kiufundi. Je, ni zana gani za kiufundi ambazo zinawawezesha vijana hawa watakapotoka pale waweze kujiajiri.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Mbwana Hamad maswali yake ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Zana za uvuvi zinaeleweka Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza; zana za uvuvi katika nchi yetu ni boti, nyavu, mishipi. Hizo ndizo zana ambazo tunajitayarisha nazo.

b) Zana za ufundi ambazo tunajiandaa kuwaimarishia vijana hawa wa JKU au Kikosi chetu cha JKU ni zana zote zinazohusiana na masuala ya umeme, masuala ya useremala, masuala ya uwashi na masuala ya ufundi mwengine wa kutengeneza magari na kadhalika. Hizo ndizo zana ambazo tunajiandaa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa JKT huwa wanafanya kazi kwa karibu na wenzao wa Jeshi la Polisi katika baadhi ya kazi nyengine ambazo zinakuwa zinahitajika. Na karibuni tu tuliwaona wenzetu wa Tanzania Bara wakifanya mafunzo ya pamoja baina ya JKT, Jeshi la Wananchi wa Watanzania na Polisi ili kuwajenga kinadharia, kisaikolojia pamoja na uelewa wa kazi zao.

Je, kwa upande wa Zanzibar mafunzo kama haya huwa yanafanyika au hayafanyiki.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mafunzo kama hayo Zanzibar yanafanyika na yamekuwa yakifanyika katika kipindi cha muda mrefu kati ya vikosi vyetu hivi vya ulinzi na usalama na yataendelea kufanyika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kuweza kumuuliza maswali mawili ya nyongeza Mhe. Waziri. Pamoja na majibu yako Mhe. Waziri mazuri sana asubuhi ya leo.

a) Mhe. Mwenyekiti, kule wenzetu JKT mara nyingi Wabunge wanakuwa wanachukuliwa kupelekwa mafunzo Waheshimiwa Wabunge. Je, Mhe. Waziri na wewe huoni ipo haja sasa katika JKU yako ukawachukua Waheshimiwa Wawakilishi ukawafanyia mafunzo. *(Makofi).*

b) Kwa kuwa vijana wetu munawakusanya kwa lengo la kutaka kuwapa taaluma kati ya kazi za mikono na kazi nyengine za kushughulisha akili. Je, Mhe. Mwenyekiti, huoni ipo haja angalau na wao wakapata shilingi hamsini ya kuondokea pale kwenda kutafuta sabuni ya kuweza kufua nguo zao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk maswali yake ya nyongeza kama hivi ifuatavyo.

a) Kwanza nataka niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge kwenda kupata mafunzo JKT, siyo suala la msingi na la lazima, ni suala la yule mtu ambaye anajihisi anataka kwenda kupata mafunzo hayo ya ukakamavu, anaomba na kikosi au jeshi la JKT likiona nafasi hiyo ipo wanawaalika wanaweza kwenda kupata mafunzo. Kwa hivyo, siyo suala kwamba ni utaratibu wa kisheria au ni utaratibu uliowekwa rasmi, ni utaratibu wa mtu mwenyewe anavyojiona. Sawa sawa na mtu kujiunga na vikundi vya mazoezi, wapo wanaojiunga na wapo ambao hawajiungi.

Kwa hivyo na sisi ikitokezea haja ya kufanya hivyo tunaweza kufanya hivyo. Kama haipo haja ya kufanya hivyo hatuwezi kufanya hivyo.

b) Je, hatuoni haja ya kuweza kuwaongezea ile asilimia fulani ya sabuni vijana wetu wanaokwenda kujiunga na JKU kujitolea. Tunaona haja hiyo ipo na katika bajeti iliyopita tulitoka kutoka shilingi elfu moja mia tatu hadi shilingi elfu tano kulingana na uwezo tulionao.

Hata hivyo mipango inafanywa ya kuingiza kwenye bajeti ijayo ikiwezekana tuone kuwaongezea vijana hawa sabuni kutoka kima cha sasa cha shilingi elfu tano hadi pale ambapo bajeti yetu itaturuhusu, lakini tunao mpango huo wa kuwaongezea sabuni.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Na. 23**

**Kuimarishwa na Kupatikana Nyenzo Vyuo vya Mafunzo**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** - Aliuliza:

Kikosi cha Mafunzo, kupitia wanafunzi wake wamekuwa na umakini mkubwa katika suala zima la uzalishaji mali kupitia kilimo cha aina mbali mbali kama vile mihogo, viazi, majimbi, vitunguu na mboga mboga.

a) Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya kikosi hiki ili waweze kununua matrekta angalau manne kwa ajili ya kambi zake zote za Unguja na Pemba.

b) Ni lini Serikali itawapelekea vijana wetu hawa miundo ya umwagiliaji ili waweze kusaidiana na Serikali katika kupunguza umasikini pamoja na kujiongezea vipato.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake Na. 23 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ofisi yangu inawasiliana na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya ununuzi matrekta mengine na vifaa vyengine vya kilimo. Kwa sasa matrekta mawili

yameshapatikana aina ya *FORD* ambayo yamegaiwa katika kambi ya Kinumoshi Unguja na Kangagani kwa Pemba.

b) Kwa upande wa upatikanaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji, Wizara yangu imeshafanya mawasiliano na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa maelekezo ya Serikali na tumekubaliana mashamba ya mpunga yanayofaa kwa kilimo ya umwagiliaji maji yaingizwe katika mradi mkubwa wa umwagiliaji maji kitaifa ambao unafadhiliwa na Korea na nchi nyengine za wahisani.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa hawa ndugu zetu wanafunzi katika Vyuo vyetu vya Mafunzo huwa wana shida sana ya bajeti, kwa sababu bajeti yao wanayopelekewa huwa haikidhi haja kwa vile muda mwengine huwa wanapambana na kundi kubwa la mahabusu ambazo kesi zao huchukua kipindi kirefu. Kwa mfano hizi siku karibu na siku za chaguzi, mahabusu wengi wanapatikana pale Magerezani huku ikiwa hawana bajeti.

Na kwa kuwa ni mpango tu uliopo kwa kuwasiliana na watu wa China ili wapelekewe vifaa mpango ambao hatujui lini utakamilika.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali bajeti hii inayokuja itapanua bajeti hichi Kikosi cha Mafunzo ili waweze kukabiliana na wimbi kubwa la mahabusu ambalo hupatikana hususan katika kipindi cha chaguzi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:**Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli tunao ufinyu wa bajeti katika Chuo cha Mafunzo kwenye hali nzima ya kukabiliana na mahabusu ambao wanakuwepo, lakini hata hivyo, haijawahi kutokea hata wawe mahabusu wa namna gani wanaopelekwa Chuo cha Mafunzo kama ni amana kutoka Mahakamani. Chuo cha Mafunzo kikashindwa kuwapatia huduma za chakula pamoja na ufinyu wa bajeti.

Kwa hivyo hivi sasa tutaendelea kuiomba Serikali au kukaa ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba bajeti ya chakula ya Chuo cha Mafunzo inaongezwa ili kuweza kukabiliana na hali yoyote ile itakayotokea ya wingi wa wanafunzi watakaokuwa wamefungwa ama wingi wa mahabusu ambao watakuwa wamepelekwa Chuo cha Mafunzo kama ni amana kutokana Mahakamani.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Mafunzo kimekuwa kikifanya kazi nzuri kwa masuala haya ya kilimo. Na kwa kuwa wenzetu Kikosi cha JKT wamekuwa na mradi wa kukopesha matrekta kwa bei nafuu na kwa masharti nafuu, kwa kupitia hasa kwenye wizara yako, kupitia JKU.

Je, haioni iko haja ya kukopa matrekta yale kwa ajili ya kuwapatia Chuo cha Mafunzo kuendeleza kilimo, na kama haja hiyo ipo, kuna mpango gani wa kukopa matrekta hayo ili kilimo kiweze kuendelea hususan kupitia vikosi vyetu vya Mafunzo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, matrekta ambayo tumeyapata yanatokana na mkopo wa serikali, JKU ni taasisi ya serikali. Kwa hivyo matrekta yamekopwa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili, serikali imeamua tupate mgao wa matrekta manne, ambapo mawili tumepeleka JKU na mawili tumepeleka Chuo cha Mafunzo. Serikali itakapoandaa tena mpango wa kukopa ama wa kununua, nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba vikosi vyetu hivi vinavyojishughulisha na masuala ya kilimo, JKU na Mafunzo basi watapata mgao kwa mujibu wa maamuzi ambayo yatafanywa na serikali.

Kwa hivyo, haja tunaiona kwa sababu bado matrekta tuliyonayo hayajatutosha, lakini hayo yaliyopatikana manne tumepewa na tumeyagawa katika vikosi viwili. Ahsante sana.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, lakini serikali ni serikali. Serikali ina mzigo mkubwa kwa jamii.

Je, Mhe. Waziri huoni iko haja sasa ukatoa kibali kwa kushirikiana na serikali ukaviruhusu vyenyewe vikosi vikaenda kukopa matreka kwa wenzao.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza vikosi hatujavizuiwa ikiwa wanaona wanazo fedha wanazozalisha, ambazo wanaweza wakaenda wakalipa Suma JKT kwa kukopa matrekta, hatujazuia serikali. Wao wenyewe wanayo mamlaka hiyo, isipokuwa tutakachotaka kuhakikisha wawe na uwezo wa kuweza kurejesha deni, kwa sababu hizi ni taasisi za serikali, inaposhindwa kulipa deni maana yake dhima ile inarudi Serikali Kuu.

Kwa hivyo, sisi wakituonesha mipango yao kwamba sisi tunao mpango wa kwenda kukopa na utaratibu wa kulipa ni huu na uwezo wetu ni huu, hata matrekta 100 kuanzia sasa waende wakakope. Mimi ni Waziri wao basi nitahakikisha hilo linafanyika, lakini lazima tuwe tunajua uwezo wa kulipa lazima wawenao, lakini kama uwezo wa kulipa hawana, bado wataendelea kusubiri utaratibu wa kiserikali ili waweze kupata matrekta hayo ya mkopo.

**Nam. 59**

**Dhima ya Serikali Kumaliza Mabanda ya Skuli**

**Mhe. Mohammed Haji Khalid** - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya swali langu namba 59 kujibiwa, naomba kufanya marekebisho kidogo katika mstari wa tano neno la mwisho, ambalo hapa linaonekana "kuongezeka", libadilike na kuwa "kuezeka". Baada ya marekebisho hayo sasa naomba swali langu hilo lijibiwe.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inawashajihisha na kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kujenga mabanda ya kusomea, kwa kuwa kwa sasa Serikali haina uwezo wa kujenga mabanda hayo lakini pia Serikali imechukua dhima ya kuyamaliza na kuezeka mabanda pale inapofikia hatua hiyo.

(a) Je, katika mwaka wa fedha 2013/2014 kulikuwa na mabanda mangapi nchini yaliyofikia hatua ya kuezekwa.

(b) Kati ya hayo mabanda mangapi yalikuwa ya Wilaya na Mkoa.

(c) Kama mabanda yote yaliyofikia hatua hivyo yangaliezekwa ni kiasi gani cha fedha zingetumika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wananchi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, wameshajihishwa na kuhamasishwa katika ujenzi wa madarasa mapya. Pia Sera yetu ya elimu inaelekeza kuwa wananchi wanapofikisha ujenzi hadi katika hatua ya kutaka kuezeka, Wizara na wahisani watachangia nguvu za wananchi. Pamoja na uchache wa fedha za miradi ya ujenzi, Wizara kwa kushirikiana na wahisani wameendelea kuunga mkono nguvu za wananchi. Katika kipindi hiki, jumla ya madarasa 177 yanaendelea kukamilishwa; ambapo Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SIDA*) limechangia katika kukamilisha ujenzi na kuyapatia samani madarasa 140 na Jumuiya isiyo ya kiserikali ya "*Milele Zanzibar Foundation*" imekamilisha ujenzi wa madarasa 37 na nyumba za walimu kwa Unguja na Pemba. Ujenzi huo utagharimu jumla ya Tshs. 2,797,384,000/= na unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi Aprili 2015. Baada ya maelezo hayo

*(Hapa ilikuwa kimya kwa dakika chache tu)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri, inaonekana hicho kitabu chako kinazuia hicho kipaza sauti na inakosekana kuingia kwenye *Hansard*. Kwa hivyo, naomba urejee tena ili iweze kuingia katika *Hansard* hayo maneno unayosema. Ahsante tuendelee.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa wananchi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, wameshajihishwa na kuhamasishwa katika ujenzi wa madarasa mapya. Pia Sera yetu imeelekeza kuwa wananchi wanapofikisha ujenzi wao hatua ya kuezeka, Wizara na wahisani watachangia nguvu za wananchi. Pamoja na uchache wa fedha za miradi ya ujenzi, Wizara kwa kushirikiana

na wahisani wameunga mkono nguvu za wananchi. Katika kipindi hiki, jumla ya madarasa 177 yanaendelea kukamilishwa; ambapo Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SIDA*) limechangia katika kukamilisha ujenzi na kuyapatia samani madarasa 140 na Jumuiya isiyo ya kiserikali ya "*Milele Zanzibar Foundation*" imekamilisha ujenzi wa madarasa 37 na nyumba za walimu kwa Unguja na Pemba. Ujenzi huo utagharimu jumla ya Tshs. 2,797,388,000/= na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili 2015. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, kulikuwa na jumla ya madarasa 501 yaliyofikia hatua ya kuezekwa.

(b) Uchambuzi wa madarasa hayo kiwilaya na mkoa ni kama hivi ifuatavyo:-

**Jedweli Namba 1. Madarasa yanayohitaji kukamilishwa na gharama zake**

| WILAYA: | YANAYOJENGWA 2014: | JUMLA YA GHARAMA (TSHS) |
|---|---|---|
| **Mjini** | **0** | **0** |
| **Magharibi** | **58** | **626,400,000** |
| Mjini | 58 | |
| Magharibi | | |
| Kaskazini A | 43 | 464.400.000 |
| Kaskazini B | 38 | 410,400,000 |
| Kaskazini | 81 | |
| Unguja | | |
| **Kati** | **44** | **475,200,000** |
| **Kusini** | 15 | 162,000,000 |
| Kusini Unguja | 59 | |
| **Micheweni** | **87** | **939,600,000** |
| **Wete** | 76 | 820,800,000 |
| Kaskazini | 163 | |
| Pemba | | |
| **Chake-Chake** | 58 | 626,400,000 |
| **Mkoani** | 82 | 885,600,000 |
| Kusini Pemba | 140 | |
| **Jumla** | **501** | **5,410,800,000** |

(c) Madarasa hayo yatagharimu jumla ya Tshs. 5,410,800,000/= hadi kukamilika na kuyapatia madawati

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nina kijiswali kimoja kidogo tu cha nyongeza.

Je, katika mwaka huu wa fedha uliomalizika wa 2014/2015, wizara yake imeezeka mabanda mangapi Unguja na Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, madarasa ambayo tumeezeka kwa mwaka huu kwa kupitia wahisani ni *SIDA* tumeezeka madarasa 177 na *Milele Zanzibar Foundation* tumeezeka madarasa 37. Bajeti ya serikali katika vifungu vyote viwili bado hatujatiliwa pesa mpaka sasa hivi.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu sana kabisa naomba pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pale nimuulize swali moja la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kabla ya kuuliza swali langu Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza mfanyabiashara mashuhuri hapa nchini Said Salim Bakhressa, kwa kuweza kuisaidia ile skuli ya Jeshi shilingi milioni 30 ambazo zimetumika katika kujengea banda moja la skuli. Baada ya shukrani hizo vile vile naomba niwapongeze skuli ya jeshi inayomilikiwa na 14 KJ iliopo katika Jimbo langu la Wawi, kwa kuweza kutokea mshindi wa mwanzo kabisa katika mitihani ya darasa la saba. Nawapongeza sana skuli pamoja na wanajeshi ambao wametusaidia sana katika skuli ile.

Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza. Kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti skuli hii ya jeshi imefanya vizuri sana inayomilikiwa na 14 KJ na hata mfanyabiashara Said Salim Bakhressa akatupatia milioni 35 kwa ajili ya ujenzi.

Je, Wizara ya Elimu haiwezi kuyaezeka yale mabanda ambayo tumeshafikia katika kuezeka pale ikawa kama zawadi kwa hii skuli ya jeshi. *That's* (a).

(b) Kwa kuwa Skuli ya Vitongoji iliopo Pemba *Dakhil Shimalia* mwa mji wa Chake Chake ina mabanda mawili na haijabahatika hata siku moja kumaliziwa. Haya mabanda yako siku nyingi sana kiasi ambacho kama ni kitu cha kuoza, tayari kiwe kimeshaoza. Huu ni karibu mwaka wa 10 yamemaliza yale mabanda pale hayajaezekwa.

Je, ni lini skuli ile ya Vitongoji ilioko *Shimalia* mwa mji wa Chake Chake, serikali itatia mkono wake kwa kuwamalizia yale mabanda ambayo karibu mwaka wa 10 Mhe. Naibu Waziri yapo hayajamalizwa na serikali, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi pia nataka nimpongeze Mhe. Said Bakharessa kwa kuisaidia skuli ile ya jeshi na pia niipongeze skuli hii ya jeshi kwa kufanya vizuri katika mitihani yao, lakini kwa hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa mzigo ambao tunao wizara wa uezekaji wa mabanda, skuli ya jeshi ambavyo najua ni skuli ya wanajeshi ambapo ni skuli ya *private* na sisi kama wizara tunawasaidia walimu, vitabu.

Skuli moja ya *private* ambayo imepata bahati kubwa basi ni skuli ile ya jeshi. Najua kuna viongozi wa serikali wengi ambao walitembelea. Mmoja ni Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye alichangia pale, wa pili ni aliyekuwa Waziri Kiongozi Mstaafu Mhe. Shamsi Vuai

Nahodha alichangia pale, wa tatu ni Makamu wa pili Rais alichangia pale na mfanyabiashara Said Bakhressa pia kachangia pale.

Sasa Mhe. Mjumbe nataka uridhike kuwa skuli ile ina mkono wa kuchangiwa sana na hizi pesa chache ambazo tunazipata Wizara ya Elimu, basi hizi zisaidie katika kumaliza mabanda ya skuli nyengine. Skuli yako ya Vitongoji Mhe. Mjumbe, nikuahidi tu kama pindipo tukitiliwa pesa katika fedha hizi za serikali, mradi wa elimu ya lazima basi tutakumalizia skuli ile kwa sababu kweli najua ni ya muda mrefu sana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa kweli umenifanyia haki sana kunipa nafasi hii, nakushukuru sana. Mhe. Mwenyekiti, kabla swali langu la nyongeza, naomba nitoe maelezo kwa ufupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna skuli ambayo ilikuwa na matatizo makubwa ya mabanda na walimu basi ni Skuli ya Mwambe ndani ya Jimbo langu. Skuli hii ya Mwambe ni skuli pekee kwa Pemba ambayo wanafunzi huwa wanakwenda mikondo mitatu. Katika kipindi cha kawaida cha kusomesha wanafunzi ni dakika 40, lakini Skuli ya Mwambe ni pekee kwa Pemba ambayo inasomesha wanafunzi kwa dakika 20 na ina upungufu wa walimu wasiopungua 16.

Nachukua nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kuishukuru serikali sana kwa kupitia *DANIDA* na *Milele*, kwa kuezeka mabanda mawili yenye madarasa 8, na kukarabati banda moja lenye madarasa manne, lakini bado hatujaweza kupunguza tatizo la mikondo mitatu kwa Skuli ya Mwambe na bado walimu na wanafunzi wataendelea kusoma kwa dakika 20.

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali imeahidi kwamba watajenga jengo jipya la ghorofa lenye madarasa 12, ambalo litapunguza tu msongamano wa wanafunzi. Naomba kujua mpango huo wa ujenzi utaanza mwaka gani.

b) Kwa kuwa skuli hiyo ina upungufu wa walimu zaidi ya 12, wananchi wa Jimbo la Kiwani na Mwakilishi wao wamekubaliana kutafuta vijana wenye Diploma na Cheti cha Ualimu ambao sasa wanajitolea bila ya malipo. Je, serikali itakuwa tayari kupokea orodha ya vijana hawa, na kushirikiana na Mwakilishi wao kuwapatia posho kwa kiwango ambacho watakubaliana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nipokee kwanza shukrani za yale mabanda 8 ambayo yamejengwa na *SIDA* na mabanda 4 ambayo yamejengwa na *Milele*. Kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kama wizara yangu ina mpango wa kujenga jengo jipya pale la ghorofa ambalo litakuwa na madarasa 12 kwa kupitia *OPEC*.

Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa mpango ule bado upo na pindipo taratibu zitakapokamilika basi ujenzi ule utaanza mara moja. Najua pia katika skuli yako kuna tatizo la walimu, lakini ikiwa wapo walimu ambao wanajitolea na wanaweza kuajirika, na kwa vigezo ulivyotoa inaonekana wanaweza kuajirika, kwa sababu anasema kuna wengine ambao wana *diploma*, basi tufuate tu utaratibu wa uajiri; waandike barua Wizara ya Utumishi, na sisi Wizara tutasimamia, kwa sababu kwa kweli kuna haja ya kupata walimu pale, walimu waliopo hawatoshelezi kabisa.

Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 38**

**Hatua Madhubuti Kukinga Kichocho**

**Mhe. Saleh Nassor Juma** – Aliuliza:

Kichocho (*Schistomiasis*) ni moja kati ya maradhi yanayozaliwa na maji (*water born diseases*), inasadikiwa kichocho cha uchango (*Intestined Schistomiasis*) kwa kiasi kikubwa huweza kusababisha Saratani ya utumbo pale kinapochelewa kupata tiba kwa muda mrefu.

(a) Je, taarifa hiyo ni ya kweli.
(b) Ni lini Serikali itachukua hatua thabiti kwa ajili ya kutoa taaluma Vijijini juu ya wananchi kujikinga na kichocho kama ilivyofanyika kwa upande wa kudhibiti malaria nchini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukawa wenye afya njema na uzima na kuwepo katika Baraza hili leo kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kichocho cha tumbo kinaweza kusababisha saratani ya machango kikichelewa kutibiwa kwa muda mrefu. Kichocho cha aina hii hakipatikani hapa Zanzibar na hakipo kabisa.

Kichocho cha kibofu cha mkojo pekee ndicho kinapatikana hapa visiwani Zanzibar. Kichocho hicho huambukizwa kutoka kwa mtu mwenye kichocho kwenda haja ndogo kwenye maji safi (mto, bwawa au ziwa), baadae vimelea hivyo huingia katika mkondo wa konokono wadowadogo maalum wajulikanao (*Bullinus Globosus*). Ugonjwa wa kichocho cha kibofu cha mkojo pia unaweza kusababisha saratani ya kibofu cha mkojo endapo kitakosa dawa ama tiba muafaka kwa muda mrefu. Kama vile ambavyo kichocho cha machango ya tumboni kilivyo.

(b) Mhe. Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupambana na kichocho hapa nchini tokea miaka ya sabini (1970). Huduma zimekuwa zikitolewa kwa watoto wa skuli katika kupunguza kasi ya maambukizo, kama tujuavyo watoto ndio waathirika wakuu wa kichocho. Kuanzia mwaka 2012 Wizara ya Afya imeongeza mikakati katika kudhibiti na hatimae kutokomeza kabisa kichocho hapa Zanzibar. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(c) Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya inaendelea kutekeleza mikakati mbali mbali ya kupambana na kichocho hapa Zanzibar tokea mwaka 1970. Huduma zimekuwa zikitolewa kwa watoto maskulini, katika kupunguza kasi ya maambukizo kama tujuavyo Watoto ndio waathika wakuu wa kichochote hicho, kwani wao ndio waogaji wakuu na waogoleaji wakuu katika mito na madimbwi hayo.

Kuanzia mwaka 2012 Wizara ya afya imeongeza mikakati katika kudhibiti na hatimae kutokomeza kabisa kichocho hapa Zanzibar, kama ilivyokuwa juhudi hizo zimefanyika katika ugonjwa wa malaria. Mikakati hiyo ni pamoja na ifuatayo:-

(i) Kulisha dawa za kichocho na minyoo katika jamii yetu mwaka mara mbili, hasa kwa yale maeneo yaliyobainika kuathirika zaidi, yenye mabwawa au mito ya maji.

(ii) Kunyunyiza dawa za kuangamiza makonokono hayo yanayojulikana kama (*gulinasi clobal sas*) kwenye mito na mabwawa katika shehia mbali mbali za Unguja na Pemba. Unyunyizwaji wa dawa unafanyika kila mwisho wa msimu wa mvua.

(iii) Kutoa elimu ya kichocho kwa jamii na katika maskuli. Pia elimu hii hupatiwa walimu kwa lengo la kuwafundisha wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kulijulisha Baraza lako Tukufu kwamba Wizara ya Afya hivi sasa kwa kushirikiana na Serikali ya China, pamoja na Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na wahusika wakuu wengine mbali mbali kutoka vyuo vikuu vya nje na wahisani wa maendeleo, tayari wako nchini kutoa huduma kwa wananchi katika kuhakikisha maradhi ya kichocho yatabaki historia hapa Zanzibar kama vile ambavyo Malaria ilivyopungua na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia kwa mafanikio ya miradi hii basi kitatoweka kabisa. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Juma Nassor:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, mimi naomba nimuulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri *Urinary Schistosomiasis* ambayo inasababishwa sana *chistosoma hemoglobin na Schistosoma japanicum* amekiri kwamba yanaweza yakasababisha kensa ya kwenye kibofu cha mkojo pamoja na mapitio ya mkojo, na kwa kuwa kensa ni maradhi hatari sana katika nchi yetu, kwa kuwa amesema kwamba lengo la Serikali ni kuifanya Zanzibar *free from Schistosomiasis* kama ilivyofanywa *free from malaria.* Na kwa kuwa Serikali mara nyingi inatupatia tiba za magonjwa mengi kwa kutumia *chemo thermotherapy* yaani kutumia makemikali, na kwa kuwa Mhe. Waziri kwa upande mmoja amekiri kwamba *without snail no Schistosomiasis,* yaani bila ya kuwepo kowa basi hakuna kichocho, hili amelikiri hapo katika jibu lake.

Na kwa kuwa wanatumia dawa katika kuangamiza makonokono jambo ambalo dawa hizi zinaweza zikawa hatari hata kwa sisi binaadamu, Je, Mhe. Mwenyekiti, haoni sasa Mhe. Waziri, kuna haja ya kutumia *biological control* ya *Schistosomiasis* kwa kutumia wanyama wanaoitwa Chonjwe kwa sababu wanakula sana makoa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba arudie ile sentensi yake ya mwisho sikuweza kuipata, ile sentensi ambayo ina swali lenyewe.

**Mhe. Saleh Juma Nassor:** Mhe. Naibu Waziri nadhani hasikii kwa sababu ya hili zogo hili suala la *scientific* lazima watu wawe makini katika kulisikiliza, kwa kuwa Serikali inaondosha magonjwa mengi, na inamuondosha huyu konokono kwa kutumia madawa ambayo ameyataja kwamba huyu konokono yaani kowa hawa ambao ndio *intermediate host wa Schistosomiasis*, yaani ina maana ikiwa hapana kowa hapana kichocho tena katika nchi. Sasa badala ya kutumia madawa ambayo yataua kowa na kutuathiri sisi viumbe, basi kwa nini Serikali isitumie *biological control,* mradi ambao mimi tayari ninao mkobani kwa kuwatumia chonjwe.

Chonjwe ni wanyama fulani katika *design* ya fungo ambao ukiwaona katika maziwa au mito wanawala makoa wote, kwa hivyo makoa wote wanaangamizwa bila ya kutumia fedha nyingi za Serikali kama ilivyotumika kule kwa kutibia malaria. Sasa haoni sasa ishafika wakati kwa kutumia *biological control* kwa kuwatumia chonjwe ili kuweza kupunguza matumizi ya Serikali pamoja na hayo ma *-chemicals* yasije yakatuathiri hata sisi binadamu, hapo ndipo nilipo Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwanza namshukuru sana Mhe. Saleh Nassor Juma kutupa darsa zuri la kisayansi kama hili, lakini namuomba katika jibu langu namuomba huo mradi wa chonjwe asikae nao mkobani, ukiwa na mradi wowote hasa katika hii *system balance* maana yake kuna *predator in prey* yaani yule anayekula na yule anayeathirika anayeliwa. Kwa hivyo namuomba sana asikae nao mkobani, autoe huu mradi wa chonjwe mimi nitahakikisha nauwasilisha kwa wahusika.

Hivi sasa tuna timu kubwa sana ya watu watano mmoja akiwa ametoka Uingereza, mmoja Ujerumani, mmoja ametokea Swiss ambao wanaangalia ile *cycle* nzima ya *Schistosomiasis.* Sasa hao chonjwe mimi katika ziara yangu nilipokwenda Pemba sikubahatika kuwaona wala siwajui naomba nikiri hilo, lakini nakuomba Mheshimiwa wewe pamoja na Waheshimiwa wengine watakaokuwa na miradi yao yoyote basi wasiweke mikobani, kwa sababu wakiweka mikoboni humo haisaidii, haisaidii wananchi, haisaidii majimbo yenu, haisaidii wananchi wenu.

Naomba Mheshimiwa alete huo mradi wake, sisi tutakaa na wataalamu wetu tuangalie na tutashirikiana katika hilo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipatia fursa hii na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako ulieleza kwamba Serikali imechukua juhudi kubwa ya kuwa inashughulikia tatizo hili la kichocho liweze kutoweka. Je, katika juhudi hizo ambazo zilizofanyika kuna utafiti wowote ambao umefanyika ukaweza kuonesha mafanikio yaliyopatikana katika juhudi hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Naomba nimwambie Mheshimiwa kwamba ndio utafiti upo wa kuthibitisha kupungua maradhi hayo. Na pia upo utafiti uliofanyika pia wa jinsi ya kutoa elimu katika jamii lakini hiyo ni endelevu, yaani ni *continuous assessment* ambayo inaendelea, kwa

hivyo kila baada ya muda tunaendelea kufanya utafiti huo na upo utafiti wa tatu ambao unafanywa na University John Hopkins kutoka kule Marekani ambao unafanyika pale *PHL* kwa ajili ya konokono. *PHL* yaani *public health laboratory* iliyopo pale Pemba, nayo pia ni endelevu, kwa hivyo kuna tafiti kadhaa.

Kuna tafiti pia iliyofanyika ya watoto tabia zao na nitatoa hadithi ndogo tu Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nilipotembelea Pemba nilikwenda baadhi ya maeneo ambayo yameathirika zaidi kwa watoto kuoga pale, sasa kuna pahala pale panaitwa Kangagani kuna dimbwi moja kubwa nikakuta watoto wapo pale. Sasa watoto wale wanaogolea mmoja akatoka nje ya bwawa akaanza kukojoa na ule mkojo wake anaurusha kutizama unafika mbali kiasi gani na wenzake wakiwemo ndani, basi mimi pale pale nilisema Hamadi! Kichocho kinaendelea hicho, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa maelezo yake marefu mtaalamu Mhe. Saleh Nassor Juma alisema kuwa kwa kutumia dawa ya kuua makono kono wakati mvua imeshapita na maji hayatembei kwa kasi kubwa, na kwa sababu ile dawa ni sumu inaweza ikaleta matatizo kwa viumbe wengine wakiwemo binadamu wanaotumia maji hayo.

Swali langu ni kuwa, kwa sababu Mhe. Waziri, hili amelinyamazia kimya inaonesha ni kweli, swali langu ni kuwa, je, dawa hii inayotumika kwa kuua konokono ina maradhi gani kwa viumbe wengine. Na kwa sababu Wizara inatumia dawa hiyo kwa kuua makonokono ili kichocho kiondoke, na kwa sababu dawa ni sumu inaleta madhara, haoni Mheshimiwa iko haja ya kuharakisha na kushauriana vizuri na Mhe. Saleh Nassor Juma ili mradi wake huu uweze kuendelea kwa maslahi yetu na viumbe vyengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Nitaanza na (b ) hapana, naomba niseme tena kwamba ipo haja ya haraka sana kwa sabbu hii ni *natural process* ya kuwatumia hao chonjwe wanaowala wale konokono kwa kuwaondoa, kwa hivyo ipo haja ya haraka sana kufanya utafiti zaidi na hili nitalifuatilia kwa karibu ili kuhakikisha hii *biological system* ipo *balanced* inafanyika katika hii *natural process* badala ya kutumia chemical *process*.

Katika swali lako la (a) dawa yoyote ile inayotumika duniani dawa yoyote hata panadol ina *advantage* zake ambazo inakuonesha lakini huacha *side effect* zake ndogo huwa zinakuwepo. Kwa hivyo kwa dawa hii *chemical* inayotumiwa haiathiri viumbe vyengine lakini huacha *chemical* ambayo inaweza kuathiri mimea na iko *system* ya pale eneo lenyewe la kwenye dimbwi au kwenye maji yale, lakini mpaka sasa hivi dawa hii haina athari yoyote ya moja kwa moja kwa mwanadamu, lakini inayo athari katika *eco system* ambayo inatumika pale. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 65**

**Ujenzi wa Barabara ya Ole – Kengeja**

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman** – Aliuliza :-

Barabara ya Ole - Kianga hadi Kengeja imefanyiwa uchambuzi yakinifu muda mrefu sasa takriban miaka mitatu sasa, barabara hii ni muhimu kwa wananchi wanaoishi ukanda wa mashariki ambao unatoa mazao mengi Kisiwani Pemba.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** – Aliuliza :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 65 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kuwa Barabara ya Ole hadi Kengeja imeshafanyiwa uchambuzi yakinifu kwa muda mrefu, na ni muhimu kwa wananchi wanaoishi ukanda wa mashariki ambao hutoa mazao mengi Kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja yenye urefu wa km 35 tayari umeanza rasmi tarehe 01-09-2014. Mradi huu unafadhiliwa na *OFID* na ujenzi wake unafanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (*UUB*) na unasimamiwa na Kampuni ya *KAPSEL* kutoka Dar-es-Salaam. Mradi huu unatarajiwa kutumia jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 12, kati ya hizo Dola Milioni 1 ni mchango wa SMZ.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa sasa hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni usafishaji wa eneo lenye urefu wa km 5 ambalo limeanza Ole Kianga hadi Dodeani. Aidha, baadhi ya maeneo tayari kifusi cha mwanzo kimeshawekwa.

Aidha, kazi za upimaji wa eneo la Barabara zimekamilika kwa urefu wa 11km, na maeneo ambayo yamebakia yanaendelea kufanyiwa kazi siku hadi siku. Hata hivyo mradi umefanya ukarabati wa ofisi ziliopo Gombani ambazo zinatumiwa na msimamizi wa mradi huo.Kwa ujumla hatua za ujenzi wa barabara zimeshaanza na zinaendelea.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.
Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa barabara hiyo ishaanza tayari, na tayari baadhi ya miti ya watu ishakatwa ikiwemo minazi, mishelisheli na miembe na pia majumba ya watu yataangushwa.

Je, wananchi washalipwa fidia za mali zao, na kama washalipwa ni kiasi gani cha fedha kimetumika kulipia fidia hiyo, na kama hawajalipwa ni lini watalipwa fidia zao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, kama maelezo yangu ya awali yalivyosema kwamba barabara hii ina urefu wa kilomita 35. Eneo ambalo limesafishwa ni kilomita tano, eneo ambalo limepimwa sasa hivi limeshafanywa *survey* ni kilomita 11, katika hilo eneo la kilomita 11 fidia ya nyumba ambayo tunadaiwa ni takriban milioni 349 katika hizo hizo kilomita 11, tunadaiwa takriban shilingi milioni 89 kwa ajili ya miti.

Sera ya serikali ipo wazi, hatutovunja nyumba ya mtu kabla ya kumlipa fidia. Lakini miti tutaikata, tutaendeleza ujenzi wa barabara, tutalipa kadri ya upatikanaji wa fedha tutakaoupata.

Sote tuna lengo moja la kutaka kuleta maendeleo, kinachotukwaza hapa ni uwezo. Tukisema tusubiri tupate fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya miti kama vile ambavyo tunafanya kwa ajili ya fidia ya nyumba, tunaamini miradi hii mingi itakwama na watakaosumbuka ni sisi sisi wananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo nikusihi tu Mhe. Mwakilishi, kwamba tunadaiwa shilingi milioni 89 kwa ajili ya miti na hatujalipa hata shilingi moja. Tutalipa kwanza nyumba ambazo ni shilingi milioni 349, baadaye tutaendeleza ujenzi wa barabara, kadri ya hali ya upatikanaji wa fedha ulivyo ndivyo tutakapopunguza madeni kwa ajili ya vipando na miti ya wananchi.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali la nyongeza asubuhi hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana serikali yetu ya Zanzibar kwa juhudi yake kubwa inayofanya kwa kutuletea miundombinu ya barabara kwa wananchi wake, lakini nina masikitiko makubwa katika hii barabara inayopitia kwa Handhari, Mwanyanya mpaka Kisasi, barabara hii imeshatiwa kifusi mara mbili, hivi sasa inavyosema ni mara ya pili imeshatiwa kifusi lakini mpaka leo haijatiwa lami.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa niliyokuwa nayo, hivi sasa barabara ile imetiwa kifusi lakini inaumiza wazee na watoto kwa vumbi kubwa, linaweza kuwaletea madhara makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, hii barabara mara mbili ishatiwa kifusi naomba kujua gharama yake bei gani imetumia serikali kwa fedha hizi kwa kutia kifusi.

Pia naomba kumuuliza Mhe. Waziri, barabara hii itatiwa lami lini ili kuweza kuokoa fedha za serikali kupunguza gharama na hasara kubwa inayopata serikali.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, tulipofanya mabadiliko ya sheria inayosimamia barabara, tulifanya baadhi ya maeneo ambayo yote yalitujengea uelewa mpana zaidi. Jukumu la Wizara liko katika ujenzi wa barabara kubwa ambazo tunaziita *main roads* au *track roads*. Tukaelezana wazi kwamba majukumu haya ya kujenga barabara hizi za ndani yanaishia Halmashauri zetu pamoja na msaada ambao tunaupata za mfuko wa barabara, ingawa sio jukumu lao kimsingi lakini na wao pia wanachangia.

Sasa ombi hili ambalo anakuja nalo Mhe. Mwakilishi sisi kama Wizara msaada wetu mkubwa ni kutoa vifaa pamoja na wataalamu. Nimuombe tu ajenge ukaribu mzuri zaidi wa kufanya mashirikiano na wenzetu wa Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Sisi kama wizara tupo tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu na wenzetu halmashauri kama watakuwa na uwezo wa gharama kwa haraka haraka tunaweza tukasaidiana nao ili kuondoa usumbufu wa vumbi wanaopata wazee na watoto katika maeneo yale ambayo yamejengwa barabara ya kifusi kama vile Mhe. Mwakilishi alivyoeleza.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Ile barabara ya Ole - Kianga hadi Kengeja iwe na faida zaidi kwa wananchi wa vijijini ni lazima barabara hiyo iunganishwe na vijiji na miji yetu.

Je, Mhe. Naibu Waziri barabara hiyo imezingatiaje kuunganisha barabara ya Ole -Vikunguni hadi Wawi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Mwenyekiti, barabara hii ukiangalia maumbile yake haipo barabara ambayo imenyooka moja kwa moja ni barabara ambayo unajenga kilomita 11 unakutana na barabara nyengine iliyopo, unatoka kwa mfano ukitoka Ole, mpaka Vitongoji inaiishia pale, unapita Fidel- Castro nyuma huku *Airport* unajenga kipande kile, ukitoka hapo unaacha unakwenda zako mpaka unakamata barabara ya Pujini. Ukiacha ya Pujini unakwenda kukamata barabara ya Chambani, ukiacha barabara ya Chambani unakwenda zako mpaka Ukutini, ukitoka Ukutini unakwenda zako mpaka Kiwani, ukitoka Kiwani ndio unakwenda zako mpaka Tundamiti ndio unatokea Kengeja Skuli.

Kwa hiyo kila eneo lile kuna barabara pale kati ambayo inakuwa ina kiungo, kiungo ambacho unakisema wewe kipo eneo la *Airport* kwa upande wa Magharibi. Kwa hiyo tunaamini barabara hii kwa sababu inakwenda vipande kwa vipande tayari viungo vipo, lakini kama kuna haja na ulazima tunaweza tukaunganisha, lakini mradi wetu huu unakwenda vipande kwa vipande, haupo barabara ya moja kwa moja. Kwa hiyo kimaumbile kwamba tayari kuna vipande ambavyo vinaunganisha barabara nyengine kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

**Nam. 54**

**Kupatiwa Wafanyakazi wa Shirika la Umeme *Units* za Bure**

**Mhe. Ali Salum Haji** – Aliuliza:-

Tunawapongeza Shirika la Umeme (*ZECO*) kwa kuwapatia wafanyakazi wake *units* za umeme za bure kila mwezi.

a. Je, ni *units* ngapi za umeme wanazopatiwa wafanyakazi hao kila mwezi.
b. Ni kiasi gani cha pesa zinazotumika kwa *units* hizo.
c. Je, ni wafanyakazi wangapi wanaonufaika na neema hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 54 kama hivi ifuatavyo:-

(a) Jumla ya *Units* za umeme wanazolipiwa wafanyakazi ni 127,400.

(b) Fedha zinazotumika katika kuwalipa umeme wafanyakazi *units* hizo ni shs. 33,948,600.00.

(c) Wafanyakazi wote wa Shirika ambao ni 754 wanapatiwa posho ya umeme. Waheshimiwa Wajumbe naomba ieleweke kwamba wanapewa *units* hizi kwa sababu.

Ni sehemu ya maposho ya Shirika. Hii ilikuja baada ya Shirika kugundua kuwa wafanyakazi wakilipwa fedha za kulipia umeme wanakuwa hawalipi matumizi hayo ya umeme.

Lengo la kutoa posho hili ni :-

i. Kushajihisha wafanyakazi na kuleta ufanisi katika kazi zao za kutoa huduma bora kwa wateja.
ii. Kuzuia wimbi la wizi wa umeme kwa wafanyakazi wa Shirika hilo.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya ufafanuzi, lakini pamoja na hayo nataka nielewe kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, ina watoto wawili; mmoja Shirika la Umeme na mmoja ni Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Je, kwa upande wa (*ZAWA*) wafanyakazi nao wanapata msamaha wa kodi ya maji, na kama wanapata ni kiasi gani, na kama hawapati ni kwa sababu gani hawapewi na wao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hivi bado wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji hawajapewa posho wala kulipia huduma ya bure ya maji. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaandaa mpango huo. Kwa sababu kama tunavyoelewa kwamba bado Mamlaka ya Maji ipo katika harakati za kujiimarisha. Kwa hiyo tunajiandaa na tunategemea wafanyakazi hawa na wao baadaye watapewa posho hilo kama wanavyolipwa wafanyakazi wa Shirika la Umeme.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwa kuwa Mheshimiwa duniani mtu ukifika katika *stage* ya kuwa na *passport* ya *diplomatic* unastahiki kuheshimiwa.

1) Je, Mheshimiwa huoni iko haja kwa Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi na wao wakaweza kupewa *units* za bure.

2) Mhe. Mawaziri nyinyi kati ya wewe na waziri wako je, na nyinyi mnapewa *units* ngapi za bure.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti,

1) Swali lake linalohusu Waheshimiwa Wawakilishi kupewa *units*, hilo tunalichukua na tutalipeleka kwa Waziri na *Inshallah* tutakaa pamoja tukisha tutalijadili ili tuweze kuona vipi itakuwa.

2) Swali la pili naomba ulirejee kidogo

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Kwa kuwa wafanyakazi wanapewa *units* za bure je, Mhe. Waziri wa Ardhi na Makaazi, na Naibu. Waziri wa Ardhi na Makaazi, mnapewa *units* ngapi na nyinyi za bure.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za (SMZ):** Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa Shirika la Umeme wanapewa *units* wanazopata kama ni motisha kwa kazi ambayo wanaifanya kwa kulitumikia Shirika la Umeme. Kwa upande wa Wawakilishi na Mawaziri utaratibu umewekwa na Serikali wa kupewa posho maalum kwa ajili ya kulipia umeme katika Shirika la Umeme.

Imefanywa hivyo makusudi kwa sababu lile ni Shirika kila mteja anatakiwa alipie huduma ile. Sasa kwa upande wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yeyote yule ambaye anastahiki kupata huduma hiyo kuna posho maalum ambalo limeingizwa ndani ya mshahara wake ili aweze kulipia huduma hiyo. Ahsante sana.

## UTARATIBU

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, swali langu halikufahamika. Kwa sababu tulisema kuwa wafanyakazi wanapewa *units* za bure na tukazitaja zipo ngapi. Mimi nilichokusudia Waheshimiwa wenyewe husika na Idara na Naibu wake wanaoshika na idara wao wanapewa *unit* pamoja na lile posho wanalopewa serikalini, na wao wanapewa *units* ngapi za kuwa na wao ni motisha kama Waziri na Naibu, ni hivyo tu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe nafikiri Mhe. Waziri amejibu vizuri. Tukianza na Naibu Waziri amesema kwamba zile posho zao wanazostahiki kupewa kwa ajili hiyo kwa sababu kwamba hawapewi posho ndio wanapewa huo umeme, na Mhe. Waziri huku amejibu kwamba utaratibu wa Waziri na Naibu Waziri, yaani Wawakilishi posho zao au gharama zao za malipo ya umeme zimo ndani ya mishahara yao.

Naona hilo jawabu lipo *clear,* sioni kama kuna tatizo lolote hapo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Wewe ni Mwenyekiti, lakini unajibu swali la Waziri.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tuendelee, ahsante.

## HOJA ZA KAMATI

### Ripoti ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2014/2015

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaanza kuwakaribisha Wajumbe ili waendelee kuchangia kama ambavyo orodha inaonesha hapa. Kuna jambo naomba tufahamiane.

Jana wakati Mhe. Waziri wa Elimu alipokuja hapa kuwasilisha ile ripoti ya utekelezaji, ile ripoti badala ya kuwasilisha ripoti ya mwaka 2013/2014, iliwasilishwa ripoti ya mwaka 2014/2015. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri ili kwanza aweze kuwasilisha upya ile ripoti yake halafu baadaye tutaendelea na utaratibu wetu.

**UTARATIBU**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, mimi niliwahi kuchangia jana wa mwanzo, na leo Mhe. Waziri anarudia tena, je, na mimi nitapewa haki yangu ya Kanuni ya kuweza kuendelea kuchangia katika hoja ya sasa hivi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Tutalizingatia hilo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana sana kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha tena ripoti yangu badala ya ile niliyowasilisha jana, lilitokea kosa dogo la kutokuelewana kidogo. Kwa sababu ripoti niliyowasilisha jana niliyoletewa ilikuwa ya mwaka 2014/2015, wakati ripoti ile nilitakiwa kuwasilisha mwakani Mwenyezi Mungu akituweka hai.

Kwa hivyo nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa kufanya masahihisho hayo ili sasa niwasilishe ripoti ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, naanza sasa kuwasilisha ripoti hiyo.

Utekelezaji wa Maoni na Maagizo ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi.

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu.
Maoni na Maagizo.

Kamati imeshauri kulipa kipaumbele suala la ukaguzi wa elimu kwa kuwatengea bajeti inayofaa ili waweze kutekeleza kazi zao kwa mafanikio.

Ukelezaji: Wizara inajitahidi kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ili watekeleze kazi zao kwa ufanisi. Wizara imeongeza maafisa katika ofisi hiyo na imewapatia magari na vespa za kufanyia kazi ili kazi yao waweze kutekeleza kwa ufanisi.

Pili Kamati imeshiauri Wizara katika kukabiliana na tatizo la utoro katika maskuli yetu, Wizara ishirikiane na walimu na wazazi ili kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi.

Utekelezaji: Wizara ilikuwa ikiandaa vikao mara kwa mara na walimu wakuu pamoja na kamati za skuli ili kuhakikisha kuwa tatizo hilo linamalizika. Aidha Wizara imeanzisha mradi wa majaribio ya lishe kwa skuli tisa; tano Unguja na nne Pemba wenye lengo la kupunguza utoro kwa maskuli na mradi huo unaonekana unaleta faida kubwa.

Tatu, kamati inaagiza kuongezwa posho wakaguzi kwani wanafanya kazi nzuri na muhimu sana.

Utekelezaji: Wizara imelifanyia kazi suala hilo na litatekelezwa pindipo bajeti yake itakapoongezwa.

Nne. Kamati inaitaka Wizara kuwapatia jengo Ofisi ya Wakaguzi wa Pemba, kwani Ofisi wanayoitumia hivi sasa hairidhishi hata kidogo.

Utekelezaji: Ukweli, Ofisi ya Ukaguzi Pemba hairidhishi, Wizara ina mpango wa kuwakabidhi jengo la Maktaba wakati wowote maktaba inayojengwa itakapomalizika.

Tano, Kamati inaagiza kuwapatia usafiri Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ili aweze kutekeleza kazi zake vizuri.

Utekelezaji, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu Pemba, imepatiwa basi moja kwa ajili ya shughuli za ukaguzi pamoja na vespa nane kati ya vespa 20 zilizonunuliwa. Wizara itaendelea kusaidia Ofisi ya Ukaguzi kadiri ya bajeti yake itakavyoruhusu.

Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi. Maoni na Maagizo, Kamati inaagiza Wizara kuwa elimu ya maendeleo na ukaguzi wa watoto ipewe kipaumbele Serikalini ili wanafunzi wasomeshwe masomo haya yafuatayo. Elimu ya Afya, Elimu ya Ustawi wa Jamii, Kinga, Lishe na kadhalika.

Utekelezaji. Wizara imelipokea suala hili na kulifanyia kazi, mkazo mkubwa utawekwa katika elimu katika ngazi ya maandalizi kwa kushirikiana na wadau wengine.

Pili, Kamati inaagiza Serikali iandae mkakati maalum kwa maendeleo ya kukuza watoto yaani *Early Childhood Development framework* na washirikiane na wadau wote ikiwa ni pamoja na wazazi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara inayohusika na Ustawi wa Jamii na Watoto, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha.

Utekelezaji. Suala hili ni kipaumbele na Kamati pamoja na kuandaa semina, imeandaliwa Serikali kupitia wizara ya ajira, ustawi wa jamii, vijana, wanawake na watoto na Wizara ya Afya na *Resource Centre.*

Tatu, Kamati inashauri Idara ya Elimu ya Msingi na Maandalizi kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufanikisha kazi zake.

Utekelezaji. Fedha zinazopatikana ni kidogo kwa kutegemea Idara ya Msingi na Maandalizi fedha hazitoshi. Hata hivyo Wizara kwa kushirikiana na mashirika mbali mbali ya maendeleo imeweza kutatua changamoto mbali mbali za Idara ya Msingi na Maandalizi, changamoto hizi ni kama vile upatikanaji wa vitabu vya kusomea na kusomeshea kwa darasa la kwanza hadi la nne. Vitabu vya darasa la nne mpaka la sita vimo katika kumaliza uchapishaji.

Aidha ujenzi wa madarasa mapya takriban 230 yatakamilika ifikapo mwezi wa Aprili, 2015 pamoja na kuipa samani za vikalio. Walimu wote wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mtaala mpya wa elimu ya msingi.

Nne, Kamati inashauri kuwa dhana ya kushirikiana baina ya Serikali na Sekta binafsi iimarishwe.

Utekelezaji. Ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi umeimarishwa kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza elimu ya msingi.

Tano, Kamati inashauri Wizara kuwapatia walimu wanaofundisha Skuli za Maandalizi na Jamii posho la angalau shilingi 20,000 kwa mwezi ili kuwapatia motisha katika kazi zao. Jibu, hili halijafanyika kwani utaratibu huu wa ruzuku kuwapa posho walimu ni kinyume na Serikali.

Sita, Kamati inaitaka Wizara kujipanga vizuri katika kuhakikisha kuwa wanazipatia skuli za Unguja na Pemba madawati kwa ajili ya wanafunzi kuachana na utaratibu wa kukaa chini haraka iwezekanavyo.

Majibu: Wizara kwa kushirikiana na mashirika mbali mbali ya maendeleo ya elimu inahakikisha kuwa katika kupunguza tatizo la vikalio ujenzi wowote wa skuli au madarasa mapya umeandaa pia na upatikanaji wa vikalio hivyo.

Saba, Kamati imesikitishwa sana na tatizo la upungufu wa walimu katika skuli za msingi, hivyo kamati inataka Serikali kwa kushirikiana na Wizara kulipatia ufumbuzi tatizo hili kwani kuna idadi kubwa ya wahitimu waliomaliza mafunzo ya Skuli ya Msingi wamebakia bado hawajaajiriwa.

Utekelezaji: Ni kweli kuna idadi kubwa ya elimu wanaomaliza ngazi na cheti na hata Diploma ambao hawajapata ajira. Hata hivyo kwa ujumla elimu ya msingi haina upungufu wa walimu na ina walimu wengi hasa katika masomo ya sanaa, dini na kiarabu ila tu kuna upungufu kwa masomo ya sayansi na kwa baadhi ya Wilaya tu kama vile Micheweni inao upungufu mkubwa kwa walimu kutokana na walimu wengi kuhama katika eneo hilo, na wengine wanaoajiriwa kwenda huko wanakuwa wazito kuitekeleza na kuikubali ajira yao.

Nane, Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa na hatimiliki za maeneo ya skuli ili kudhibiti suala la uvamizi wa majengo na uharibifu wa majengo kwa skuli Unguja na Pemba.

Utekelezaji. Ni kweli kuna idadi kubwa ya walimu waliomaliza ngazi ya cheti na hata diploma ambapo hawapati ajira. Hata hivyo, kwa ujumla elimu ya msingi haina upungufu katika elimu ya sanaa, dini na kiarabu ila kuna upungufu katika masomo ya sayansi.

Nane, Kamati inashauri Wizara kuhakikisha kuwa na hatimiliki za maeneo ya skuli ili kudhibiti suala la uvamizi wa majengo na uharibifu wa majengo kwa skuli Unguja na Pemba. Jibu jitihada za kuhakikisha skuli zote zinapata hatimiliki ili kukuza kuzuia uvamizi na uharibifu mbali mbali unaoendelea zimechukuliwa kwa skuli zote za Unguja na Pemba. Wizara ya Ardhi, Nishati na Mazingira imepewa orodha kamili ya skuli zinazohitaji hatimiliki.

Idara ya Elimu ya Sekondari. Kwanza ya maagizo, Kamati imeshauri Wizara kutegemea fedha katika bajeti ya mwaka 2014/2015 Skuli ya Ufundi Kengeja kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa dakhalia ya wanawake.

Utekelezaji. Wizara imetenga jumla ya shilingi 300,000,000 katika kuimarisha elimu ya ufundi ikiwemo ujenzi wa dakhalia katika Skuli ya Sekondari ya Kengeja. Hata hivyo fedha hizo bado hazijapatikana.

Pili, Kamati inaiagiza Wizara kuipatia Skuli ya Ufundi Kengeja vifaa vya umeme ili wanaofundishwa wapate fursa ya kuvitumia katika somo lao la *practical*.

Utekelezaji. Vifaa mbali mbali kwa ajili ya *workshop* ya umeme kununuliwa ili viweze kuwasaidia wanafunzi mazoezi ya vitendo katika somo hilo.

Tatu, Kamati inaitaka Wizara kutoa ajira ya dereva kwa ajili ya kurahisisha shughuli mbali mbali katika skuli hiyo. Jibu mpaka sasa ajira ya dereva wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja haijafanyika, hata hivyo anatoa pia huduma za udereva pale ambapo anapata nafasi ya kufanya hivyo.

Taasisi ya Elimu Zanzibar. Maoni na maagizo, Kamati imeitaka Serikali kuipa Wizara ya Fedha kuiingizia katika fedha za bajeti zilizoidhinishiwa kwa matumizi ya taasisi ya elimu ili kuweza kufanikisha shughuli zake.

Utekelezaji. Taasisi inapatiwa fedha za ruzuku kwa wakati, hata hivyo fedha hizo hazitoshi katika kutekeleza kazi zao.

Pili, Kamati inashauri Serikali katika mipango yao waliojipangia na kujenga Ofisi mbali mbali za Serikali kuwagaia na kuwapatia kipaumbele Taasisi ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ujumla kwani ufinyu wa nafasi hizo ni changamoto kubwa kwa Wizara nzima.

Utekelezaji. Ushauri wa Kamati umepokelewa na unazingatiwa kulingana na uwezo wa Serikali katika mipango ya uendelezaji Ofisi.

Tatu, Kamati inashauri Wizara kuipatia taasisi ya elimu vitendea kazi ambavyo vitaendelea na kuhitajika katika shughuli hizo.

Utekelezaji. Wizara inajitahidi kuipatia taasisi vitendea kazi mbali mbali kwa kutumia fedha za bajeti ya Serikali.

Bodi ya Huduma za Maktaba. Maoni na Maagizo, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inaipatia Bodi ya huduma za maktaba usafiri wa uhakika ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Utekelezaji. Bodi imeipatia gari moja na taratibu zinaendelea za kununua basi moja kwa ajili ya huduma za maktaba.

Pili, Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kuipatia Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali na taasisi zake kwa ujumla fedha za kutosha na kwa wakati ili iweze kutekeleza maagizo yake.

Bodi ya Huduma ya Maktaba inaingiziwa fedha za ruzuku kwa ajili ya kulipa mishahara. Mazungumzo yanafanywa na Wizara ya Fedha kuongeza bajeti ya huduma za maktaba katika fedha zinazotolewa za ruzuku.

Tatu, inaishauri Bodi ya huduma za maktaba kuchukua jitihada za makusudi katika kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu kwa kusoma vitabu katika kuelewa kwani uelewa bado ni mdogo kwa wananchi walio wengi.

Utekelezaji. Katika kuwahamasisha wananchi kupenda kusoma vitabu, Bodi ya Huduma za Maktaba ina utaratibu wa kuendesha programu ya watoto ambao wanasimamia wanafunzi wa Skuli za Msingi. Programu hii inalenga kuwahamasisha watoto kupenda kusoma vitabu. Pia kupitia mradi wa *GPE* Serikali imepanga kuendesha *program* ya *Reading Tent* kwa *Mobile Library Program,* hizi zinalenga kuwashawishi watoto, vijana na wazee katika kusoma vitabu mbali mbali hapa nchini.

Nne, Kamati inashauri kuanzishwa kwa wingi maktaba ya jamii ili huduma zao ziweze kuwafikia wananchi kirahisi.

Utekelezaji. Jitihada hizo zinafanyika, katika mwaka 2014 Bodi ya Huduma ya Maktaba imeanzisha maktaba katika mji wa Wete tarehe 18/12/2014.

Tano, Kamati inashauri kuendelezwa kwa mpango wa Maktaba ya visanduku katika skuli mbali mbali ili huduma za kusomea vitabu zipatikane kwa ufanisi wa hali ya juu.

Utekelezaji. Maktaba ya kisanduku vimeongezwa vitabu zaidi tumenunua kupitia kwa *Global Patnership for Education.* Hadi hivi sasa skuli 55 za msingi zimefaidika na mradi huu, zikiwemo 20 kwa Wilaya za Kaskazini A, 20 Wilaya ya Micheweni, 10 Wilaya ya Wete na 5 za Wilaya ya Mjini. Katika mwaka huu wa fedha 2015 Serikali inatarajia kuendeleza skuli 10 katika Wilaya za Kati Unguja.

Sita, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Maktaba ya Pemba kwani ni dhahiri kuwa huduma ya maktaba kwa upande wa Pemba itakuwa bora na uhakika na utapatikana ufanisi mkubwa.

Utekelezaji. Pongezi tumezipokea.

Saba, Kamati inashauri kutolewa mafunzo ya ukutubu kwa maskuli ili waweze kutoa huduma zao kwa utaalamu unaotakiwa. Bodi ya Huduma za Maktaba inaendesha mafunzo mbalimbali kwa wakutubi kwa skuli mbali mbali za Unguja na Pemba.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar SUZA. Maoni na maagizo, Kamati inashauri kukamilishwa kwa baadhi ya majengo katika Chuo Kikuu cha Taifa ili majengo hayo yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

Utekelezaji. Kazi za usambazaji wa umeme zimekamilika na kazi ya ujenzi wa mitungi ya kuhifadhia gesi katika maabara zimo katika hatua ya kukamilishwa kazi hiyo.

Pili, Kamati inashauri uajiri wa wahadhiri wa kufundisha *course* zote zinazotolewa chuoni kuondokana na tatizo la kuwa na walimu wa muda.

Utekelezaji. Chuo kimefanikiwa kupunguza wahadhiri wa muda kutokana na kuajiri baadhi ya wahadhiri wapya na kurejea kutoka masomoni baadhi ya wahadhiri wa zamani na kuendelea na muda wa kufundisha.

Tatu, kamati inakitaka Chuo Kikuu cha Taifa kutenga fedha maalum kwa ajili ya ununuzi wa vitabu hasa vile vitabu ambavyo vinatumika kwa kozi za masomo yanayotolewa chuoni.

Utekelezaji: Chuo kinatenga bajeti kwa ajili ya vitabu vya mwaka. Kwa mfano, mwaka huu wa fedha bajeti ya vitabu ilitolewa ni shilingi mia moja na thalathini na tano milioni na mwaka jana bajeti iliyotolewa ilikuwa ni shilingi hizo hizo mia moja thalathini na tano milioni, kwa ajili ya kununua vitabu hivyo baada ya kutenga bajeti. Chuo kinaendelea na ununuzi wa vitabu hivyo kila mwaka mpaka vitakapomalizika.

Zaidi ya bajeti ya chuo kwa mapato yake ya ndani kupitia miradi mbali mbali chuo kinanunua vitabu kwa ajili ya masomo mbali mbali yanayohitajika katika chuo. Kwa mfano, kupitia *SIDA* chuo kilinunua vitabu 92 mwaka jana na kupitia Mradi wa Benki ya Dunia chuo kimenunua vitabu 2256 miaka mitatu iliyopita.

Nne, kamati imeshauri Chuo Kikuu cha Taifa kubuni njia nyengine za kujiongezea mapato kwa lengo la kuendesha shughuli zake za chuo kwa ufanisi.

Utekelezaji, ushauri umepokelewa na unafanyiwa kazi. Chuo kimebuni njia nyengine za kuongeza mapato kwa kuandika nyaraka za mradi na kuwasilisha kwa wahisani mbali mbali ambao wanazihitaji nyaraka hizo. Chuo kimepata mashirikiano makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa wageni.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ingawa matayarisho ya waraka huu yalikuwa ni ya lazima na ya haraka sana tumefanya kazi hii kucha, lakini nimejitahidi kuwasilisha kazi hii ipasavyo. Ahsante sana.

**UTARATIBU**

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii jana ililetwa na tukaambiwa imeletwa ripoti iliyokuwa sio, kwa bahati nzuri baada ya kuwa sio imefanyiwa iliyokuwa ndio, na mimi Mheshimiwa kama ni mjumbe kumbe nimepotoshwa nimechangia ripoti iliyokuwa sio. Sasa na mimi unipe haki yangu japo dakika tano niweke na mimi *hansard* vizuri ili niweze kuichangia hii ripoti iliyokuwa sahihi. Kuninyima haki yangu Mheshimiwa ni kwenda kinyume na Kanuni. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe nafikiria umesema kwanza *concern* yako na kiti kimekwambia kwamba italizingatia hilo, sasa hujakataliwa katika hilo. Naomba uheshimu

utaratibu baadae tutakupa nafasi utachangia, lakini kwa vile tumeshamtaja mjumbe mwengine muache aendelee halafu na wewe utapewa nafasi.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataallah* kwa kutuamsha tukiwa hai na wazima na kuturuzuku neema zake tukaweza kukutana hapa kuendelea na shughuli zetu.

Pili, Mhe. Mwenyekiti nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia mjadala huu wa hoja ya ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii na Wanawake pamoja na wizara tatu ambazo zinasimamiwa na Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wote ambao wamewasilisha ripoti zao hapa zenye maelezo juu ya hoja mbali mbali ambazo ziliibuliwa na kamati. Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu sasa naomba niende katika mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza nirejee lile ambalo nililisema katika mchango wangu wa mjadala wa kamati ya kwanza kuwasilisha ripoti yake hapa ambayo ilikuwa ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Nalo ni kwamba Mhe. Mwenyekiti ukiangalia mtiririko wa maagizo mengi ambayo yametolewa hasa yale yanayohusu mambo ya msingi sana kufanyiwa kazi, utakuta majibu ya mawaziri yanafanana tangu wale watatu wa mwanzo na hawa watatu wengine, na kinachofanana Mheshimiwa ni ufinyu wa bajeti.

Sasa Mheshimiwa niliuliza na majibu ya mawaziri katika kamati iliyotangulia yalikuwa ni hayo hayo kwamba mapato yetu ni kidogo, tunahitaji kutizama upya bajeti yetu. Mhe. Mwenyekiti, mimi hili binafsi nalikataa la kuniambia hoja ya fedha za washirika wa maendeleo kwamba ndio tatizo kwa mambo yanayohusu shughuli zetu za kawaida, kwa maana ya matumizi mengineyo (*other charges*) siwezi kulikubali Mhe. Mwenyekiti.

Ningeifahamu kwamba bajeti tuliyokuwa tumeipitisha mwaka jana ingelikuwa ina fungu linalotoka fedha za washirika wa maendeleo kuingia katika utendaji wa shughuli zetu za matumizi ya kawaida, ningeelewa. Lakini hakuna kitu kama hicho, sasa unakuwaje na hoja ya upungufu wa fedha za washirika wa maendeleo kwamba ndio hoja ya kujibu kwamba jambo fulani halikutekelezwa katika shughuli ambazo zinahusu shughuli za kawaida za serikali yetu.

Na zaidi kama nilivyouliza na naendelea kuliuliza tena Mhe. Mwenyekiti bado mimi naona sijapata jawabu tunababaishwa tu na serikali, kwamba hizi shughuli za kawaida zinahudumiwa na mapato ya ndani, mapato ambayo tunaambiwa serikali kila siku inaongeza mapato (ukusanyaji wa mapato). Katoa mfano, kwamba tunaambiwa mwaka 2010 *ZRB* kwa mfano ilikuwa inakusanya bilioni kumi na saba, sasa hivi imefikia pahala inakusanya mara moja nilimsikia Mhe. Rais akisema bilioni ishirini na tisa kwa mwezi.

Sasa najiuliza Mhe. Mwenyekiti bilioni ishirini na tisa mara kumi na mbili kwa mwaka ni kiasi gani? Kwa nini hata katika hizo hali mbaya iliyokuwa katika serikali iliyopita, ilikuwa mambo ya msingi yanakidhiwa kwa shilingi bilioni kumi na saba kikomo ambacho wamekifikia mwaka 2010. Leo serikali hii imefika bilioni ishirini na tisa bado tuna tatizo kubwa sana la utekelezaji kuliko ilivyokuwa hapo kabla, kuna tatizo gani katika serikali hii?

Mimi nasema bado serikali ina swali la kulijibu katika Baraza hili. Fedha zinazokusanywa zinakwenda wapi? Na hii ni moja tu Mhe. Mwenyekiti ya *ZRB,* kuna fedha vile vile zinazotokana na makusanyo ya *TRA* na vyanzo vyengine vya mapato ya ndani. Sasa tunapopewa taarifa za kuongezeka ukusanyaji wa mapato halafu zikawa haziendi sambamba na uingizwaji wa fedha katika mawizara ili kukidhi haja ya kuwahudumia wananchi. Na fedha hizi Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema si fedha kama zinatoka mbinguni, zinatoka kwa hao waliokusudiwa, wananchi wanyonge, masikini wa nchi hii. Huyu ndiye anayekwenda kununua mchele, akienda akinunua bati, akienda akinunua saruji, akienda akinunua chochote katika nchi hii anachangia kodi katika serikali hii. Msingi wa kodi dunia nzima ni kurudisha huduma kwa wananchi.

Kwa hiyo, nasema bado Mhe. Mwenyekiti nikisoma ripoti zote za mwanzo narudi pale pale ufinyu wa bajeti, ufinyu huu unatokana na nini hebu tupatiwe jawabu Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi zinazokusanywa za wananchi masikini, wanyonge, tunawakamua, zinakwenda wapi? Mimi bado sijapata jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, na katika hilo nije na suala maalum ambalo limo katika agizo Nam.3 la kamati kwa Wizara ya Elimu kuhusiana na tozo ya bandari ambayo ilikuwa inahusu kwenda kuhudumia madeski (vikalio).

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma humu agizo la mwaka huu linaonesha kamati imegundua kwamba fedha zile hazipelekwi, na Mhe. Mwenyekiti, wanaingiza kutokana na makisio yaliyowekwa. Kwa mfano, kama ni bilioni mbili kwa mwaka, tunaambiwa humu walichoingiziwa ni milioni mia saba, na katika pahala ambapo naamini mimi makisio hayawezi kwenda ovyo ni katika eneo hili. Kwa sababu bila shaka makisio yanafanywa kwa kutambua idadi ya wasafiri ambao wanasafiri baina ya visiwa vyetu na Dar es Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa mimi leo nasema, narejea tena, nasema kama Baraza hili halikuwa makini kila siku tutapelekeshwa ovyo na serikali. Tulishawishiwa katika bajeti kuongeza shilingi elfu katika nauli, nasema tena hizi ni fedha tunawakamua wananchi si kama zinatoka mbinguni! Ni shilingi elfu anayochangia mwananchi katika tiketi yake, mwananchi mnyonge, tukaambiwa hapa lengo lake ni kwenda kununua vikalio ili kuwaondoshea tatizo watoto wetu suala la kukaa chini. Sasa leo fedha zinapokusanywa na Wizara ya Fedha halafu zikawa hazipelekwi kunakohusika, Mheshimiwa huku Wizara ya Fedha kuna nini? (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi mtazamo wangu ni kwamba Wizara ya Fedha imekuwa ni kama vile shimo kubwa kazi yake kumeza tu. Kwa sababu suala hili hili liko katika tozo nyingi zinazotozwa makusudi kwa kuhudumia jambo fulani halafu hazifikishwi kunakohusika. Sasa kama tulisema tumeongeza hizi kwa mwananchi mnyonge ili kuhudumia upatikanaji wa vikalio halafu zikawa hazipelekwi kunakohusika Wizara ya Elimu, tuambiwe ile mantiki yake kweli na kwa nini ikija bajeti inayokuja wawakilishi tusimame kila aliyesema hii tozo iondolewe kwa sababu haihudumii ilichokusudiwa. Kilichonipa tabu mimi ni kwamba serikali inalidanganya Baraza la Wawakilishi na inalitumia vibaya Baraza la Wawakilishi kuongeza kodi kwa wananchi masikini, halafu malengo ya kodi yale hayaendi kuhudumia kile kitu ambacho kimekusudiwa. Hii si kuwatendea haki hata kidogo wananchi wa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti.

La pili Mhe. Mwenyekiti, niseme kuna suala la mikopo ya elimu ya juu. Zimetolewa ripoti vile vile humu suala la malalamiko. Na mimi narejea Mhe. Mwenyekiti kila siku ya Mungu inayopita Wawakilishi huwa tunapokea ujumbe wa simu kupigiwa simu na wanafunzi waliokuwa katika vyuo vikuu mbali mbali wakilalamikia kutokuingiziwa fedha.

Mwaka jana nakumbuka tulipokuwa tukipitisha bajeti hapa vile vile tulisimama kidete tukaondosha fedha katika baadhi ya maeneo tukasema hizi zikaongezee mfuko wa kuhudumia elimu ya juu. Lakini bado wanafunzi hasa mchukulie mwanafunzi huyu yuko nje ya Zanzibar kwa mfano, yuko pahala ugenini, sote tumepitia baadhi yetu humu katika vyuo tunajua mazingira ya kusoma yanavyokuwa. Leo unapokuwa humuingizii fedha kwa wakati unategemea huyu atasoma vizuri. Mwanafunzi anayekaa katika dakhalia anadaiwa pengine pesa ya dakhalia, kama anakaa katika nyumba ya kukodi anadaiwa pesa ya kukodi, hakijui chakula chake, hana pesa ya vitabu, unafikiri mwanafunzi huyu atakuwa na tija katika kusoma kwake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa linalotukwaza ni kwamba mimi ningeelewa angalau tungesema kwamba kuna wizara fulani haziingiziwi fedha lakini kipaumbele kinatoka wizara fulani, lakini kila wizara inayokuja inalalamikia suala lile lile. Sasa hizi fedha zinazokusanywa zinahudumia kitu gani? Afya wanalalamika, elimu wanalalamika, Katiba na Sheria wanalalamika, Ustawi wa Jamii, Wanawake wanalalamika, wamekuja Utumishi wa Umma na Kazi wanalalamika, wamekuja Tawala za Mikoa, sasa kila mtu analalamika tu katika serikali, hizi fedha zinazokusanywa zinakwenda kuhudumia nini Mhe. Mwenyekiti? Mhe. Mwenyekiti, mimi bado napata mashaka makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine kuna agizo limetolewa hapa kuhusu skuli mpya zilizojengwa za sekondari. Kamati imeziona kwamba skuli hizi ni mbovu na suala hili liliwahi kuja hapa katika Baraza la Wawakilishi katika kikao kilichopita tu. Sasa unajua mara nyengine mtu anaweza akakosea lakini akatusaidia, huku kukosea jana kwa Wizara ya Elimu mimi kumenisaidia sana kuja kutupa maelezo ya ripoti ya mwaka huu kabla ya mwaka uliopita.

Niliona katika hayo maelezo yaliyokuwa yamekusudiwa mwaka huu kwamba wizara inasema nimeona kama ni hivi kweli kama itakuwa si kuondoshwa njiani basi jambo zuri sana kama tayari wana majibu ya mwaka unaokuja, kwamba wanasema zitatengwa shilingi milioni mia moja kwa skuli ya Dimani kwa mfano. Sasa najiuliza fedha hizi anabeba nani gharama Mhe. Mwenyekiti. Skuli kama zinajengwa zilikuwa na mikataba ya ujenzi, na bila shaka zilikuwa na kiwango fulani kwamba kifikiwe katika ujenzi ule, anapokuwa mkandarasi hakufikia kiwango kile kwa nini wizara tena itoe shilingi milioni mia moja kwenda kutengeneza skuli ambayo mkandarasi kafanya uvundo katika ujenzi? Mbona kuna picha inajitokeza ya kufichiafichia watu maradhi.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, tafsiri yangu itakuwa yeyote aliyehusika katika kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skuli zile alikuwa anajua anachokifanya ndio maana ilipotokezea matatizo sasa anachukua bajeti tena ya wananchi wanyonge na masikini wa nchi hii anakwenda kulipia ubovu ambao umesababishwa na mkandarasi mbovu. Na si skuli moja tu, hapa imetajwa Dimani lakini tulisema hapa siku ya kuulizwa maswali kikao kilichopita, kwamba takriban skuli nyingi sio zote ni nyingi katika zilizojengwa. Ni mbovu kwa sababu ya wakandarasi ambao walichaguliwa, na

hicho tunasema mara nyingi katika masuala ya *procurement* iwe ni utoaji wa huduma iwe ni ujenzi serikalini, hii imeoza kwa kuwachukua wakandarasi wabovu wanatuingiza katika matatizo kila pahala.

*Airport* limekaa lile pale *white elephant*, skuli ndio hizi kila unapokwenda kuna jengo la Wizara ya Fedha pale mpaka leo Tibirinzi limekaa kama ukumbusho sijui wa kitu gani, kila unapokwenda tunavuruga fedha za wananchi masikini halafu tunakuja kusema kwamba tuna ufinyu wa bajeti. Hivyo ndio mnazisaga pesa za wananchi wanyonge wa nchi hii Mhe. Mwenyekiti, hakuna nidhamu ya matumizi ya fedha, hakuna nidhamu ya usimamizi wa matumizi ya fedha. Ndio maana nasema leo unachukua milioni mia moja unazipeleka kwenda kuhudumia ubovu wa skuli ambayo imefunguliwa mwaka jana tu, huyu mkandarasi aliyetufikisha pale tunamuacha kwa sababu gani, huyu anayewalinda hawa ana maslahi gani? Tukisema na yeye ni sehemu ya maamuzi yale kwa sababu na yeye ana chake tutakuwa tunakosea nini Wawakilishi wa wananchi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, pamezungumzwa katika agizo Nam. 5 la kamati suala la kusomesha upya mitaala na vitabu na pameelezwa kwamba kuna vitabu tayari vya masomo matano vimepatikana. Lilonishtua moja katika vilivyoorodheshwa humu ni vitabu vya Kiingereza. Ningependa Waziri akija aje anijibu vitabu vya Kiingereza hivi ni vile ambavyo katika bajeti ya mwaka jana nimekuja navyo hapa vilivyokuwa vimejaa makosa kuanzia mwanzo hadi mwisho, ndio vitabu vile?

Lakini ningependa pia aje anisaidie kwamba vitabu vile baada ya kutokezea yale wale waliohusika wamechukuliwa hatua gani? Au ndio basi mtindo wa serikali hii ni kwamba "*funika kombe mwanaharamu apite*" kwamba anakuja hapa tunaibua mambo tunasema tukiondoka hapa hakuna linalokuwa na ndio maana watu wanaendelea kila siku na utaratibu ule ule kwa sababu hakuna hatua zinazochukuliwa tunalindana tu Mhe. Mwenyekiti. Anayeumia mwananchi mnyonge, masikini anayetoa fedha zake kuichangia serikali hii. Naomba maelezo kwenye hilo Mheshimiwa Waziri akija.

Jengine Mheshimiwa vile vile naomba maelezo kuhusiana na ajira ya walimu. Hili halikutajwa katika ripoti ya kamati ingawa yamezungumzwa masuala ya upungufu wa walimu na haja ya kuajiri wapya. Mimi nasema kuna walimu wameajiriwa mwaka jana mwezi wa Oktoba, kuna walimu 68 wa sayansi waliajiriwa, hawa mpaka leo wanadai mshahara wao ule wa mwezi wa kwanza hawakulipwa na mpaka leo hawajalipwa. Naomba akija Waziri anisaidie kuna tatizo gani kuhusu walimu hao?

Mhe. Mwenyekiti, haraka haraka naomba niingie katika Wizara ya Afya. Katika wizara hii narejea pale pale tatizo linarejea lile lile nililolizungumza, kwamba nao wanalalamikia ufinyu wa bajeti. Nikisoma hii ripoti ya kamati kila hospitali kuanzia Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja na zile hospitali ambazo zimeambatanishwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa maana ya idara, Hospitali ya Mwembeladu, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, zimetajwa humu Hospitali ya Makunduchi; imetajwa Makunduchi kwa sababu naamini ndio iliyotembelewa lakini naamini pengine kila *cottage hospital;* iwe ya Makunduchi, iwe ya Kivunge, iwe ya Micheweni, iwe ya Vitongoji.

Pia mumetajwa humu vituo vya afya kwa mfano cha Kojani na Ukutini vilivyotembelewa kote kunazungumziwa tatizo kubwa la upungufu wa dawa, mbali ya matatizo mengine yametajwa ya vifaa na huduma nyengine lakini nalizungumza hili la dawa ambalo limetajwa katika ripoti hii katika kila eneo. Sasa narudia pale pale ikiwa mambo ya msingi kama si kipaumbele cha serikali kila wizara ikija hapa inasema haikuingiziwa fedha, narudia tena hizi fedha za wananchi zinakwenda wapi?

Mwaka jana tuliambiwa hapa katika bajeti kwamba serikali imekusudia kuondosha utegemezi wa wahisani katika suala la dawa na umekuja utaratibu wa kutenga bajeti ili kununua dawa wenyewe. Sasa kama hiyo ndio *solution*, ufumbuzi mbona kamati yetu ya Baraza inayokwenda kukagua kwa niaba yetu inakuja kutuorodheshea humu kwamba kila ilipokwenda kuna tatizo la upungufu wa dawa na hizi ni dawa za msingi tu, sio zile dawa za mambo makubwa makubwa. Hizi ni dawa za msingi, *basic medicines* zinakosekana katika vituo vya afya na hospitali zetu. Naomba maelezo katika ule mpango tulioambiwa mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine limezungumzwa hapa jana suala la Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ingawa naamini mimi kwamba hali hii iko katika maeneo mengi sana, suala la usafi wa majengo yetu. Mimi nimesema sana katika michango yangu mingi hapa na nikawahi kutoa mfano kwamba unakwenda hospitali pale palipobandikwa kibango pakawekwa karatasi kwamba weka hospitali yako katika mazingira ya usafi penyewe pameng'ang'anaa, pale palipobandikwa lile tangazo hasa.

Juzi yameonekana rasmi mpaka vyombo vyetu vya habari vimeonesha, mpaka wakubwa ikabidi kwenda kutembelea kule. Sasa najiuliza hawa wenye mamlaka ya kusimamia hili nasema Mhe. Mwenyekiti nasikitika sana, tunayazungumza haya, hapa najiuliza mimi anayechukua kwa niaba ya Wizara ya Afya nani? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi watu walikasirika sana, na baadhi ya Wajumbe wenzangu huku wakawa wao ndio watetezi wa serikali kwamba serikali hii haijashindwa. Mimi nauliza kwamba watendaji wako wapi huo ukaimu wa kuundiwa hapa hapa sisi unatutia mashaka. Kaimu anapokuwa Waziri hayupo, waziri yupo tunapishana naye hapo nje Mwenyekiti, huyu ndio wale wababaishaji kwamba hapa hapa tunataka kuundiwa undiwa mambo, Waziri yupo, Naibu Waziri wapo ndani ya nchi, wako wapi hapa tunajadili utendaji wa wizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena hatuko makini na mimi narudia kwa yale yale mtu akasirike lakini ukweli utabakia ukweli. Kuna tatizo la msingi katika serikali katika kuratibu shughuli zake na ndio maana nikawa na haya.

Kwa hivyo, mimi nasema hali ya hospitali ni mbaya sana, lakini nasikitika sitaki kuendelea nimekuja kushtuka ghafla kwamba hakuna watendaji wenyewe. Kwa hivyo, siwezi kuzungumza na hewa Mhe. Mwenyekiti, naomba kukaa kitako, ahsante.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Mweyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii asubuhi hii kuchangia maoni haya. Lakini pia niseme kwamba Mhe. Ismail Jussa kakaa kitako kutokana na uchungu wa mawaziri na manaibu waziri kuwa hawapo hatujui tumueleze nani,

lakini kwa vile limeshatajwa jina langu itabidi na mimi niendelee hivyo hivyo sijui kama atakayechukua ni hiyo hewa au kitu gani kitakuja kuwaeleza hao mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na maoni na maagizo yaliyopendekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Afya katika ripoti ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kitengo cha maradhi ya kuambukiza. Katika maradhi haya niseme pamoja na kamati kutoa maagizo yao lakini pia yapo maradhi ambayo yanaambukiza, lakini hayajaeleweka. Kwa hivyo, niseme kwamba wizara ingechukua fursa zaidi kuwapeleka madaktari wetu nje kusoma ili kuona hali halisi ya maradhi yale ambayo yamejitokeza na bado hayajajulikana, ili kuweza kuchukua utaratibu kwa madaktari hawa kufanya bidii na kusoma ili kurudi hapa kuja kueleza wananchi hali hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije katika kitengo cha kupambana na maradhi yasiyopewa kipaumbele. Kwanza niulize maradhi yasiyopewa kipaumbele ni maradhi gani. Lakini pia niseme katika ukurasa huu wa pili namba 1 panaposema; "wizara huchukua jitihada za kuelimisha jamii umuhimu wa kutumia dawa za kichocho ambazo gharama yake ni kubwa lakini jamii imekosa muamko wa kuzitumia dawa hizo".

Mhe. Mwenyekiti, niseme hii ni kweli, lakini pia niseme kwa maelezo yangu na pia wale ambao wanapewa huduma hii ya kupita kuwaeleza wananchi kutumia matumizi haya ya dawa ya kichocho, pia niseme ni tatizo kubwa. Kwa sababu wengine wanapewa dawa zile ambapo bado hawajatia kitu tumboni, na dawa zile mtu anazila na hatimaye kumlewesha. Hili ningeomba likatolewa elimu zaidi kwa watu wetu ili kuweza kuwaeleza wananchi wetu kuzitumia dawa hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa nne unaosema Kitengo cha Matibabu ya Macho. Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kinahitaji kupewa kipaumbele zaidi, kwa sababu wengi wetu sasa hivi ni wagonjwa wa macho na hiki kitengo kinahitaji kupewa msaada zaidi ili kukiendeleza. Lakini niseme kitengo hiki pia kiongezewe madaktari zaidi katika hospitali yetu ya Mkoani ili kufanya kazi kwa ufanisi, kwa sababu pale madaktari ni kidogo wanahitaji kuongezwa na kufanya kazi kwa ufanisi.

Pia katika Hospitali ya Mkoani kuwapunguzia gharama wananchi wetu kwenda Hospitali ya Wete kutafuta matibabu. Hili naomba Mhe. Waziri alielewe kwamba kitengo hiki kipewe kipaumbele zaidi ili kiweze kuhudumikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Baraza la Dawa, Tiba Asilia. Juzi hapa Mhe. Naibu Waziri alituelezea amepata madawa mazuri na amefahamu jinsi ya mpatakuva na dawa nyengine za mzalia nyuma, lakini tukimuangalia hapa kumpa maelezo yetu yeye hayupo, ili kumpa zaidi yale maelezo ya dawa nyengine na kuweza kuzitumia na kuzifuatilia. Sasa maelezo haya tutampa nani wakati wao watibabu wa dawa asilia ambazo zinaweza kuwatibu wananchi na pia kuwaendeleza wakawa wazima kwa dawa hizi. Lakini tukiangalia Naibu Waziri hayupo, Waziri hayupo, tumpe nani maelezo haya Mhe. Mwenyekiti na watibabu wapo wa dawa hizi za asili ili kufuatana nao na kuweza kuwaeleza hizi dawa zinatumikaje na asili yake ilianzaje mpaka kufikia hatua hii.

Mhe. Mwenyeki, kwa hivyo niseme kwamba kuna umuhimu wa kuwafuatilia hawa wataalamu wa dawa hizi za asilia. Kwa sababu dawa hizi zipo na ningemuomba Mhe. Naibu Waziri au Mhe. Waziri wawafuatilie watu hawa ambao ni waganga zaidi wa kienyeji kuweza kuelewa kuna dawa fulani hii inatibu hiki na kuna dawa fulani inatibu hiki, hapa nadhani wanaweza kupata utaratibu wa pamoja wa kuweza kuzinufaisha zile dawa na kuweza kutibu watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo katika kifungu cha kwanza kinasema, "Kamati inaitaka wizara kuishajihisha jamii kushiriki kikamilifu katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili zipate ufumbuzi".

Hapa naunga mkono wizara, lakini pamoja na hayo ipo haja ya sisi wazee kukaa chini na watoto wetu wa kike na wa kiume kuwa karibu nao ili kuwaelezea nini maana ya ubakaji na nini maana ya ubakwaji. Suala hili litatupunguzia sana mzigo kwa watoto wetu.

Pia niseme kwamba, kuepusha vigenge vya watoto wetu wanawake na wanaume kuwa pahala pamoja kuchanganyika wakati ambao sio wa kufanya kazi pamoja, wakati wa kufanya kazi mtawaachia lakini kuna wakati ule ambao watoto wameshatoka skuli ni lazima wazee tuwe nao na sio suala hili kuiachia serikali pekee, lazima na sisi wenyewe tuwe makini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia umasikini nao unachangia, umasikini unachangia kutokana na asilimia kubwa kuwa ni masikini hawana uwezo wa kujikimu. Kwa hivyo, niseme kwamba nalo watoto wetu na wazee wengine huweza kurubuniwa kutokana na suala hili la udhalilishaji. Lakini pia kuwa karibu na watoto wetu ni kuwaepusha pia na maradhi ya UKIMWI. Kwa hili niseme kwamba ni muhimu kuwa na watoto wetu karibu ili kuwa nao pahala pamoja kuwaepushia matatizo hayo ya ubakwaji na hasa ukiangalia wakati huu umezidi, licha ya kupiga kelele kwamba siku zote tunapiga kelele kuhusu suala hili la ubakwaji lakini bado kila uchao suala hili linajitokeza kwa kasi kubwa.
Kwa hiyo, nawaomba wanawake wenzangu tukae pamoja na watoto wetu kuwaelezea hii hali halisi ambayo hivi sasa kila uchao unaanza kujitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wizara hii ilikuwa ni tofauti na tulivyojipanga na kupewa namna nyengine ya kabrasha. Kwa hivyo, niitake tu wizara hii kuna mishahara ya walimu 159 Pemba warejeshewe mishahara yao, kwani kutowalipa ni kuwarejesha nyuma walimu hao na kuwavunja moyo walimu ambao ndio tegemeo letu. Naomba hili wizara iliangalie kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwa upande wa bodi basi iangalie wanafunzi ambao wanahitaji mikopo ili kuwapatia mikopo hiyo na kuweza kuendeleza shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme kwamba walimu wanachelewa kupewa huduma za likizo, tokea mwaka 2012 huduma ya likizo kisiwani Pemba bado hawajalipwa. Namuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwa makini ili kuepusha mizozo na watu wetu.

Baada ya hayo niseme ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia angalau machache katika maagizo ya kamati hii ambayo iko mezani. Kwanza kabisa naomba niwashukuru mawaziri kwa kutoa taarifa zao na pia nimshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa kusoma taarifa ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza naomba nianze na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, naanza katika Idara ya Mikopo. Naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa na pia nimpongeze Mkurugenzi wa idara hiyo kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifuatilia kwa karibu nimeona kwamba idara hii inafanya kazi zake vizuri, inatoa elimu vizuri kwa walengwa, inatoa mikopo na shughuli zao zinakwenda vizuri. Wanakwenda kwa utaratibu mzuri na kabla ya kutoa mikopo kwanza wanatoa elimu kwa walengwa halafu wanawaelekeza kila kitu. Kabla ya hapo pia wanakwenda kuangalia wale ambao wameomba mikopo ni mradi gani wanauombea na unakidhi kwa kile ambacho wamekiomba au laa.

Sasa mimi naomba niwapongeze sana Mkurugenzi na wafanyakazi wake kwa kufanikisha hili kwa utaratibu mzuri. Vile vile namuomba Mhe. Waziri aiangalie vizuri idara hii ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha ni kwamba Idara ya Mikopo inafanya kazi zake vizuri lakini jengo wanalofanyia kazi halikidhi haja hata kidogo. Jengo lenyewe liko ndani wananchi wanapata shida sana kulifikia jengo hilo, halafu pia halina nafasi wala halikidhi hata kidogo mahitaji ya ofisi yao. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri na hili aliangalie, kuwatafutia jengo ambalo litakidhi na wataweza kufanya kazi zao kwa utulivu na usalama zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Idara ya Ushirika. Idara ya Ushirika huwa naichangia sana na ninasikitika sana kuwa idara hii katika jengo ambalo wanafanyia kazi nalo pia lina matatizo mno. Kipindi hiki cha mvua ambacho kinakuja Idara ya Ushirika hivi sasa tayari wana kite katika nafsi zao, kwa sababu katika idara ile kuna nyaraka mbali mbali, vifaa mbali mbali, kuna mafaili, kuna vitendea kazi, lakini wakati wa mvua lile jengo linavuja kupita kiasi. Sasa iko hatari kubwa ya kupoteza kumbukumbu nyingi za ofisi ya ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa yake imesema kwamba tayari Idara ya Ushirika wameshaipatia jengo Mazizini, sasa ninachokiomba wizara ifanye juhudi za makusudi ili kuweza kuwatengenezea jengo hilo ikiwezekana katika bajeti inayofuata wapewe kipaumbele Idara ya Ushirika kutengenezewa jengo ambalo wataweza kuhamia na kufanya kazi zao kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende Wizara ya Afya. Kwanza naomba nianze na Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali ya Mnazi Mmoja wameweka kitengo cha ulinzi kwa ajili ya hospitali. Hili si jambo baya ni jambo jema, lakini sasa lengo la idara na kitengo kile kinavyofanya kazi ni tofauti kabisa. Kwa hivyo, naomba Idara ya Mnazi Mmoja labda iwaweke kitako viongozi wale wa kampuni na iwape hasa zile kazi zao ambazo zimewaweka pale. Kwa sababu wale askari Mhe. Mwenyekiti wananyanyasa sana wananchi ambao wanakuwa na

wagonjwa pale hospitali. Mimi nina mfano hai, mfano mgonjwa anahitaji dawa, mzee wa mgonjwa anapewa karatasi kanunue dawa anaporudi pale na dawa zake mlangoni hawampitishi, wanamwambia mwite mgonjwa aje achukuwe dawa pale mlangoni na mgonjwa yuko kitandani ataweza kweli kuja pale.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, kile kitengo sio kibaya lakini wafanye utaratibu mzuri, wanafika kugombana, wanafika kupigana na wananchi pale. Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama mtu atatoka tu awe anapenda kwenda Hospitali bure bure kama atakuwa hana tatizo. Mwananchi anakuwa na tatizo la ngonjwa wake halafu akifika pale anakuta tatizo la wale askari mlangoni, unamzidisha tatizo mara mbili zaidi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba wizara kupitia hii Idara ya Mnazi Moja waweke utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naiomba Wizara hii ya Afya kupitia hii Idara ya Mnazi Mmoja Hospitali, Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mmazi Mmoja ni chafu, chafu kupita kiasi. Ninaomba au nina ushauri kwa Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwamba ukiacha ile kampuni ya Ulinzi waweke na Kampuni ya usafi, ili kuweza kuendeleza usafi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, inafika wakati mgonjwa anakwenda kule Hospitali mfano wodi ya watoto. Wodi ya watoto, mtoto anakuja pale anaumwa lakini mtoto aliyechuchuka alikuwa mkubwa mkubwa kidogo akeshapata nafuu huwezi kumzuia na kumpakata lazima atataka atembee tembee apipe mule, lakini mle anamopita anaweza akapona maradhi yale aliyoyaendea lakini akapata maradhi mengine akaondoka nayo, akenda nayo nyumbani, nina mfano hai.

Mhe. Mwenyekiti, nilikwenda kumuangalia mtoto Hospitali siku ambayo amelazwa nikienda nikakuta sehemu pamemwagika sijui kama uji, sijui kitu gani chini. Wiki nzima nakwenda Hospitali nikirudi bado uji ule au chakula kile kimebakia pale hakikuzolewa, hakikufagiwa wala hakikusafishwa. Utaratibu wa usafishaji katika wodi ya watoto hamna kabisa kabisa, hawafagii hawasafishi.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na Kampuni ya Ulizni iweke na Kampuni na usafi kwa sababu ma-*orderly* wetu hawafanyi kazi.

Nimekwenda katika Wodi ya wazazi kumtizama mgonjwa. Mhe. Mwenyekiti, kile kitanda kile chote kimezungukwa na mabui mabui, hawasafishi. Naishukuru sana Wizara ya Fedha ama Wizara ya Afya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inawaingizia pesa nyingi sana kwa mwezi. Lakini pesa hizo sijui zinafanya nini, Hospitali chafu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Hospitali ya Mnazi Mmoja kama wanashindwa kuwasimamia wafanyakazi na ma-*orderly* kufanya kazi vizuri katika wodi zao basi Hospitali itafute na hii Kampuni ya Usafi, ili iweze kusafisha kwa sababu Hospitali ni pahali nyeti kabisa, unakwenda na maradhi unarudi umechukuwa maradhi mengine, kwa hivyo naomba sana hilo. Lakini "Mnyonge mnyongeni haki yake Mpeni".

Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara hii hii ya Afya naomba kuipongeza sana Wizara kwa kutengenza chumba cha *ICU* kipya nadhani kikimalizika kitakidhi haja. Kwa hiyo, na hilo naomba kusifu Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda kwenye Hospitali ya Makunduchi. Hospitali ya Makunduchi ina changamoto nyingi ambazo humu wameziandika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Wizara iangalie Hospital ya Makunduchi ina changamoto nyingi. Changamoto ya kwanza ni upungufu wa wafanyakazi. Hospitali ya Makunduchi inatakiwa iwe na *Nurse- midwife* saba (7) kwa wakati mmoja. Lakini kwa ushahidi yuko *Nurse-midwife* mmoja (1). Kuna siku idadi ya wagonjwa inapanda siku nyengine inashuka hebu fikiria kuna siku inatokezea wagonjwa wanajaa atafanyakazi vipi *nurse* yule 1 katika Hospitali ile. Kwa hivyo, naomba Wizara ya Afya iangalie hospitali ya Makunduchi.

Mhe. Mwenyekiti jengine kwenye taarifa wamesema kwamba kuna upungufu wa nyumba za daktari. Ni kweli unamuhamisha mfanyakazi unampeleka Makunduchi kufanya kazi kwenda na kurudi mjini ni tatizo, lakini pia na akienda pale anakosa nyumba ya kukaa, kuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za madaktari.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na mradi wa *ADB* ulikuwa unajenga Vituo vya Afya pamoja na nyumba za daktari. Lakini kwa bahati Wizara ya afya sijui walipanga vipi na mipango yao ilikuwaje hata wakawa hawakuliona hili. Lakini naomba kama utatokezea mradi mwengine au ifanye juhudi ya makusudi Hospitali ya Makunduchi kujengwe nyumba za madaktari kwa sababu Hospitali ni kubwa na Hospitali ambayo inatumika Mkoa mzima wa Kusini. Kwa hiyo, kutokuwa na nyumba za madaktari ndio kunaletea usumbufu na kupunguza nguvu ya kufanyakazi kwa fanyakazi wa Afya Hospitali ya Makunduchi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Uzio Hospitali ya Makunduchi haina Uzio, naomba kwa sababu lile eneo la Hospitali kama nilivyosema kwamba ni eneo nyeti. Hospitali kuna vifaa mbali mbali; kuna mambo mengi anaweza akatokea mtu tu labda pengine ana tatizo na mtu kapata maradhi kalazwa pale itakuwa rahisi usiku watu wamelala kwenda kuingia na kumuhujumu kwa sababu hakuna Uzio na hakuna Ulinzi wa kutosha. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba katika bajeti inayokuja Mhe. Waziri hili ulipe kipaumbele, Uzio wa Hospitali ya Makunduchi ujengwe.

Jengine bado niko Hospitali ya Makunduchi kuna tatizo la upungufu wa vifaa na dawa. Hospitali ya Makunduchi ni Hospitali ambayo inakuwa na wagonjwa wengi na ina mambo mengi. Lakini sasa kuna upungufu wa dawa, vitendea kazi na dawa hakuna, inafika wakati anakuja mgonjwa pale ma-*nurse* wanashindwa kumhudumia kwa sababu hakuna vitendea kazi wala hakuna dawa.

Halafu hapo hapo kuna upungufu pia gari ya kubebea wagonjwa, anakuja mgonjwa wanashindwa hawana dawa, hawana vifaa vya kumshughulikia wanataka kumleta mjini wanashindwa kwa sababu pia kuna tatizo la gari ya wagonjwa na mafuta ya gari ya kubebea wagonjwa kuleta mjini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na hilo Mhe. Waziri aliangalie kwa sababu kwenye kamati nao wameliona na mimi kwa kuwa ndio katika maeneo yangu pia hilo nimeliona.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, katika hiyo hiyo Hospitali ya Makunduchi kuna uhaba wa Maabara walionayo ni ndogo kazi zao nyingi. Kwa hiyo, naomba na hilo pia liangaliwe. Mimi

kwa leo ni hayo tu ambayo nimekusudia kuchangia, kwa hivyo nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Na mimi nitambakishia zangu 10 vile vile nadhani 20 zinaweza zikamtosha.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu sana naomba nitumie fursa hii kufanya mambo yafutayo.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai mpaka sasa hivi na kutupa uwezo wa kuweza kuchangia hizi hoja zilioko mbele yetu. Hii ni hazina kubwa aliyotupa Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru kwa sababu kuna wenzetu wengine sasa hivi kuingiza pumzi na kutoa ni tabu wanatumia mashine, wengine sasa hivi kaburi zao zinachimbwa.

Sasa sisi kutoka nyumbani hadi hapa bila ya kushikiliwa na kuanza kuchangia mambo mazito kama haya, hii ni hazina kubwa aliotujaalia *Allah* na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwennyekiti, jengine ninalohitaji kulifanya kabla sijaanza mchango ni kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kunipatia mimi fursa, tumo wengi humu lakini ukaona na mimi unipatie. Hili nadhani si jambo la hivi hivi lakini ni mapenzi halisi kwangu na hivyo nasema ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Sasa kabla sijaanza mchango nimnukuu mwanafalsafa mmoja maarufu ambaye kwa sasa ni marehemu ametwambia "msema kweli hukimbiwa na marafiki zake siku zote, sitochelea kusema kweli kwa kuogopa upweke wa kitambo nikajinyima ushirika wa milele baada ya kushindikana kwa uongozi" mwisho wa kunukuu Shaaban Robert 1957.

Aidha, ningependa nimnukuu vile vile mwanasiasa mgongwe ambaye ni marehemu mzee Tuntemeke Sanga alisema kwamba " Nguvu za Kamati za Bunge ndio Nguvu za Vikao vyenyewe vya Bunge" huyu ni bwana Tuntemeke Sanga 1998 kabla hajafa usemi huu aliutoa.

Sasa Waheshimiwa nimelazimika kutoa hizi nukuu mbili kuona kwamba kamati zetu zina tatizo hata ripoti zao wameshindwa kufanya kwa kina hizi taarifa zetu za kamati pamoja na kwamba wana uwezo hawa Wajumbe wa Kamati zote. Wana uwezo kila Kamati ninayoiangalia ina watu waliobobea katika mambo ya sheria, kuna watu waliobobea katika mambo ya taaluma mbali mbali, katika mambo ya sayansi ya siasa. Lakini kamati zinashindwa wakati mwengine kwenda *deep* katika kazi zake kwa sababu ya mambo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza Kamati zetu hizi wakati tunatoa taarifa ambazo tunatakiwa tuzisome leo hii Afisi ya Spika haiko tayari kutuwezesha kufanya kazi vizuri. Sisi juzi moja tulikuwa tunataka kwenda kuangalia *Environmental Degradation* iliyoko katika kisiwa cha Matumbini na bahari ilikuwa haipitiki kwa vidau ambavyo tumezoea kusafiria, taarifa hiyo mngeipata hapa nyinye wenyewe mngekionea huruma kile kisiwa cha Matumbini. Lakini tukashindwa kufika

kwa sababu upepo mkali na serikali haikuweka boti ya nguvu kidogo kutupeleka pale. Sasa watu wanakodiwa helikopta, mimi ni mtaalamu sana katika mambo ya Mabunge.

Kamati za Bunge hizi Mhe. Mwenyekiti, zinafanya *throughout the year* wanafanyakazi Kamati za Mabunge. Sisi katika siku katika siku 365 na robo za mwaka tunafanya siku 50 kwa wingi, si dhani kama zinatimia, hili ni tatizo ambalo kwa kweli nimelazimika dibaji hii niianze kwa sababu wakati mwengine wataalum wakiziangalia kwa kina taarifa zetu na wananchi wakizisikiliza wanaweza wakaziona zina mapungufu kwa sababu serikali haituwezeshi. Hata miswaada tunayoitunga.

Mhe. Mwenyekiti, Mahakamani wao wana nafuu, hii serikali kila wakati wanajisafirisha wao kwenda kufanya utafiti, sisi wakati tunatunga sheria hapa tunabanya banya na miswada yetu inayokuja haina upembuzi wa kina. Hivi juzi wakati tunataka kutunga ule mswada ya Maadili ya Viongozi tulitaka na tulitajiwa nchi nyingi zenye sheria ile za Ulaya, zikatajwa tukasema kwamba aah tunataka kwenda hapo Ghana tu kuangalia wenzetu uzoefu wao katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha sana achilia mbali Ghana pale Micheweni hatukuwezeshwa kwenda, sheria inapita hapa hivi hivi tu wakati mwenzetu muhimili mwengine wa Mahakama hakimu anatoa hukumu ana *site reference* kama inahukumiwa China hivi, inahukumiwa India hivi na inahukumia hapa hivi, ndio anatoa hukumu. Sisi sheria ile zaidi ya hapa mji wa Unguja Mjini na pale Kisonge tukipata hatuna pengine popote tunapopata. Mambo haya vipi na kila siku serikali inakwenda Uengereza, Marekani, wakirudi Marekani Japan, sie kwenda kufanya utafiti wa kina hatuwezeshwi basi tusilaumiwe na wananchi, mnaotusikia huko kwamba kamati zetu hizi wakati mwengine zinakosa mambo, zinakosa mambo nyeti kabisa kwa sababu Afisi ya Spika haituwezeshi kabisa, hivi ninavyokwambia mie nadaiwa nauli.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuja kuupitisha huo mswada ambao tumeshaupitisha hapa, nilikopa nauli kwa Shirika la ndege mpaka leo nauli ile sijalipwa huku napigiwa simu kweli mswada ule unajadilika. Unapitika mswada huo, hivi sasa hata nauli yao sijailipa. Nakaa hapa humu mwa jirani zangu siwezi hata kukaa hoteli sasa, ilimuradi sisi tunafanyakazi naona naona tu.

Sasa katika hili wananchi watakapotuona wasije kutudadisi kwamba hatuna uwezo katika kutayarisha taarifa, wasije kutuona kwamba sheria zetu zina tatizo ni kwa sababu Afisi ya Spika haituwezeshi kufanya *feasibility study* tukaweza kupitisha mambo makubwa makubwa kama haya, tunataka sana. Sisi watu wanatwambia aah nyinyi mnataka safari tu, hatutaki safari kama ni safari mie nimeletewa tiketi *up and down* na *visa* nimeshagongewa nimeiuza kwa mashaka.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sisi safari tunazo nendeni mkaangalie *passport* yangu kuna masafari tele na hata moja sijalipiwa na hili Baraza, tunataka tukasome sisi tuwezesheni tukaangalie nchi nyengine tuwaletee taarifa nzuri hapa Barazani, tuwaletee miswada mizuri ya kina lakini hatuwezeshwi.

Hivi sasa nina deni la kamati mpaka sasa nadaiwa huko, hotelini, humo kwenye shirika la ndege nadaiwa. Haki ikichelewa kutolewa Mhe. Mwenyekiti, ni sawa sawa na kuwa haikutolewa kabisa, mimi si mwanasheria lakini nasikia wanasheria wakisema hivyo na haki na wajibu ni vitu vinavyokwenda sambamba. Sasa niende kwenye mswada Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nawapongeza wenyeviti wote wa kamati waliowasilisha kamati zao, wamewasilisha kwa kina na kwa utulivu na umakini wa hali ya juu mno. Sasa tatizo nililokumbana nalo ni kwamba kutokana na baadhi ya mambo yanasonga hayakufanyiwa tafiti za kina nataka uone nianze na hospitali ya Mnazi Mmoja.
Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja ule ndio uso wa nchi maana ingekuwa ni kiganja tu tungekitia mfukoni kikawa hakionekani. Lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja ni uso wa nchi tunategemea sisi Wazanzibari pamoja na wageni ile Hospitali, wanaitegemea. Lakini tatizo liliopo pale kwanza ameshasema yule mama pale kwamba hali ya usafi hairidhishi hata chembe, laiti ingelikuwa kamati inapewa nafasi hii kamati inayohusika na mambo ya afya wakaenda wakafanya tafiti katika Mahospitali mengine ya Rufaa, basi nakuhakikishia kwamba taarifa yao wangeiita kwamba hospitali ile haina kiwango, ile ya Mnazi Mmoja.

Mimi nilikwenda Al-Rashid Hospitali hivi karibuni iko pale Dubai nikaona tabu kujisaidia maana nilishikwa na haja nikataka kwenda chooni, nilisema hiki ni choo au nishapelekwa chumbani kwa watu, kumbe ni choo! usafi uliomo kumbe choo sikuwa nimeingia kwenye vyumba vya wagonjwa. Choo tu nikaogopa kujisaidia kwanza mpaka nikauliza, nikatoka lakini hiki ni choo, ndiyo nikaambiwa ndicho, jisaidie tu. Sasa hospitali Mheshimiwa ya Mnazi Mmoja, mimi nilipita pale nilikuwa naogopa kupitia lifti yao, nikapita kwenye ngazi ninapanda juu nikakuta *blood sheed*, yaani kama matonge tonge ya damu. Nikasema sikukaa kule juu, kupita tena nikasema labda huyu mama alipatwa hapa na matatizo, lakini kupita tena baada ya karibu saa nzima nipo kule juu, niliporudi pale mambo yale yapo.

Sasa kwa mimi mwenyeji *okay* nitavumilia ingawa kichefu chefu kilizidi, nilipofika chini kule lakini sasa wageni je, ni tatizo Mheshimiwa. Kama ni suala la bajeti Waziri hana aje hapa aombe pesa, ikiwa ni ajira amuombe Mhe. Haroun Ali Suleiman kule Ofisi yake ili apate watu wa kusafisha, hili tatizo.

Mheshimiwa tuje katika *mortuary*. Mheshimiwa *mortuary* pale ni hifadhi ya maiti. Kuna maiti kwa sisi tuliopo hapa nikipata tatizo mimi nikishaekwa pale wanaweza wakaja jamaa zangu wakanipeleka, wakanitoa haraka haraka kunipeleka hapa Mwanakwerekwe nikazikwa au waliopo Pemba ikiwa watapata uwezo watanitia kwenye ndege nikazikwe Mkomani kule. Lakini kuna wengine ni wageni wanakaa pale siku nne, tano au wiki mbili. Haina uwezo *mortuary* ile. Maana nimeshawahi kuingia mimi nilikuwa kwenye kamati, unakuta maiti wamekunjwa hivi, yaani almuradi haina kiwango ile *mortuary*. Sasa mimi ninadhani katika hili Serikali iangalie.

Halafu kutokana na kwamba ndani ya taarifa hii ya kamati hii haikuonekana, lakini changamoto ni kwamba kulikuwa na mpango wa hospitali kuzi-*up grade* kuzitoa za *cottage* kuzifanya kuwa za Wilaya. Haikuzungumzwa kwenye kamati. Ninaamini kwa sababu ya mashaka pengine na wao walikuwa wakidaiwa nauli walikuwa hawakufika kule Vitongoji. Ile hospitali haijenda hata *step* moja kutoka *cottage* kuelekea huko Wilaya, hatujaiona kwenda. Tatizo ni nini?

Ninafikiri kama Waziri akija akatujibu na haya mambo ya Hospitali ya Kidongo Chekundu, siku hizi matatizo yamekuwa mengi Mheshimiwa, vijana wanatumia unga, kuna matatizo ya maisha mazito watu yanawapa uchizi wakati mwengine, kazidiwa maisha ijapokuwa hatumii unga. Mimi ninadhani kuna haja ya kuiboresha ile hospitali yetu nayo ikaweza kujitegemea.

Aidha, kuna kile Kitengo cha Mifupa katika Hospitali yetu ya Rufaa Mnazi Mmoja. Mheshimiwa Kitengo cha Mifupa ndiyo hakiridhishi kwa sababu hakuna *specialist*. Mimi ninadhani Serikali iwaombe hawa vijana wanaosoma hawa kwa sababu labda hawataki kuchukua hii kozi, wawaombe waweze kusoma mambo haya. Sisi kule huwa tunaanguka sana mikarafuu. Leo ukija hapa ukishaanguka mkarafuu unataka huduma wataalamu hapana. Mimi ninadhani katika hili Serikali ilione nalo.

Mheshimiwa *ICU* kongwe kule. Kwanza niipongeze Serikali kwa kujenga ile *ICU* mpya, lakini vile vile na huku tunahitaji huduma ya *ICU*. *Nurse* mmoja kule kuhudumia ni tatizo. Mtu akishakuwa mahututi anatakiwa kila pahala ashughulikiwe. Sasa naomba ikiwa ni kwa sababu..., vyuo tunavyo vinatoa, vinavyozalisha kama Mbweni hapa, sijui ni sababu gani inayosababisha kuwa na upungufu angalau *clinical officers* pamoja na madaktari pale.

Mheshimiwa sasa niende katika Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu nimeangalia sana kwa sababu ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nimeangalia hawa mafunzo ya amali hawana changamoto wao. Kwenye taarifa huku ya kamati sikuiona hii, hizi changamoto za watu wa mafunzo ya amali. Lakini mimi kama mimi nikipita pita huko vyuo naona changamoto.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwakilishi una dakika 5.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa watu wa mafunzo ya amali wana matatizo makubwa. Changamoto kubwa wanazo kwa mfano, hivi karibuni kuna walimu walifanya ziara ya mafunzo nchini Iran kule, wakaahidiwa kupatiwa *out fit allowance* na maduhuli mengine. Wamekaa kule karibu mwezi mmoja, walimu kutoka mafunzo ya amali hapa Unguja na wale wa Pemba wamechanganyika kwenda Iran. Mpaka leo hii hawajapewa maduhuli ya *sample* yoyote.

Sasa ile ni haki yao ingawa sikuiona kwenye changamoto, lakini walimu wanahitaji haki zao Chuo cha Mafunzo ya Amali, wameandika kwa Katibu Mkuu, wameandika wapi na wapi lakini Serikali imeziba masikio. Ile ni haki yao hata nyinyi wakubwa mukisafiri munapeana maposho chungu nzima huko. Je, wale maskini za Mungu, walikuwa hawawezi kufika hapa wakakopa wakavua yebo-yebo, ikabidi wapate buti na mashati. Wamekwenda kule kwa pesa za kukopa.

Niendelee hapo hapo kwenye mafunzo ya amali kuna changamoto nyengine. Kwa mfano Chuo cha Mafunzo ya Amali kule Fidel Castro, pale Pemba bado kuna uharibifu wa vifaa, wamedai wajengewe uzio pale miaka kadhaa hadi leo hii hata maana yake kusemwa katika taarifa haimo, hata taarifa za Waziri hatupati. Mambo ni kimya tu hivi hivi, kimya kimya mwaka umalize. Sasa sijui mambo haya mpaka lini.

Mhe. Mwenyekiti, twende sasa katika walimu 159 wa Pemba ambao wale kwa kweli mishahara yao imekatwa. Ile ni dhulma na mfalme hatakiwi kumdhulumu raia wake. Mimi ninadhani kwamba mufanye kila mbinu wale walimu walipwe, ni haki yao na sioni sababu kwa nini hawalipwi.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani musiwavunje moyo walimu wetu hawa. Hawa ndiyo wanaoufinyanga udongo ukawa chungu, ukawa kikaango, ukawa kikombe. Sasa tukija tukimkasirisha mfinyazi basi tutakuja lilia gae. Mimi ninadhani tujitahidi hawa walimu tuwape mafao yao kusudi wapate moyo wa kutufinyangia watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika elimu ya maandalizi na msingi hapa. Kama kuna watu muhimu sana katika nchi hii basi ni wale walimu wa maandalizi na msingi. Wale walimu wana shida. Mimi nimesomesha karibu miaka ishirini lakini sikuthubutu hata kusogea darasa la sita kwa sababu watoto wadogo siwawezi. Leo darasa la sita lenye watoto karibu miaka kumi na tatu na nne, nilikuwa sithubutu kusogea, ninawaogopa watoto wadogo.

Hawa wanachukua vinyaa-nyaa vile vidogo vidogo, wanafanya kazi kubwa zaidi. Leo Serikali inashindwa ati kuwalipa angalau posho la shilingi elfu ishirini. Hii ni aibu kubwa kwa Serikali yetu jamani, mcheza kwao hutunzwa, hawa walimu wanavisomesha vitoto vidogo sana vina kazi sana. Wewe tukikuletea, ninahakikisha Mheshimiwa yeyote tukimpa watoto wanne tu awakamate tangu asubuhi mpaka saa sita, basi atapata *hysterical case.* Leo mwalimu mmoja yule anakaa na vinyau nyau vile ishirini au ishirini na tano. Tuwaoneeni huruma jamani. Kweli Serikali sijui skuli za jamii hamuzisaidii lakini hamuwezi hata kutoa sadaka. Maana basi kutoa sadaka kwa raia wake ni dhambi? Tuwasaidieni hizo shilingi elfu ishirini wale.

Mhe. Mwenyekiti, halafu hawa walimu wanaosomea mambo ya kusomesha watoto wadogo, hawana chuo. Chuo wanachokitegemea ni pale Skuli ya Maandalizi ya Saateni, kama ninavyokumbuka hadi hii leo. Kwa nini Serikali haijengi eneo maalum kwa ajili ya walimu wale wa watoto wadogo wadogo. Kwa nini Serikali haifanyi hivyo, leo tunawagandamiza tu kwenye ile skuli ya pale Saateni.

Mhe. Mwenyekiti, tuwatafutie pahala hawa wasomee na wakishasomea *diploma* ya mambo ya watoto wadogo wadogo, wasome tena diploma ya ambao ya watoto wakubwa wakubwa wapate digrii, almuradi kitu kama hiki, *academical up heed* wale.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Wizara ya Wanawake na Watoto sasa. Kasema hapa kwamba mambo nimeangalia maagizo kwamba kamati inataka wizara kuishajihisha jamii kushiriki kikamilifu katika kutoa ushahidi wa kesi za udhalilishaji ili zipate ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea na kazi zake za kuhamasisha. Mimi ninadhani Wizara isiendelee kuhamasisha kwa sababu mimi nilikuwepo katika Kamati ya Wanawake hii ya nyuma, nilikuwepo tukamkutia mtu kwenye kituo cha mkono kwa mkono Chake-Chake, watu wapo tayari kutoa ushahidi, kesi haikufikisha Mahakamani.

Mtoto wa Mfikiwa pale katika jimbo langu, kadhalilishwa mtoto wa miaka sita na jamaa mmoja anajulikana, watu wapo tayari kutoa ushahidi. Leo tunaambiwa watu hawapo tayari kutoa ushahidi. Mambo hayo vipi. Tusidanganyane bwana, watu wapo tayari kutoa ushahidi lakini kesi kufika Mahakamani ndiyo tatizo. Tatizo lipo wapi. Naomba kamati sasa muendelee kupembuapembua, mujue tatizo lipo wapi. Huyo aliye na hilo tatizo ndiyo tumpeleke Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo haya kwa heshima kubwa naomba niunge mkono taarifa za kamati ingawa majibu ya Serikali ni ya kulengalenga tu mengine. Lakini ninaunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Sasa tunampa nafasi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk dakika zake kumi baadae Mhe. Ashura Sharif Ali, jitayarishe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wala mimi sina sehemu kubwa sana, nina sehemu mbili tu na hiyo pengine dakika nyengine nitamgaia na mwenzangu.

Kwanza nianze na suala la Mhe. Mwenyekiti alipokuwa akiwasilisha hapo, alikuwa anawasilisha kwa masikitiko makubwa sana suala la mishahara ya wale walimu wetu. Mimi naomba niulize swali. Hii mishahara iliyokuwa imekatwakatwa mpaka leo hawajapata. Nani aliyekuwa mkataji kati ya Wizara yenyewe ya Elimu au Wizara ya Fedha. Hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, pili kwa sababu gani hata ikafikia mwaka mzima hawa watu mpaka leo kwenye ripoti hii hawajalipwa fedha zao. Hapa nimeona niulizie na ikiwa tukimtambua, ninataka Mhe. Waziri wangu wa Elimu awe wazi, aeleze kama jana mheshimiwa wangu mmoja hapa aliposema kama hahusiki yeye, twende kwengine. Sasa na yeye ninamuomba na yeye awe wazi aeleze wapi, na tukimjua Baraza hili litatoa hukumu kwa mujibu wa sheria na Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa ripoti ya kuwa tumeinuka kiuchumi na tunakushanya si chini ya bilioni 35 kwa mwezi. Kama nitakosea nitapewa *corrections* kwa sababu ulimi hauna mfupa. Lakini humo humo kati ya 33 na 35 bilioni kwa mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti yetu sisi ina-*run* katika milioni 700. Sasa watu wanaojua hesabu, hebu angalieni hapa, zinakwenda wapi pesa za wavuja jasho walipa kodi hata leo tunaambiwa bajeti finyu.

Mhe. Mwenyekiti, hatupo *serious* katika masuala ya kuwafundisha watoto wetu, kuwapa elimu inavyoonesha tu, tunawapa mzigo bure Wizara ya Elimu. Kwa sababu wanahangaika vya kutosha, lugha yao finyu na Waziri mwengine kama alivyojipanga hapo, yote inakwenda eneo hilo hilo bajeti finyu. Sasa mimi ninashangaa sijui munaambizana hapo au vipi, lakini tuchukulie ndiyo kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mjumbe alisema hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuwa watu wanalalamika, mimi zaidi ya *message* ya tano zimeshaniingilia hapa sasa hivi, kwa kweli watu hawajalipwa fedha zao. Mhe. Mwenyekiti, kuna wengine wamepewa mikopo na mpaka leo hawajalipa na wao. Lakini niseme kuwa wenzetu huko Bara na wao wanatusaidia katika kutupa mikopo hii.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili suala linasikitisha sana, tunasaidiwa kupewa elimu ya juu mikopo lakini wanafunzi wengine hawarejeshi. Lakini na sisi hapa tuungane na lugha ile ile ya kusema bajeti finyu. Hatupo serious na masuala Mhe. Mwenyekiti, ninasema ukweli ulivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nishukuru sana Mhe.Waziri ameingia lakini siyo wangu mimi huyo, wangu mimi yupo hapo Mhe. Waziri ninamjadili sasa hivi. Jana nilimwambia Mhe. Makamu wa Rais, haiwi taswira nzuri kuwa leo maafisa hawapo, Makatibu hawapo, wale waliokuja sasa hivi wamekuja kwa kusikia bomba tu linapiga kelele. Kwa kweli jamani hivi tunavyofanya sivyo, hii ni moja katika dharau kubwa. Tukifanya sisi magazeti...

Mhe.Mwenyekiti, mimi siku moja hapa niliumwa na ngiri na sikuweza na ulikuwa wewe, ulikaa pale, mimi sikuweza ku-*submit* ripoti yangu. Ikawa sewe waandishi wa habari mpaka BBC Mshimba na ripoti yake, nikanukuliwa kila ninavyonukuliwa kwa sababu gani umuhimu wa lile jambo na mimi sikukasirika, kwa sababu ndiyo umuhimu.

Lakini binadamu munakuwa maumbo hayakamiliki, wakati wowote inaweza ikatokea jambo usishangae Mhe. Mwenyekiti wangu, na wewe ndiyo uliokuwepo siku hiyo, na wewe ndiyo uliyenitangaza yupo wapi Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na ulikuwa umesema shahidi. Lakini leo ninashangaa huwatangazii wale Wakuu, Wakurugenzi. Kwa mfano jana aibu, leo Mhe. Waziri anarudia tena ripoti, aibu kubwa sana ninakwambia.

Waziri wangu jana alieleza vizuri na mimi nimekuwa nime-*question* vizuri, nimejiandaa vizuri na nikauliza masuala ya mambo ya skuli tuliyojenga kwa majimbo utaratibu ule wanao wa kuturejeshea ili tumalize. Haya mimi nilichangia, kama wengine wanakwambia sijachangia, waambie wafahamu vizuri nilivyochangia, sisemi Kihindi mimi wala Kiingereza, ninasema Kiswahili hapa mimi. *(Makofi)*

Kwa hivyo nieleweke ninachozungumza nini. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, jana mimi nilichangia suala hilo na nilichangia masuala ya Bodi ya Mkopo, vile vile Waheshimiwa basi na sisi angalau tupewe nafasi za kuwasaidia watoto kwenye majimbo. Hayo ndiyo niliyochangia jana. Naomba nifanye kama hiyo *hansard* haingia kwa ripoti ile. Sasa leo ninarudia tena hapa hapa upya, kwa sababu ripoti upya ninaeleza hali halisi ilikuwepo.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hatupo seriou Mawaziri tuseme ukweli ulivyo na watendaji wetu. Ni suala ambalo la aibu sana. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wewe ndiye mwenye rungu katika Baraza hili, kwa sababu leo kitendo kile ingekuwa Mhe. Waziri wangu wa Elimu kama maafisa wangekuwepo jana, wangewahi kumshushia ki-*memo* mara moja.

Lakini hawakuwepo wakamuachia Mheshimiwa wangu akajilabu pale, akajieleza na hiyo ripoti yenyewe ukiisoma ni sawa sawa na ile ile ya jana, ukiitizama wasikae maeneo mengine. Sasa hivi tunavyokwenda sivyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, bado tutakurushia wewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili suala bado kabisa mheshimiwa kuwa *serious* na watendaji. Toa onyo kali mheshimiwa. Siku utakayolifunga Baraza hili toa ukali kweli kweli kama unavyotukemea sisi tukikimbia Barazani. Na wao uwatolee ukali kwa sababu ni jambo ambalo wananchi sasa hivi wanaangalia, Rais mwenyewe anaangalia, hatumtendei haki Rais jamani. Ametuteuwa sisi, amekuteuweni nyinyi Mawaziri; sisi ndiyo maana tukasema mutupe sisi kwa sababu musifikirie labda tunapenda huo Uwaziri, mimi siupendi lakini kutokana na hali ya hilo jambo, sumu tunataka tuitengeneze, mimi siupendi bwana Uwaziri kabisa. *(Makofi)*

Jambo linawezekana Waziri anashindwa kulitengeneza. Ndiyo pale tukasema tupeni sisi *back benchers*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme ukweli wa hali halisi ulivyo. *(Makofi)*

Hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimalizie. Kumalizia Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tunapokuwa tunakaa katika viriri au katika ku-*submit* ripoti hapa kuwaelimisha wananchi, suala la kodi ya mapato ambayo tunayoitoa wanavyochangia wenyewe wananchi. Kwa kweli wanataka kuona jinsi gani utekelezaji wake. Kuna maeneo ambayo inatakiwa ifike na ni muhimu. Kwa mfano unaambiwa katika ukurasa huu unaosema kuna posho lile la Makamisaa ambao wanaotembelea katika maskuli, mheshimiwa anasema atatekeleza, lini hajajua kwa sababu hajui bajeti yenyewe ataipata au vipi. Sasa hili tulione kutokana na hali hii, hili neno la ufinyu ufinyu mheshimiwa naomba liondoke.

Kwa leo mimi kama nilivyosema sitokuwa na mchango mkubwa, nilikuwa nataka na mimi niweke *hansard* kwa hii ripoti mpya. Kwa hayo machache mheshimiwa naunga mkono mia kwa mia ripoti hii. Ahsante sana.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa hii. Awali ya yote nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetujaalia uhai, lakini pia akatupa na uzima akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba nakushukuru tena kwa kunitaja jina ili na mimi niweze kutoa mchango wangu mfupi. Lakini pia niwapongeze mawaziri kwa kuweza kutusomea hotuba zao za mapendekezo ya kamati na maagizo, lakini hatimaye Mwenyekiti wa Kamati hiyo na yeye pia kuja kueleza taarifa yake.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba taifa lolote duniani ambalo limefikia maendeleo ya kweli basi mwanzo wake linaekeza katika elimu, afya na ustawi wa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, mada iliyombele yetu hapa mezani leo inagusa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya lakini pia na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ambao ndio taifa lenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia walianza na masikitiko makubwa ya namna ya utekelezaji wa kazi hizo kwa wizara husika kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wa Baraza hili ni mashahidi wakati nikichangia bajeti ya serikali mwaka huu, niliiomba wizara na serikali kuweza kuandaa mipango ile ambayo serikali inaendana na mapato ambayo tunakusanya, ili kusudi kukwepa kuona kwamba kuna mambo yanashindwa kutekelezeka zaidi ya miaka mitano yanakuwemo katika bajeti za serikali, lakini yanashindwa kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, niliyasema haya nikiwa najua kwamba serikali pale tunapoyasema haya itazingatia na itafikiria na kuona, kwamba michango yetu tumefikiria sana zaidi kwa wananchi waliotutuma katika chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa jana sikupata fursa ya kuchangia kamati iliyopita. Lakini kamati hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Afya na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto napata fursa na kupekua humu kuona mambo ambayo yanafanana.

Mhe. Mwenyekiti, tusisahau kwamba Marehemu Mzee Abeid Aman Karume baada ya Mapinduzi ya 1964, mambo ambayo aliona kwamba ndio itakayokuwa kwamba dira ya kulifikisha taifa la Wazanzibar katika maendeleo ya kweli basi yeye alitangaza, hakusita. Alisema elimu iwe bure, matibabu bure lakini pia njia zote kuu za uchumi zimilikiwe na wananchi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mtazamo huo nilikuwa natarajia kwamba serikali katika mipango yake yote basi itawekeza katika elimu, afya na hatimaye kurudi kwenye ustawi wa jamii. Baada ya utangulizi wangu huu nianze kuingia katika hiyo ripoti yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi bado kidogo tu niweze kuacha kuchangia kwenye Wizara ya Afya kwa kuhofia kwamba inawezekana ikawa ninasema, lakini yasitekelezeke kwa kuwa mawaziri walioko mbele kila mmoja alijibu dhamana yake, na nisingedhani kwamba katika taasisi hiyo nyengine ingepata majibu ya kutosha na kuridhika.

La pili kabla sijachangia, niseme kwamba serikali inapokuwepo hapo mbele tulitarajia na watendaji ambao wana sekta zao wawepo hapo nyuma kusikiliza yale ambayo yangeweza kuwasaidia na wao karibu ndio watekelezaji wa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Wizara ya Afya kwa kuwa waziri kafika. Naanza na Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inatoa huduma za wagonjwa wa sukari katika wodi hiyo. Kwa masikitiko makubwa wodi au hospitali ya Mnazi Mmoja katika wodi hii imekabiliwa na tatizo ambalo ni la kutisha, linahitaji kuhamiwa. Eneo hili kila kitanda kimoja kina shuka moja, likifuliwa au ikitokea bahati mbaya mgonjwa basi atalala hivyo hivyo ama jamaa yake aje na shuka kutoka kwake. Hii ni hospitali ya rufaa, tumeondoa msongamano huu kutaka kuibadilisha na kuifikisha kuwa hospitali yenye kujitegemea na kwamba haitafikiwa na mtu yeyote, isipokuwa wale ambao wametoka kwenye hizo hospitali zao nyengine za wilaya na kufikishwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hali ya dharura ichukuliwe ionekane mbali na wenzangu waliozungumzia usafi na mengine, lakini hili la kitengo hiki cha wagonjwa wa sukari lichukuliwe kipaumbele, kwamba shuka likitolewa liwekwe jengine na hayo pia si hapo tu, ukienda kuangalia vyema utakuta kila wodi, kila mgonjwa ana shuka la aina yake. Hospitali ya Rufaa au hospitali ambayo imejiwekea mambo maalum kwa ajili ya raia wake ni aibu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme kwa hospitali hii ya Mnazi Mmoja ni vyema basi tukaandaa utaratibu wa kuona vipimo vyote vinapatikana pale, haipendezi na pia ni usumbufu wa kwa wale wanyonge waliotoka vijijini na kupewa uhamisho wa kuja Mnazi Mmoja, lakini hatimaye akaambiwa ondoka na mgonjwa wako na uendenaye katika hospitali nyengine kupata kipimo fulani. Hili jambo sio zuri, haliko vyema, haliko sawa kwa serikali. Ni vyema serikali ikaamua kuona kwamba vile vifaa vyote vinavyokubalika vipimo vyote vinapatikana katika eneo hili la rufaa ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba imekuwa ni kitendawili cha *DNA machine*. *DNA machine* imekuwa ni hadithi, imekuwa ni gumzo, ukipata moja moja haikupatikana idadi ya tatu hakuna. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba nitake kujua tumeambiwa kwamba katika ripoti huku kwamba kuna magulio yatajengwa katika sehemu 45 ambapo maradhi ya kichocho yametapakaa. Labda tujuwe ni sehemu gani hizo na pia tujuwe kwamba je, mmeshaanza au imekuwa ndio kupewa taarifa tu tungependa kuelewa hilo, kwa kuwa nimeliona hapa kwa hivyo niseme hivyo.

Jengine ni kuimarisha hospitali yetu ya wagonjwa wa akili ni suala la msingi. Tunauua dunia na hali halisi ilivyobadilika sasa, kwamba madawa ya kulevya yamesababisha matatizo makubwa ambapo pale sasa kuna mrundikano mkubwa wa vijana wetu ambao wanapata matatizo ya akili kwa kupitia madawa ya kulevya. Ni vyema basi napo pakaweza kuangaliwa. Kamati ilisema hili kwamba ionekane iweze kutengenezwa kama idara, lakini serikali majibu yake ilisema kwamba inaboresha ikiwa ni miongoni mwa idara yake, kwa hivyo italifanya hilo. Mimi nadhani sambamba na hilo ni vyema ikalishughulikia vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Hospitali ya Mwembeladu, hospitali ambayo inatoa huduma kwa mama wajawazito. Pia hospitali hii inatoa huduma za wagonjwa wa maradhi ya *VVU*. Haikuwa vyema wagonjwa wale kuwaweka hadharani kila mmoja anayekwenda anapita na kuwaona, lile halikuwa jambo zuri. Ningependa uongozi ufanye utaratibu wa hospitali ile ili kuona wale watu wanawekwa katika sehemu ya stara ili na wao kuwajenga hamasa na kuwanao pamoja. Huku tunakataza unyanyapaa, lakini pale umewaweka hadharani kila mmoja anasoma na anajua hasa kitengo hiki kunafanywa hivi, akiingia ndani huwezi kujua, lakini nje hadharani, wale wanafanya huduma hizi na wale zile wanawapita tu. Mimi nadhani lile sio jambo zuri, ningependa uongozi wa Hospitali ile ya Mwembeladu ifanye utaratibu ili kuwapa huduma katika sehemu ambayo itakuwa na stara.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, kawaida "ukimkera mchinja mbuzi utaukosa mchuzi". Nalisema hili nikiwa na maana ya kusema kwamba kuna walimu 159, ambao inasemekana kwamba hawa wako Pemba mishahara yao hawajalipwa eti ilipotea potea katika taratibu zisizojulikana.

Mwaka 2013 hadi 2014 hadi leo tukao mwaka 2015. Wakati huu tunasema kwamba ziko Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha naye hajatoa. Kwa hivyo, mimi nasema walimu hawa walipwe haki zao hizi. Hizi ni haki zao na kuwanyima ni kufanya kosa, kwa hivyo ninashauri serikali ichukuwe hatua za dharura kuwalipa haki zao hizi.

Mhe. Mwenyekiti, sio hawa tu kuna ile ya nyongeza za mishahara kwa walimu, ambao walikuwa wao katika kufanyiwa utaratibu wao waliambiwa ni walimu wenye uzoefu wa muda mrefu, lakini hawakuwa na taaluma iliyowafanya waongezwe mishahara. Hadi hapa niliposimama hapa walimu hawa hawajalipwa pesa zao kwa hapa Unguja pia. Mhe. Waziri, wizara na serikali naomba sana kabisa kwamba hili ulichukulie kipaumbele na walipwe haki zao hizi. Hawa ndio wenye kuandaa, hawa wanafunzi tunaowataja tukawatengenezea *boarding school* na tukawajengea. Hivi tukiwakosa hawa walimu wakitoka kwenda sehemu nyengine, hawa wanafunzi wetu watakwendaje.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika elimu ya msingi na maandalizi nachanganya. Kuna mabadiliko ya mitaala, lakini nitake kujua hivi katika mtaala huu ambao mmeuanzisha ambapo utaratibu huu tayari umeshaanza kutekelezwa na nyinyi mnadai hamna vitabu na walimu nao wana manung'uniko, wanasema hawana miongozo katika hili, hawana vitabu vya kufundishia na wanafunzi hawana vitabu. Hivi jamani mmeingia kwa utaratibu upi, tuweze kujua mmeanzaje. Lakini pia mtaala huu ambao mnasema kwamba mmeanzisha *nursery school* katika skuli za serikali, skuli hizi mmewaambia lazima waanzishe katika kipindi hiki, wameanzisha kweli.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie wizara mimi binafsi hili sikuhadithiwa nimekwenda kuliona na kusimuliwa katika skuli za serikali, wameanzisha madarasa haya lakini walimu wa madarasa haya nyinyi mmesema hamna fedha za kuwalipa hawa walimu. Walimu wenyewe mmewalazimisha hilo na wameanzisha, lakini wao walimu wanachanga fedha zao wenyewe za mishahara kuwalipa walimu hao wengine walioanzisha *nursery school* madarasa hayo ya maandalizi.

Jamani hili jambo haliwezekani, nasema kwa utaratibu huu muwaajiri walimu wa *nursery* na ninaamini kwamba wapo vijana waliosomea wenye uwezo huo, kwa hivyo waajirini hao vijana, ili mifumo yenu hii mlioanzisha mitaala yenu muweze kufanikiwa.

Jengine katika mtaala huu mumeanzisha masomo 10 kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza, hivi jamani tutafika huko, wana uwezo huu, tumeuangalia vizuri huu utaratibu, masomo 10. Sisi ambao tumeanzia huko tunaona kwamba masomo 10 kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza sio jambo rahisi. Iko haja ya kuangalia utaratibu na mfumo mzuri ambao utawezesha kuboresha elimu na sio kwa kupiga brashi brashi na blaa blaa hizi hatuwezi kufika.

Mhe. Mwenyekiti, darasa la saba inaishia mwaka huu na hatimaye darasa la sita kuanzia kipindi cha mwaka utakaofuata watakuwa wanafanya mtihani ambao ni wanafunzi wadogo lakini masomo yake pia yataanza kwa Kiingereza kuanzia darasa la tano. Hivi huko chini hana msingi anakuja kupata Kingereza darasa la tano inakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara iuangalie kwa kina mfumo huu. Lakini niwaulize tena swali jengine dogo wanipatie jibu. Hawa wadau walimu wenyewe ambao wanakaa na wanafunzi, hivi mlipata *impute* zao hawa katika kuanzisha mtaala huu, hawa ndio wenye kutekeleza hili, mlipata vitu kutoka kwao jamani wakakusaidieni mambo, ndio wanaoishi na hao vijana, wenye uelewa na kupima viwango vya hao wanafunzi, mlipata chochote, mlikaa nao.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye bodi ya mikopo. Mhe. Mwenyekiti, ucheleweshwaji wa uingizwaji wa fedha za bodi ya mikopo na wanafunzi kushindwa kupata fedha hizi kuna mambo yanaweza yakazorotesha, hususan kama mimi mwanamke nasema kwa wanawake wenzangu. Kusababisha wakati mwengine kujiingiza kwenye mambo mabaya.

Mhe. Ismail Jussa alisema hapa kwamba pengine uweko nje ya nchi fedha zile haziingi, hana chakula, hana huduma wala pesa ya kulipia afanyeje. Yaani tayari unampoteza mwanamke mwenye uwezo wa kuendeleza taaluma na kuweza kusomea fani fulani, lakini anakatishwa njiani na mazingira kama haya, serikali ambapo haikuyawekea utaratibu maalum unaokubalika.

Kwa hivyo, nadhani serikali kwa wale ambao imewakopesha wengine si wako nje, hawa waliopewa basi mkopo na kukubaliwa waingiziwe hizo fedha kwa wakati, mara nyengine tunawasababishia matatizo ya kukatisha hizo taaluma zao, wengine wanapata ujauzito huko, wengine wanakubwa na mabalaa ya majanga ya mambo hayo ya ukimwi na vitu vyengine.

Mamabo ambayo yangewekewa utaratibu mzuri, yasingeweza kutokea kwa mtoto wa kike. Hili nalisema hususan kwa mtoto wa kile, lakini pia nagusa kwamba na wengine waliokubalika kupewa mikopo basi wapewe kwa wakati unaostahiki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nirudi tena nione kwenye majibu hapa

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe una dakika tano za ziada.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Niseme kwamba kuna majibu hapa. Anasema kwamba kamati ilishauri wizara kuwapatia walimu wanaofundisha skuli hizo za kijamii huko posho la shilingi 20,000. Mimi nasema, huko mwenyewe kajibu, yaani serikali imejibu hili halijafanyika kwani utaratibu hauruhusiwi. Huo ulioko serikalini hawajapewa watawapa hawa, hivyo haupo kweli.

Jengine ni hili la kamati kufikwa na tatizo upungufu wa walimu. Tunajibiwa kwamba hao walimu upungufu wake, inasema kwamba ni walimu wa sayansi. Tatizo likiwa mwalimu bado limebaki kuwa mwalimu, akiwa ni wa sayansi, akiwa huyo mwalimu ni wa *art*, lakini bado tatizo linawakabili walimu mufanye juhudi ili waweze kupatikana walimu hao. Hatutarajii kupata majibu kwamba, kwa sababu waliopo walimu ni wengi, lakini fani hiyo sio yao.

Tatizo ambalo kamati imeliona ni upungufu wa walimu, msingi tunatarajia taasisi hii ituambie kwamba limetatuliwa tatizo hili kwa kupelekwa walimu wanne, ili waweze kumaliza hilo tatizo na ndio msingi ambao tunautarajia sana tupate hilo, hatutarajii kuambiwa kama walimu wa sayansi au walimu wa Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa hapa kwamba skuli zote hazina hati miliki na uvamizi wa ardhi tunajua kwamba sasa imekuwa ni tatizo kubwa na gumu. Kamati imelibaini hilo na imesema hivyo. Lakini majibu ya kijumla jumla, kwa sababu serikali inatabia ya kujibu jumla jumla bila ya kutupa hata takwimu zenyewe na jambo lililofanyika kwa uhalisia wake. Humu tumekuta hivyo vitu vya kijumla jumla. Majibu haya hayaoneshi ufanisi mwenye kufanya, atajibu tumefanya jambo moja, mbili, tatu.

Sasa nataka kujua basi je, kuna skuli ambalo tayari limeshapata hiyo hati miliki katika huu utaratibu ambao mnasema mmeshapeleka Wizara ya Ardhi, zipo hizo skuli zilizopatiwa na hali ya uvamizi inaendelea huko.

Nipewe pia taarifa ya kamati ya Idara ya Elimu ya Sekondari katika hili agizo namba mbili ambapo kamati imeagiza Wizara kupitia skuli yake ya ufundi ya Kengeja kwamba wapate hivyo vifaa vya kazi, lakini tunaambiwa vifaa vyote vimepelekwa kwa wanafunzi vya kufanyia ni vipi, mbona havina orodha au ni majibu ya mkato ili tuweze kufahamu hilo tu, majibu haya hayakidhi haja jamani ndio ukweli, kama kweli jambo wamelitekeleza tungelipewa takwimu, idadi na vipi

lilivyotekelezeka. Tukipewa majibu ya jumla jumla, sisi ndio wasimamizi wa fedha za walipa kodi jamani. Hapa hatujengi imani Wizara ya Fedha inasema haikuingiza ndio jibu limekwisha, aliyeambiwa katekeleze anasema tumelipeleka fedha, aliyesema tumelitekeleza anasema tumelitekeleza kwa asilimia mia moja lakini unaambiwa limetekelezwa tu limetekelezwa kwa ufanisi upi?

Hata kwenye idara ya ukaguzi tumeambiwa kwamba kumenunuliwa vespa ishirini hilo limetajwa ishirini tu, lakini je, hao walimu waliokwenda kufundishwa kwa ajili ya kuweza kuhimili na kuweza kukagua hiyo taaluma, ni fani gani hizo walizosomea, hamna humu tumeelezwa jumla jumla.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Wizara ya Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Wanawake na Watoto nayo niseme kidogo niipe haki yake kwenye habari ya mikopo na kuhusu lile shamba la *green house,* Mhe. Mwenyekiti, mimi naona kama tunacheza hatujataka hasa vijana kuwatafutia ajira, huu ni mchezo maana ukenda ukiwaona hao vijana na ukaona shughuli na ukaona maelezo ambayo yanasema humu na fedha na taratibu sijui na mikopo. Lakini hizo hali huzioni vijana bado wako vijiweni, bado malalamiko yapo mengi, hivi ni vijana gani hao wanaopewa mafunzo na kuweza kuwa na hizo ajira kwamba wanajiajiri.

Si kweli kwamba vijana ambao wanakataa kilimo si kweli mimi nasema, kama wanawezeshwa na kupewa fedha na kupewa taaluma vijana wanazikubali kazi. Vijana wa Kizanzibari sio wavivu kiasi hicho wanao uwezo huo maana asili yetu sisi tangu zamani ni kulima, wakwezi na wakulima ndio wananchi wa nchi hii. Sasa kama watawezeshwa wanao uwezo huo kama haliwezi hili basi twendeni uvuvi wa bahari kuu, si tunayo fanyeni basi miundombinu mingine twende huko mbadala hiyo. Ama twende kwenye uchimbaji wa mafuta na gesi si tunaona kwamba hii hawakubali kuelewa tuwaeleweshe huko.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Subuhana wataala aliyetujaalia sisi kufika hapa na kuwa wazima na afya inaturuhusu kusimama mbele ya baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa vile vile niipongeze kamati kwa kufanya kazi nzuri. Vile vile na Mawaziri wetu watatu kuwasilisha ripoti hizi za kamati vizuri tu. Mimi kama Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, sina mchango mkubwa bali mambo mengi tumeyaona ila tunatia nyalio tu hapa tuliyofikia, tumeyaona mengi *live* kabisa. Lakini niseme si vizuri kama na sisi hatujasimama kutoa mchango wetu japo mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nitakwenda katika Wizara ya Afya na katika Wizara ya Afya niseme tu sehemu inayoitwa afya ni sehemu ya unadhifu, ustaarabu uliokithiri, kwa sababu ninapozungumza neno afya kama mahali sio safi basi afya haipo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa Makamo wa Kamati kama nilivyoeleza nimetembelea jengo la Mnazi Mmoja, tumetembelea katika sehemu ya wagonjwa wa sukari, tumetembelea katika wagonjwa wa mifupa.

Mhe. Mwenyekiti, ile sehemu ni mbaya sana ni mbaya na nathubutu kusema mbele ya Baraza lako tukufu uchafu umekithiri hili hatulifumbii macho hata kidogo na tutalieleza na inshaallah kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu wanaohusika watalifanyia kazi. Tumekwenda pale kuona katika sehemu ya mifupa kuna vitanda vichakavu vichafu kabisa, na vitanda vile vimepangwa kwa mawe leo mgonjwa unakwenda kumlaza kitanda kimepangiwa mawe unategemea nini mtu aliyekuwa hajiwezi akianguka tutasema nini.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kama haitoshi lakini katika sehemu hizo hizo mbili nilizozitaja basi Haki ya Mungu wagonjwa wanasikitika sana kutokana na harufu mbaya iliyopo pale, ukiwauliza wagonjwa wanakula pale wanakwambia hapa hatuna *dettol* ya kusafishia, hatuna *gloves*, uchafu umekithiri kabisa, na hili pamoja na kuwa ni kamati yangu lakini silifumbii macho kwa sababu ndio shughuli yetu katika kazi lazima tuwaeleze.

Mheshimiwa Wizara hii yepi waliyotupatia sisi kama Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, tulipata safari ya kwenda Dar es Salaam tulitembelea pale *Ocean Road,* jambo tulilojifunza katika *Ocean Road* pale nakumbuka pale kuna wagonjwa wa kensa, vidonda vyao ni vibaya sana lakini *wallahi* tuliuona unadhifu wa kutosha, hospitali ilikuwa ni safi tukenda tukaulizana pale tukawapa pongezi sana, kwamba jambo tulililoliona hapa ni usafi. Basi na sisi katika jambo la kuiga tuige usafi katika vituo vyetu vya afya na hospitali zetu.

Leo mtu unakwenda kumuweka katika hospitali basi unamzidishia maradhi Haki ya Mungu, juzi pale hopitali ya Mnazi Mmoja tarehe nimeisahau walikuwepo waandishi wa habari kutembelea waliwaona pale hata chakula kinashindwa kulipa kwanye sehemu ya wagonjwa hili ni tatizo. Japo kuwe dawa hamna hospitalini lakini usafi uwepo hilo ni jambo moja, unaridhika ukenda katika mahospitali ya wenzetu. Lakini tunakwenda pale inakuwa ni hatari kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha katika vituo vya afya au katika hospitali zetu hizi nakwenda katika sehemu za uwezeshaji, Mheshimiwa kwa kweli uzalilishaji wa jinsia kwa watoto wetu ni *inverses* na mtu anapofanya kosa lile ushahidi haupatikani kisingizio hatuna kipimo cha *DNA* hili ni tatizo, lakini katika fursa hii tuliyoipata kwenda kutembelea pale kutembea katika kitengo cha *DNA* na tukauliza masuala.

Jamani hiki kipimo cha *DNA* kinachukua muda gani katika kupima, tuliambiwa kwa kuchelewa ni muda wa wiki mbili kwa kuchelewa muda wa wiki mbili lakini vipimo vinavyotolewa hapa vikenda kule basi unatimiza mwaka au miaka miwili halafu halijapatikana jibu. Je, tunawatendea haki watoto wetu waliodhalilishwa kwa kutoa ushahidi hatutendi haki kabisa kabisa na hili tulielewe tunavuruga ushahidi moja kwa moja kwa hawa wahusika wajue kwamba hatuwatendei haki wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumetembelea hospitali ya wagonjwa wa akili pale Kidongo Chekundu hawa ni wagonjwa wa akili lakini ni ubinaadamu kama binaadamu mwengine, nao wanahitaji kuishi vizuri kama tunavyoishi sisi lakini pale Kidongo Chekundu ukenda utafikiria hospitali ya wagonjwa wa adhabu kabisa sehemu zinanuka uchafu. Ni pabaya na wale wanaoweza kusema wanasema wanavyo vitanda vizuri lakini magodoro hawana lakini huo uchafu umekithiri. Wewe tu kwenda kuangalia kwa moja basi afya yako inaathirika je, hawa tunategemea kuwatibu au

kuwaumiza zaidi lazima Serikali ijipange, kufanya jambo kwa nia safi hawa ni wananchi wetu wamepata athari tu na binaadamu mwengine yeyote anaweza kupata athari kama hiyo. Yeye si kwamba matatizo aliyoyapata anayataka hayataki hata siku moja, lakini kwa sababu Mwenyezi Mungu ameshamjaalia awe hivyo haiwezi kuepukika.

Kwa hivyo tuwafikirie wagonjwa wa akili waliopo Kidongo Chekundu ni hatari kweli kweli, lakini watu wanasema mnyonge mnyongeni lakini na haki yake mpeni jambo moja kwa wagonjwa wa akili nashukuru ni mlo, sasa hivi *alhamdulillahi* mlo wanapata mara tatu pale. Hili tunawapongeza hata wale waliotoka pale washaenda majumbani kwao basi ukifika muda wa kula wanarudi pale Kidongo Chekundi.

Mheshimiwa nikitoka hapo nakwenda katika Wizara ya Elimu, Wizara ya Elimu kamati yetu ilitembelea kisiwani Kojani tarehe 12/12/2014 na kama ilivyoeleza pamoja na mabadiliko yaliyotiwa muhumu lakini nilielezwa kukiwa na upungufu hakuna kabisa sio upungufu walimu wa sayansi, kamati ikaiambia Wizara ilichukulie hatua suala hili na wakasema watachukua hatua za dharura. Kama mliona kabrasha nililopewa jana hapa nimeambiwa tayari mwalimu mmoja ameshaajiriwa na mwengine anafuata, jamani si kweli hii mnatudanganya vibaya, tunatoka majumbani huku tunajua kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, mwalimu aliyeajiriwa ameajiriwa anasomesha kiingereza na kiarabu si mwalimu wa fani hiyo, lakini sisi tumeelekeza yupo kijana wetu aliyesoma pale Diploma ya sayansi, yupo ndio niliyetegemea kwamba ameajiriwa, lakini wamemuajiri mtu mwenye kufundisha Kiingereza na Kiarabu na niliwatajia jina lake kama watalipinga wapo wenyewe hapa anaitwa Khadija Mohammed Omar ndio waliyemuajiri.

Sisi tuliyekusudia aajiriwe kwa mambo ya sayansi hajaajiriwa kwa hivyo mumekwenda kinyume na taratibu na agizo la kamati tunaomba mujirekebishe tena mara moja, maana tulivyosema na nyinyi mlikubali kwamba ni dharura, wale wanafunzi wana fursa nzuri ya kusoma soma sayansi na huyu tuliyenae twende nae.

Kwa hivyo tunawakumbusha tu kama mulivyokwenda nje kidogo na tulivyokusudia, lakini kama kwamba haitoshi katika sehemu hiyo hiyo kama nilivyosema Mwenyekiti wetu ni mahiri, Mhe. Mgeni mpaka kufika Kojani kafanya kazi kubwa sana wengine wanaogopa mambo ya visiwa, nyote mtakuwa mashahidi Mhe. Haji Omar Kheri alikuwa katika mambo ya utumishi wa umma alifika pale na tukamuomba akasema paletwe upendeleo katika mambo ya visiwa.

Visiwa vina dhiki kubwa sana jamani nyie wenzetu mnaokaa ng'ambo ya pili mnajua lakini wale wanaokwenda wakipata ziara kutembelea wajue lazima upendeleo utolewe. Kwa hivyo, ile dhamira aliyokuwa nayo yule nzuri ifanyiwe kazi, walimu tuwe nao wa kutosha na walimu wa sayansi tupewe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie nyuma kidogo ingawa imeshapita si vizuri lakini nikumbushe kitu katika kituo cha afya Kojani, pale pana malimbikizo ya umeme na nyumba haiko katika hali nzuri ya madaktari. Ipo katika hali mbaya sana nyumba inavuja, madaktari hawapo makini na wote sio watu wa pale kisiwani ni watu wa upande wa pili, kwa hivyo wakati wowote wanaweza kutuacha kutokana na hali jinsi ilivyo kutoka jengo lile la nyumba ile ya madaktari. Kwa hivyo

Mheshimiwa ningeomba hapa tufanyiwe fungu la huruma angalau ufanyiwe ukarabati na yale malimbikizo ya deni la umeme yalipwe.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi sina mchango mkubwa lakini nimalizie kwa hao walimu ambao wanadai haki yao walimu 159 kwa nini mtu haki yake mumnyime, haipendekezi kabisa mtu kumnyima haki yake na huyu ni mwalimu mmemuajiri mumpe zile nguvu afanyie kazi, leo wakati nguvu ile unamnyima atakuwa na akili ya kumsomesha mtoto akafahamu haiwezekani hivyo kwa sababu anakuwa na fikra za kujipatia riziki kwa upande mwengine, lakini haki yake ya kimsingi tangu mwaka 2013 mpaka leo hajapata.

Kwa hivyo kama ni Wizara ya elimu pamoja na Wizara ya Fedha washirikiane kulitatua tatizo hili, limeshakuwa la muda mrefu si kuliacha hata dakika  na wale kila siku wanatwambia wanatukumbusha na chombo chao cha kuwasemea leo tunasema kama mlikuwa hamsikii, leo tumeshapeleka *message* kwa hivyo ifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia wizara hizi, kwanza sina budi kuweza kuchangia Wizara ya afya ambayo ndio yenye masuala mengi sana na hata hivyo ndivyo ilivyo hasa kwa hivi leo. Wizara ya afya ndio inaongoza katika matatizo yetu hasa kwa vile masuala yake mengi yanatugusa sisi binaadamu.

Zaidi ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu zaidi kwa kuwepo hapa ili kuhakikisha kwamba kuweza kuisaidia Wizara hii kuipa nafasi ya kuweza kujikosoa yale yote ambayo tumekusudia kuiambia Wizara hii. Zaidi nampongeza Mhe. Waziri, pamoja na kamati yake ya utendaji ya shughuli zake kuweza kuhudumia wagonjwa kwa dhati, isipokuwa matatizo madogo madogo yapo katika wizara hii ambayo yanahitaji kushughulikiwa vizuri kama tulivyoanza kuyataja pamoja na wenzangu.

Hivi sasa katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, kuna matatizo makubwa ya madawa hivyo iko haja Wizara kuhakikisha kwamba madawa yanapewa umuhimu zaidi kuhakikisha kwamba yanahitajika katika sehemu zote za huduma za biaadamu katika hospitali hiyo.

Nikiondoka Mnazi Mmoja tunaweza kusema kwamba katika hospitali zetu za Wilaya hasa katika majimbo yetu ni hospitali nyingi sana ambazo hazina upataji wa madawa, ukiangalia tunazo hospitali lakini ni magofu tu ukienda hupati hata *panadol* kuweza kuhakikisha kwamba wagonjwa wanaokwenda pale wanahudumiwa.

Mimi niko katika jimbo la Koani kwa hakika hospitali yetu ya Uzi Ng'ambwa hata sijui kama yeye Waziri amefika ukienda huko badala ya kupimwa watoto hupati jambo jengine, isipokuwa ukifika matatizo muwakilishi au mbunge tatizo kubwa unaombwa kwamba hospitali yetu ina tatizo la madawa.

Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba hospitali za wilaya zote apite ili ahakikishe kujua hospitali zetu zina matatizo ya aina gani. Ukienda hospitali ya mjini ambayo ni

ya rufaa haina madawa basi ipo haja kwamba uhakikishe hospitali za Wilaya ndio zimeoza kabisa, ukienda za Majimbo ndio hazifai.

Kwa hivyo tunazo hospitali nyingi katika majimbo yetu lakini mahitaji hayapatikani, ukienda hospitali ya Machui tuna hospitali pale ya Serikali lakini imefungwa muda wote ukienda utakuta huduma hamna. Watu ukisikia wanakwenda Machui wanakwenda katika hospitali za *mission* ambazo kule wanalipia, ndio wanapata huduma zao.

Kwa hivyo hospitali yetu ile ya Serikali muda wote haina matibabu  na ukiangalia daktari hawana daktari anakwenda na kutoka hana hata nyumba ya kuweza kukaa pale kuweza kuhudumia wananchi wetu, kwa kweli hospitali zipo lakini magofu, hazina vifafaa vya kuweza kuhudumia wagonjwa. Ukenda Uzing'ambwa ni ambapo mahala unatoka katika kisiwa unavuka, anaweza akatokea mgonjwa mahututi kwa mara moja lakini hospitali ya Uzing'ambwa ninavyojuwa kwamba haina daktari. Daktari anakwenda kutembea tu kwa gari hilo hilo likipinda ndio anapinda nalo kurudi tena mjini.

Mhe. Waziri nakuhakikishia kwamba hospitali zako za majimbo zipo lakini hazina huduma. Ipo haja uwe unazitembelea au Makatibu wako angalau kujua madaktari pale ni wangapi ama yupo au hayupo. Lakini nakuthibitishia kwamba Uzing'ambwa ni kisiwa ambacho maji yanajaa na kupita kwa shida lakini na daktari pia hamna.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hizi ndizo lawama kubwa za hospitali zetu, kila anayesimama hapa anatoa hoja za hospitali kwamba kuna matatizo. Lakini tukirudia rudia kwa kweli itakuwa haina faida. Nimemtajia hapa Mhe. Waziri moja kwa moja anihakikishie ni lini atakuwepo daktari wa kudumu katika kisiwa cha Uzing'ambwa, tukiachilia Machui ambapo hospitali tunayo lakini haina daktari haina nyumba ya daktari. Hayo kwa kweli ni matatizo ambayo tunayo katika majimbo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikichangia zaidi nije kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii. Kwa kweli tuna matatizo sana katika Wizara hii hasa kutokana na udhalilisha wa watoto umekuwa ni mkubwa sana katika nchi yetu, na hivi sasa bado unaendelea na bado hatujaupatia uvumbuzi. Kila siku tunasema kwamba jambo hilo tunahakikisha tutalishughulikia lakini matatizo bado yanazidi nchini na uhalifu bado unaendelea hasa kutokana na kukosa kile chombo muhimu cha DNA.

Hicho ni chombo muhimu sana, naomba Mhe. Waziri atakapotoa majumuisho yake atutajie lini chombo hiki kitapatikana nchini, ili kuhakikisha kwamba kupatiwa uvumbuzi wa watoto wetu kuhakikisha kwamba wapo katika hali salama, ili wapate haki zao za kuweza kuhakikisha kwamba wahalifu wanaokamatwa wanapatiwa maamuzi ya serikali na kuhakikisha kwamba wanapata adhatbu inayostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, wahalifu hawa kama hakuna chombo hiki siku zote wao watakuwa ndio washindi. Kwani wakitoa rushwa pale pale kesi inaisha lakini jambo ukitajia unahakikisha kwamba hiki kitu kimefanyika hasa. Lakini mtu anarusha kwamba chombo muhimu ambacho kinahitajika nchini na sio thamani ya pesa nyingi kuliko ambavyo meli ambayo tumeweza kununuwa kwamba kinashindwa kuletwa nchini kwa muda muwafaka. Namuomba Mhe. Waziri

akija kujumuisha atuhakikishie ni lini chombo hiki kinaweza kufanikiwa kuwa nacho na tukaweza kukihudumia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mchango wangu ni mdogo naendelea kuchangia katika Wizara ya Elimu. Mtu yeyote katika dunia hii jambo muhimu ni kuhakikisha kwamba tunapata vijana ambao wamesoma katika nchi yao. Utakuta katika wizara hii majengo ambayo yanajengwa ili vijana waweze kusoma majengo yetu yanakuwa hayana uhakika wala udhibiti. Utashangaa kwamba shule hizi zimejengwa hata mwaka mmoja hazijafika leo zinaanza kufanyiwa *repair* kabla hata wanafunzi hawajasoma.

Mhe. Mwenyekiti, nashangaa sana kwamba ni afadhali skuli zetu ambazo tunajenga sisi majimboni ambazo za kujitegemea ambazo serikali inatutilia mabati tu, utakuta zinadumu na zina uhakika, utamaliza miaka husikii kwamba skuli ile imefanyiwa *repair*. Imejengwa vizuri tena kwa nguvu za wananchi peke yao. Serikali inakuja kwa kutia mabati na rangi. Utashangaa skuli hizi ni kubwa na zimejengwa kwa fedha nyingi sana za serikali, lakini hazijamaliza hata mwaka mmoja hivi sasa zimeanza kuwekewa fedha za kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Wizara ya Elimu ituhakikishie kwamba hawa wakandarasi wanaowapata wanakuwa wanawapa majukumu yao ambayo wayashughulikie ama hawawapi uhakika wa kujenga kiwango gani kinachohitajika kujengwa, ili wapate malipo yao halali ya kuweza kujenga hizi Skuli zenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atuhakikishie kwamba hizi skuli ambazo zinafanyiwa *repair* sasa hivi kwa milioni hizi mia moja, zimekaa muda gani kwamba hivi sasa zianze kufanyiwa *repair* kabla ya nyengine ambazo hata hazijaanza kukaa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mchango wangu mdogo huo leo, nimefikia hapo naomba haya yote niliyoyasema au tuliyoyachangia yachukuliwe hatua ili wananchi wetu wahakikishe kwamba tunawatetea katika masuala yao ambayo ni magumu sana na yanahitajika kutolewa uwamuzi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Muhammed Haji Khalid:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, nami leo nitakuwa na mchango mdogo zaidi kuliko ule wa Mhe. Mussa Ali Hassan.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa kuendelea na majukumu yetu ya kawaida ya kazi. Pia nikushukuru na kukupongeza kwa kutupa nafasi hii ya dakika za mwisho nami angalau kutoa maoni yangu machache juu ya ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa Wizara ya Elimu, na nianze na yale maposho ya walimu 145 ambayo hawajalipwa na fedha zilizokatwa za walimu 159 ambao kadhalika na wao fedha hizi zinaonekana kwamba zimekatwa katika mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha, matukio yote mawili haya yanawahusu walimu waliokuwepo Kisiwa cha Pemba, wale waliokuwa hawajalipwa posho zao na waliokatwa pesa

zao, kwa njia yoyote ile. Hili ni tatizo, kama ni kukosea kwa nini kukosewe kwa upande mmoja tu Kama hakuna pesa kwa nini ikoseke pesa kwa upande mmoja tu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna nyongeza zilizotolewa, Unguja walipata miezi mitatu kabla ndio wakapewa walimu waliokuwepo Pemba. Maana yake chochote kilichofanywa Wizara ya Elimu kuwa huku wanatangulizwa walimu waliokuwepo Unguja wanatangulia kuliko wale waliokuwepo Pemba kwa nini? Wote ni walimu, wate ni wa kwetu, wote ni wafanyakazi wetu. Lakini matatizo agh'alabu mengi yanawakumba wale waliokuwepo kule.

Mimi sikubaliani na serikali kuwa ni kwa makosa na jambo makusudi limefanywa. Kwa nini serikali ifanye hivyo na wote hawa ni watumishi wetu, na wote ni walipa kodi. Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kwa kuwa hili suala sio la jana na juzi, tokea mwaka 2012 bado Serikali inasema ni kosa na kosa hilo haliwezi kurekebishika miaka yote hiyo, watu na haki yao. Mambo mengine ni hatari sana.

Mhe. Mwenyekiti, ningeiyomba Serikali pesa hizi ifanye juu chini kabla ya mwaka huu wa fedha haujamalizika walimu hawa wapewe haki zao. Ingelikuwa hii bajeti *Wallahi* nisingeipitisha Wizara ya Elimu bajeti yake. Lakini bahati mbaya limekuja suala hili bajeti bado na kama siku ya bajeti kama hili halijatekelezwa Wizara ya Elimu bajeti yake mimi sitoipitisha kama hawa hawajalipwa. Nitatumia uzee wangu na uzoefu wangu kuwashawishi wajumbe waikatae bajeti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni ule mchango wa madawati kwa ajili ya maskuli tuliyoagiza kila tiketi ichangie shilingi elfu moja. Kama kweli fedha hizi zinakusanywa kiadilifu na kwa uwaminifu, nadhani tokea tulipopitisha sheria ile au agizo lile skuli nyingi zingelikuwa tayari zimepata madawati hayo. Lakini imani yangu fedha hii inakusanywa, wapi inamalizia sijui. Kwa hivyo ningeomba fedha hizi zitumike kwa ajili ile iliyokusudiwa. Tulikusudia kwa ajili ya madawati, vikalio maskuli wala sio kwa njia nyengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine watu wanasema mtu lake halimtapishi linamuumiza moyo, lakini itafika siku mtu lile lake limtapishe. Kwa hivyo tusifike pahala tukatapishwa na letu, kila mmoja atimize wajibu wake kwa jinsi ambavyo anatakiwa atimize wajibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, niguse kidogo Bodi ya Mikopo. Mikopo ya Elimu ya Juu ni muhimu kwa sababu wanafunzi wengi wanaopewa wengine huwa hawana uwezo wa kujisomesha. Ningeiomba bodi hii itizame zaidi wale ambao hawana uwezo zaidi kuliko wengine ili kupatiwa mikopo hiyo. Na wale ambao waliohakikishiwa kuwa wapate kwa hivyo mikopo hii wapewe kwa wakati, ili iweze kuwasaidia katika shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi kadhaa wanatufata sisi kuwa hawajaingiziwa, kwa hivyo wanataka misaada yetu. Mimi huwa nawauliza wewe huna mkono, anakwambia nnao lakini bado hatujatiliwa. Kwa hivyo wanaohusika wajitahidi kukamilisha ili kuwaondoshea hawa watoto au wanafunzi matatizo mengi yanayowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije katika suala la ukaguzi mashuleni. Bahati mbaya nimeacha shule kwa muda mrefu na pengine *system* ya sasa ya ukaguzi siijui. Lakini kwa kuwa mara kwa mara

hupita maskuli, ukaguzi unaweza ukamaliza mwaka mzima kuna skuli fulani haijakaguliwa. Hii ina maana kitengo hiki kama kipo hakifanyi kazi yake kama inavyotakiwa. Ama pengine kwa ukosefu wa usafiri na mambo mengineyo au kukosekana kwa hao wakaguzi. Lakini kitengo hiki ni muhimu kweli kweli na ni lazima kiwe na walimu ambao wamesomea hiyo fani ya ukaguzi. Kwa sababu bila ya ukaguzi walimu wanakwenda shule vile wanavyotaka wao.

Mhe. Mwenyekiti, mara moja nilifanya ziara katika skuli yangu fulani. Kuna mwalimu nilipouliza matatizo yeye akanambia tatizo ni hawa wakaguzi Mheshimiwa. Nikamuuliza wana nini? Akasema wanapokuja wanatudai *scheme*, wanatudai *records*. Nikaona ohoo! huyu mwalimu kwa sababu kachukuliwa tu kaajiriwa hajui chochote, mkaguzi kufanya kazi yake yeye anaona ndio tatizo. Lakini pia nikamuuliza hawa wakaguzi wanakuja mara ngapi kwa mwaka. Wakasema wanaweka wakakaa hata miaka miwili wakaja kwa mara moja. Kwa hivyo na huu ukaguzi nao ni hafifu kweli kweli. Kwa hivyo kitengo hiki kiimarishwe ili walimu wapate kukaguliwa na waonekane ule utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, mimi nije katika suala moja tu hili la udhalilishaji wa watoto. Hili ni tatizo tena ni sugu, kwa sababu watu wasio na huruma wanaacha watu ambao ni wanene kama mibuyu, wanatuharibia watoto wetu wadogo. Watoto wadogo ambao hata shughuli hizo hata hawajaziweza kuzitekeleza. Huu ni msiba na inafaa kwa nguvu zetu zote tuupige vita uhalifu huu. Pale ambapo mtu atatiwa hatiani kwa tatizo hili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Mhe. Mwenyekiti, hiki kipi au hicho chombo cha DNA tunachokilalamikia hicho ni chombo tu cha kutafuta ushahidi wa damu ya muhusika kama yule aliyetuhumiwa ndiye au laa, huwo ndio umuhimu wake tu. Lakini kama kipo au hakipo tatizo linapotokezea ni kwa muhusika achukuliwe hatua za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, muda umemalizika ningekuomba nimalizie jioni. Asante

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe ambaye uliyekuwa unachangia Inshallah dakika zako tano utamaliza jioni utakapokuja kurejea. Lakini Waheshimiwa Wajumbe huku nina majina manne ya ziada. Tujitahidi basi, tujipange vizuri ili ndani ya saa moja majina haya waliobakia wamalize kuchangia na hatimaye Waheshimiwa Mawaziri waweze kuja kutoa maoni yao, pamoja na kujibu baadhi ya mambo baadaye tumkaribishe Mwenyekiti kwa ajili ya kuja kufanya majumuisho.

Wahusika wenyewe ni Mhe. Abdalla Muhammed, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Abdi Mosi Kombo na mwisho kabisa Mhe. Abdalla Juma. Baada ya maelekezo hayo sasa naahirisha kikao hiki mpaka saa 11: 00 jioni.

*(Saa 7:00 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Kama tulivyosema mwanzo tuna idadi ya watu 4, tutaanza na Mhe. Abdalla Mohammed nakuomba uchangie chini ya dakika 15 au zisizidi hapo. Tulikuwa tuna kiporo cha Mhe. Mohammed Haji Khalid haya una dakika zako kumi zimalize kabisa.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mwenyekiti, kwa kunisahamu lakini nikakumbusha nina kijiporo kidogo cha kumalizia maelezo yangu ya leo mchana.

Mhe. Mwenyekiti, nitasema jambo dogo katika Wizara ya Afya, wizara hii ni moja katika wizara muhimu sana ingawaje hakuna wizara iliyokuwa si muhimu kwa sababu uongozi ni mnyororo lazima mkamatane ili kipatikane kitu kamili, lakini halafu kila mmoja una umuhimu wake. Wizara hii ndio inayohusiana na afya za wanaadamu na hata viumbe vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja na Idara ya Tiba, Idara inayohusika na kutibu wanaadamu magonjwa mbali mbali yanayotusibu. Mhe. Mwenyekiti, jina la wizara hii inajieleza afya pengine ni tafsiri hata kuwa sivyo kuwa ni usafi. Kwa hivyo unapokwenda hospitali pamoja na kuwa ni pahala ambapo kuna wagonjwa wenye matatizo mbali mbali wenye matumbo ya kuharisha, wenye vijaraha na vidonda vinavyonuka, wenye matatizo mbali mbali wamekwenda pale, ili kupatiwa tiba na yale matatizo waliyonayo kwa lengo la kuyaondoa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, unapokwenda hospitali unategemea kuwa matatizo yako yanayokusibu yataweza kuondoka.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa inaonekana pana mawasiliano hapo katika eneo lako ulilokaa, simu, endelea.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, wengi wamezungumzia hospitali ya Mnazimmoja jinsi ambavyo ni chafu lakini mimi niseme si ya Mnazi Mmoja peke yake, lakini kwa sababu ile ndio iliyo mbele ya macho yetu wengi ndio inaonekana. Lakini takriban hospitali zetu zote hali yake ya kiusafi si nzuri. Si Wete, sio Chake Chake, si Abdalla Mzee iliyoko Mkoani na hii hospitali mama na kubwa ya rufaa ambao tukishindwa humo tunakimbilia pale nao pia ndio pameoza kulingana na maelezo yaliyotolewa tokea asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, pahala pa tiba panatakiwa pawe safi, mtu kenda pale kwa lengo la kuondoa lile ambalo limemsibu, lakini kuna uwezekano kuwa kenda na malaria akaondoka na *dysentery* kwa sababu ya hali ya uchafu ulivyo. Mara nyengine Mhe. Mwenyekiti, muambatano wa vitanda watu wenye magonjwa tofauti ni tatizo. Kwa hivyo ina maana kuwa hospitali zetu zinachukua wagonjwa kinyume na idadi ambayo ya uwezo wake. Yuko mwana falsafa mmoja anasema maendeleo yetu ndio yanayoleta matatizo, kwa sababu watu kuitikia wito wa kwenda hospitali na tukenda hospitali kumbe hazina uwezo wa kutuchukua wala kututibu. Haina uwezo wa kutuweka kwenye nafasi za kukaa kwenye vitanda wala hazina uwezo wa kututibu. Maendeleo haya yamesababisha matatizo kwetu, ni maendeleo kwa sababu watu wameitikia wito kwenda hospitali, ni tatizo kwa sababu hospitali wenyewe hazina uwezo kwa kutoa huduma zinazostahiki kwa wale ambao wanafuata huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo la ufinyu wa bajeti mara nyingine ni msitu wa kujificha kama walivyo watu wengine pengine akija mtu kwa mtu anayemtarajia kuwa anaweza akamsaidia pengine anataka kumkopa lakini kwa sababu hali ya nchi yote haina pesa yule mtu atatwambia hali kwa kweli ngumu, kwa kila mtu na ndio hivyo Serikali na Wizara zote zilivyo kila Wizara inasingizia inadai kuwa hili halikutekelezeka kulingana na ufinyu wa bajeti tuliopangiwa. Lakini Serikali *alhamdulillahi* inajisifu kuwa inakusanya pesa nyingi zaidi kuliko ilivyokusanya nyuma. Sasa sifa hii Mhe. Mwenyekiti, ingemalizia katika matumizi ya Wizara zetu. Je, tujaalie huyu mkusanyaji pesa hazitoi na kama hazitoi na lengo katika Serikali kwenye Wizara mbali mbali yeye anazipeleka wapi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ili ufanisi upatikane katika utendaji wa Wizara ya Afya angalau ile bajeti iliyopitishwa waweze kuipata ili waweze kutuhudumia kulingana na hali ilivyo, vyenginevyo hospitali itaendelea kuwa chafu na kunuka ingawaje kunuka kwa Zanzibar ndio sura yetu kwa sababu hata mji unanuka. Kwa hivyo ilivyokuwa mji ambao unatarajiwa uwe msafi unanuka hospitali ikinuka pia si ajabui sana, kwa sababu ile harufu ya uvundo pengine ndio sifa ya mji wa Zanzibar.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ili kuondokana na hali hii, ili Wizara ya Afya iweze kutekeleza majukumu yake Wizara inayohusika na ugawaji wa fedha za matumizi waijaalie Wizara hii katika Idara zake mbali mbali bajeti waliopangiwa ili waweze kutoa huduma zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tumekumbwa na magonjwa mengi siku hizi na yaliyo maarufu zaidi ni mawili makubwa, ama *pressure*, sukari. Hutozungumza na watu 10 ikawa japo mmoja akawa hanalo tatizo hili. Sijui Wizara imefanya utafiti gani kuweza kubaini kwa nini magonjwa haya yanaongezeka kwa kasi sana katika visiwa hivi. Kuna kitu ambacho tunatumia kinachosababisha hivyo na viko Wizara ina wito gani au inatoa taaluma gani ya kutuelimisha kuweza kuacha kutumia vyakula vya aina hiyo ili kupunguza tatizo kubwa linalotukabili la *pressure*, sukari haya ni matatizo makubwa na yanatuathiri wengi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nina hakika kuwa dakika zangu tano zimemalizika kwa hivyo naomba kumalizia hapo na ahsante sana kwa kunipa muda wangu.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazingatia muda sana kwa sababu wajumbe wengi weshayasema, lakini itabidi tutulie mkazo. Mhe. Mwenyekiti, ripoti kila mwaka zinakuja na kila mwaka tunazichangia na kila mwaka zinakuja vile vile. Kwa sababu matokeo ya ripoti zetu ninafikiri hazisikilizwi wala hazizingatiwi kwa maana hiyo kila leo tunabakia pale pale hospitali hakuna dawa, walimu hawalipwi mishahara, posho ndogo, haya yote tuliokuwa na jukumu la kusimamia ni sisi na ninafikiri wakati wa bajeti unakuja huo kila mmoja kama atakuwa anajua wajibu wake sawasawa, kama ni mwakilishi basi nina imani mengi yataondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na kusema kwamba kinachonishangaza sana ni kwamba wizara ambayo inahusika na mapato wao ndio wanaogawa haya mapato. Wizara husika zinajieleza mbele ya Wizara ya Fedha kwamba mimi mwaka huu nitafanya hiki na nitafanya hiki kwa thamani fulani na matokeo yake Wizara ya Fedha wao ndio wanaoamua na sio wizara, kwamba sisi uwezo wetu ni kuwapatia nyinyi katika ujenzi wa maabara kiasi fulani ya fedha. Wakijua kwamba Wizara ya Fedha sisi fedha hizi tutazipata na tutazikusanya, kwa maana hiyo

uwezekano wa kuwapatia Wizara ya Afya fedha fulani kwa ajili ya kutekeleza mradi fulani tunao wala haamui yeye, wanaoamua Wizara ya Fedha. Lakini cha kusikitisha Mheshimiwa, inapofika sasa ugawaji huo wa fedha kama wamepangiwa asilimia 80 anapata asilimia 20 nani mkosa.

Waziri wa Fedha akija hapa atatwambia tumekusanya mara hii bilioni thalathini na tano, kuna mfuko mwengine zinapokwenda hizi fedha makusanyo hayo au mfuko ni ule ule wa Serikali ulioidhinishwa hapa kwamba zikipatikana zitumike hivi, mnatushangaza.

Leo tunabakia tunamlaumu Waziri wa Elimu hujajenga mabanda, unamlaumu Waziri wa Afya hujanunua DNA anunue fedha atoe wapi. Kwa hivyo chanzo cha haya Mheshimiwa ni Wizara ya Fedha, wao wanapanga lakini wao hawasimamii na fedha wanazozikusanya hatujui zinakwenda wapi, kama umepata bilioni ishirini na tisa kwa nini Wizara ya Kilimo unampa asilimia 20 ya makisio uliyomuwekea yeye mwenyewe.

Wewe Wizara ya Fedha ndie uliyesema kwamba mimi nitakupa kiasi fulani na umezikusanya, kifua mbele hapa unatwambia kwamba umekusanya bilioni thalathini na tano mwaka huu, kuna mfuko mwengine zinakwenda, mbona haziendi huko zinakotakiwa. Sasa hapa tujuwe wajibu wetu, bajeti inakuja sio tena tuje tutizame pita, imekubalika, ndio, haina maana tusimamie wananchi wapate haki zao. Mabanda ya Skuli yatajengwa kutokana na mfuko wa Serikali, Wizara ya Elimu haitotoa fedha yeye bali ni Wizara ya Fedha ndio itakayotia fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabanda ya shule.

Mhe. Mwenyekiti, lawama hizi zote zinakwenda kwa Wizara ya Fedha wao ndio wanaokusanya kwa nini hawazipeleki na wanazipata, kila mwaka tumeongezeka asilimia 4.5, tumeongezeka asilimia 6.7 *what is it?* Mbona haziendi katika matumizi. Kuna matumizi mengine ya siri Mhe. Waziri hayupo lakini aje atwambie hapa, kama kakusanya hivyo kwa nini hazipo.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukuwe muda wako mrefu lakini niende katika mwalimu. Kila mwaka tunapozungumzia mapungufu na uzembe tunawazungumzia walimu, wamekosa nini? Hapa ukija walimu hawapati posho walimu, wakenda kusainisha mitihani hawapati walimu, wao hawatengewi fungu, wao ni watumishi wa umma. Sasa hapa wajumbe wengi wamezungumza kwamba kuna walimu 69 walimu hawa hawajalipwa mishahara yao ya Oktoba. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mshahara unapita ngazi tatu hebu Serikali twambieni Wizara ya Elimu wao wanatayarisha kwamba sisi tuna mfanyakazi fulani Wizara ya Utumishi wa Umma ndio wanaemuombea, tuna mfanyakazi ana digrii ya sayansi, wao wanaipeleka Wizara ya Fedha alipwe na Wizara ya Fedha.

Sasa hiki kitendawili cha kuwa walimu hawajalipwa mishahara yao ya Oktoba, uzembe huu umefanyika wapi? Wizara ya Fedha hawajatoa fedha, Utumishi wa Umma hawajampelekea ripoti yake kwamba mfanyakazi huyu kaajiriwa rasmi na kiwango chake cha mshahara hiki au Wizara ya Elimu Mhasibu kazitafuna?

Mheshimiwa hizo ndio ngazi za mshahara, sasa hapa tusiseme tu hebu twambieni nani aliyekuwa anahusika na hili, mshahara wao haujatoka Wizara ya Fedha, au Utumishi wa Umma hawajapeleka ripoti yake kwamba huyu ni muajiriwa. Lakini kama ni hivyo kwa nini mwezi wa Novemba wamepata mshahara.

Sasa je, Wizara ya Fedha wamezipeleka fedha Wizara ya Elimu hawakulipwa, hebu twambieni Serikali nani aliyehusika mpaka leo tunasema hatuna walimu leo tunawa-*demoralize* zaidi kwamba nyinyi msifanye, mshahara mtu haki yake humlipa, nani muhusika hebu twambieni nani aliyekuwa hajafanya wajibu wake, amefanya uzembe huu Wizara ya Fedha,Wizara ya Utumishi wa Umma au Wizara ya Elimu, alipofika Mhasibu katafuna kasema mishahara hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, ni aibu na ndio ukakutia waandishi wengine wa vitabu vya nchi nyengine na wao wanajumuika na wawakilishi katika kuzikosoa serikali zao lakini matokeo yake unaishia jela. Akina Ngugi wa Thiong'o wamesema hapo wao *No Longer at Ease,* akina Chinua Achebe na wao wameishia jela wanasema *Things Fall Apart* na sisi tunataka tu-*Fall Apart?* Hakuna lazima kila mmoja awajibike. Leo tukitia ripewa ni yale yale mwalimu hajapata mshahara, tumesimama tu wajibu wetu nini sisi kama ni Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme sana niende katika Bodi ya Elimu ya Juu, sisi tunasema tunawakopesha wanafunzi wetu vijana kwa ajili wasome, tunawapa mikopo wanakwenda kusoma nchi mbali, wengine wanasoma Tanzania Bara wengine wanasoma hapa lakini cha kushangaza hii bodi ya mikopo lazima ipewe fedha ili hawa wanafunzi wasome. Lakini leo mwanafunzi anafika Mzumbe anatoka Kisiwani Pemba kwa mfano yuko Kojani kachanga nauli anapofika pale anaambiwa *admission fee* Bodi haijaingiza fedha za *admission fee,* kwa hivyo wewe rudi kwenu nani muhusika, Wizara ya Fedha kwa nini hawaiingizii Bodi, huwapi pesa kwa wakati wanaotakikana kusoma, kusoma kuna wakati wake sio kila wakati.

Unajua kwamba *admission* inaanza mwezi Julai, kwa nini huitilii Bodi pesa akaweza kuwalipa wale, halafu unakuja hapa aa kuna hiki tunapata pesa bilioni hamsini, bilioni ngapi zimeongezeka ziko wapi, kwa nini unawasumbua vijana. Ukenda huko hivi sasa kuna utaratibu eti mtu wa fedha anatoka anakwenda kuwalipa watu *cash!* Wewe zako hizi, anakwenda Mzumbe anakwenda Chuo cha Kiislam Morogoro ndio utaratibu huo, pesa zimeshachelewa hawatiliwi. Ukenda huko kwenye Bodi yenyewe unakutia mtu huyo huyo anasoma ICT yuko Morogoro analipwa pesa tofauti na anayesoma ICT ambaye yuko Chuo cha Chwaka.

Sasa ukenda Chwaka anakwambia sisi *admission* hatuna wanafunzi kwa sababu wanatafuta mkopo ambao utakuwa ni mkubwa yule yule wa ICT, tunafanya nini? Lazima tuwe *systematic,* tupeleke fedha haraka na kwa wakati wanafunzi wapate kusoma. Leo wengine wanafika njiani wanarudi kwa sababu *admission* haijapatikana, na *admission* anatoa nani? Hatowi Wizara ya Elimu inatoka Wizara ya Fedha aingiziwe Bodi ya Mikopo zile fedha ili yeye azigawe. Leo unakuja hapa unatwambia tumepata bilioni 35.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Kazija Khamis Kona:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza mchango wangu naanza na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto, Idara ya Mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, katika agizo kamati imeagiza kwamba Idara ya Mikopo ina tatizo la ofisi, na wizara imejibu kwamba tatizo hilo linashughulikiwa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuwa hili ni tatizo la ofisi linapelekea hata kufanya kazi zao wasifanye ipasavyo, hili ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kabla ya mipango yao haijatimia ya kulitengeneza jengo lililokuwepo Mwanakwerekwe watafute namna nyengine ya kuwapatia ofisi watakayofanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Kilio hiki kila siku kipo tokea wizara hii haijahamishwa ipo katika Wizara ya Uwezeshaji na Habari tulikuwa tunalipata tatizo kama hili, sasa na kila siku mtu analalamika kwa tatizo hili mwisho wake unamvunja moyo. Kwa hiyo, wizara itafute namna ya kuwatafutia sehemu ama kuwakodia sehemu nyengine itakayokuwa na nafasi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea agizo jengine la tano Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Katika agizo hili Mhe. Mwenyekiti, inatuelezea kwamba sitaki kuisoma yote naomba nisome kipande kidogo, katika jitihada hizo imeonekana kwa kuwa tayari idadi ya kesi zilizopata hukumu inaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hizi kesi ambazo zilizopatiwa hukumu ilikuwa Mhe. Waziri aziainishe ni kesi ngapi zimepatiwa hukumu baada ya kupewa agizo na kamati. Mhe. Mwenyekiti, lakini humu utekelezaji wake tumeambiwa tu kwamba zimepungua kesi ambazo zimepatiwa hukumu. Kwa hiyo, Mhe. Waziri aje atufahamishe atuambie ni kesi ngapi tokea kupata agizo hili zilizopatiwa hukumu, na kesi ngapi hazijapatiwa hukumu zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nihamie katika Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu imetuelezea kwamba inashughulikia suala la kumtafutia hatimiliki za maskuli, lakini pia na yeye hawajatwambia kwamba mpaka sasa hivi wamefika hatua gani. Hapa wametuelezea tu wamepeleka orodha katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati lakini hawajatuelezea kwamba kama kuna skuli ambazo tayari zimepatiwa hatimiliki au la. Sasa Mhe. Waziri aje atufafanulie vizuri zaidi ili tuzijue skuli ngapi zimepatiwa hatimiliki na ngapi hazijapatiwa hatimiliki na ni ngapi ziko katika hatua ya kupatiwa hizo hatimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea na mchango wangu hiyo hiyo Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu kamati imetoa agizo, agizo ambalo la tatu lakini Wizara ya Elimu ilijibu maagizo hayo kwamba wameyapatia ufumbuzi kwa kushirikiana na washirika mbali mbali wa maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa ufupi ufupi kwa kujali muda. Changamoto hizo ni kama vile upatikanaji wa vitabu vya kusomea na kusomeshea kwa darasa la kwanza hadi la nne. Vitabu vya darasa la nne na la sita vimo katika hatua za mwisho za ununuzi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Wizara ya Elimu sera yake ya mwaka huu iliamua kwamba wanafunzi kuanzia darasa la sita mwaka huu wataanza kufanya mitihani ya Taifa. Lakini hadi muda huu Mhe. Mwenyekiti, vitabu hivyo havijapatikana, havijanunuliwa ndio kwanza viko katika utaratibu wa kutafutwa vitabu hivyo. Mhe. Mwenyekiti, sasa wakati vitabu hivi havijapatikana hadi muda huu mwezi wa tatu sasa, hivi tutategemea nini kwa wanafunzi wetu au tutapata matokeo mazuri kwa wanafunzi wetu kutokana na hali hii?

Kwa hiyo, Mhe. Waziri aje atufahamishe ni lini vitanunuliwa vitabu hivyo na kusambazwa katika mashule ili walimu wapate kuwasomesha vizuri wanafunzi na mitihani yao waifanye vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kwa sababu kila mwalimu ananyofoa nyofoa tu achukue kitabu hiki asomeshe, achukue sehemu hii apate akamsomeshe mwanafunzi kwa tatizo la kutokupatikana vitabu. Sasa Mhe. Waziri hili liharakishwe haraka vitabu vipatikane kwa haraka sana ili wanafunzi wetu wapate kusomeshwa na wapate kufanya mitihani vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nihamie Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wengi hapa wamezungumzia suala la usafi, usafi ni muhimu sana na wameielezea Hospitali ya Mnazi Mmoja, ni kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja ni chafu, lakini tuiombe wizara ijitahidi na hilo japokuwa inasema ina changamoto kubwa na changamoto hiyo kubwa ni bajeti. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa ninajiuliza hii changamoto kubwa ya bajeti ikoje ikoje, kwa sababu kila mwaka tunaambiwa uchumi umekuwa, sasa mimi kwanza nije nifahamishwe huu uchumi unakuwa vipi?

Kwa sababu kama uchumi unakuwa na uchumi ukikuwa tutaweza kutatua katika zile shughuli zetu kuzifanyia kazi, lakini leo tunaambiwa uchumi umekuwa, sijui asilimia ngapi, lakini ukija katika utekelezaji katika mawizara, idara zote zinasema changamoto ni bajeti ndogo. Na hiyo wanayoiomba hawapatiwi kwa wakati sasa sijui tutafika wapi Mhe. Mwenyekiti, sijui sisi tutaimarika lini na changamoto hii ili idara zetu zionekane zinafanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili linawarejesha nyuma watendaji kufanya kazi zao, wanaumiza vichwa sana kutupangia mipango ya kuendelea katika nchi yetu lakini wanarejeshwa nyuma na suala la bajeti. Kila idara unayokwenda unaambiwa bajeti ndogo, bajeti haitoshelezi, bajeti hivi na hivi na huku waziri hapa akija na koba lake lile begi anatwambia uchumi umekuwa kwa asilimia kadhaa. Sasa tuamini vipi huu uchumi unakuwa vipi? Tunaomba tufahamishwe namna ya kukua uchumi na namna ya matumizi ya kuongeza shughuli za serikali ili wananchi wapate manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru. (*Makofi*)

**Mhe. Abdi Mossi Kombo:** *Bismilahi Rahmani Rahiim***.**

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi karibu ya mwisho, yaani karibu ya kichinja mimba.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah kwa hivi sasa kutuwezesha kufika hapa katika Baraza letu tukufu na kuchangia michango yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu kama walivyoanza wenzangu, nitaanza kuchangia kwa vile ilivyokuwa na mimi mmoja katika Wajumbe wa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii nitachukua dakika kidogo sana kukumbusha.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitaanza kama walivyoanza wenzangu katika Wizara ya Afya katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, kwa sababu Hospitali ya Mnazi Mmoja nitaizungumza sana kwani ndio hospitali mama kwa Zanzibar. Hata mgonjwa akishindwa Matemwe analetwa Mnazi Mmoja, akishanda Pemba analetwa Mnazi Mmoja, lazima tuizungumze Hospitali hii ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja inaitwa Hospitali ya Rufaa, lakini mimi naomba Mhe. Waziri wa Afya aje anifahamishe hii rufaa maana yake nini?

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa lakini hospitali hii ina sifa, sifa ya kwanza ni mbovu. Hospitali ya Rufaa ukipanda ngazi ukienda katika roshani ya mwisho utakuta ma-*hardboard* yote mabovu. Ukija ghorofa ya pili wanapolazwa wagonjwa wa sukari panavuja na hayo Masika sasa hivi yanakuja sijui hawa wagonjwa watakuja kuwa vipi wakati Hospitali ya Rufaa ni mbovu, inavuja. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ninaiomba wizara iangalie Hospitali yetu ya Rufaa jinsi ilivyo.

Jambo la pili katika hospitali zetu zote za Unguja hivi sasa nachanganya na Pemba wale wafanyakazi bado hawajakuwa na utaratibu wa kuwabembeleza wagonjwa, mgonjwa akifika pale kwa muuguzaji hana maneno mazuri anayoyapata, atapata ukali tu na kukaripiwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri azungumze sana na wafanyakazi wa mahospitali zetu hizi za Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika ukurasa wa nne Kitengo cha Huduma za Macho. Mheshimiwa katika kitengo cha macho kuna tatizo la hili jengo ni dogo na hata hifadhi ya madawa yanakuwa hayahifadhiki vizuri. Kwa hivyo, naiomba wizara iangalie sana jengo hili la Hospitali ya Macho.

Mhe. Mwenyekiti, ili kwa kujali muda nakwenda katika Wizara ya Uwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, mimi niwape pongezi Idara hii ya Ustawi wa Jamii kushirikiana na Wizara ya Fedha kuwalipa wafanyakazi ambao waliokuwa wanadai fedha zao shilingi milioni 100. Kwa hivyo, hapa nawapa pongezi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali muda ninakwenda katika Wizara ya Elimu, Kitengo cha Elimu Mbadala. Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kina ukosefu wa walimu katika elimu mbadala. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri azingatie sana katika kitengo hiki cha elimu mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia namkumbusha Mhe. Waziri miaka miwili iliyopita Mhe. Rais aliweka jiwe la msingi katika Kijiji kimoja cha Pwani Mchangani, kijiji hicho kilijenga ukumbi mkubwa wa kufanyia mitihani wanafunzi na Mhe. Rais alikwenda kuweka jiwe la msingi na Mhe. Waziri yeye aliweka ahadi ya kuliezeka. Kwa hivyo, namkumbusha Mhe. Waziri jengo hili bado wale wananchi wamenituma nije nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba lile jengo linataka kuezekwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali wakati wako na mimi nikiwa ni Mjumbe wa Kamati hii ningependa kukumbusha tu. Ahsante, nakushukuru.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii angalau niweze kutoa machache katika hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kujali muda wala sitaki niseme muda mrefu sana hasa ukizingatia hoja hii toka asubuhi leo Waheshimiwa Wajumbe wanaichangia hapa na wameshasema mambo mengi ambayo pengine nilikuwa nimepanga kuyasema, lakini kwa sababu tayari wameshawakilisha wananchi hakuna haja ya kuyarudia isipokuwa yale ambayo kwa umuhimu wake inabidi lazima tutulie mkazo kidogo. Mhe. Mwenyekiti, katika kutia mkazo nataka na mimi nigusie kidogo Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali ile ndio kimbilio la wanyonge, juzi Mhe. Naibu Waziri hapa wa afya alisema watu milioni 1,300,000 wote wanaitegemea Hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa si ubishi kwamba wanyonge wote wanakimbilia pale, mtu akiwa na pesa zake pengine anaweza akenda pahala pengine, lakini wale masikini za Mungu hawana budi waende Mnazi Mmoja. Sasa Mnazi Mmoja kuna tatizo la siku nyingi sana na Waheshimiwa Wajumbe wamelisema muda mrefu sana lakini bado nasikitika sana kuona tatizo hili bado linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo lenyewe ni tabia mbaya walizonazo wale madaktari wetu wale wanaotoa huduma pale, lugha zao hadhirizishi na hata utendaji wao wa kazi hauridhishi. Sasa imefika pahali mpaka wale wananchi sasa wanajua kama ukitaka ujiudhi wewe basi uende Mnazi Mmoja.

Kwa msingi huo sasa na wao wananchi wameanza kubadilika wakienda pale hawana imani kwamba watapata maneno mazuri, maana yake hakuna mtu ambaye anahitaji maneno mazuri kama mgonjwa, ile kumpembejea kwa maneno mazuri ni sehemu ya tiba anapata moyo. Lakini kutokana na lugha mbaya ambazo wenzetu hawa, ndugu zetu wa damu kwa kweli wanazitumia mpaka wale wananchi sasa wakienda pale na wao hujitayarisha na kauli mbaya vile vile. Unaweza ukamkuta mwananchi anaripuka ovyo pale, kwa sababu tayari keshajenga ndani ya nafsi yake kwamba hapa siwezi kupata kauli nzuri.

Kwa hivyo, na yeye anajitayarisha kwa kauli mbovu. Sasa daktari kauli mbovu na mgonjwa kauli mbovu matokeo yake hapana kinachokwenda, ni aibu. Sasa bado mimi naendelea kuwanasihi sana madaktari ni ndugu zetu wewe huwezi kumtibu Mzanzibari au huwezi kum-*treat* Mzanzibari yeyote akawa si ndugu yako, *once* wewe ni Mzanzibari na yule na kama unataka kupeleleza hebu muulize mmoja akija, wewe umezaliwa na nani, unatoka kijiji gani, mwisho utakuta munakutana kwa damu kabisa. Kwa hivyo, yule ni ndugu yako usimtolee kauli mbovu haina haja, na hata asiwe ndugu yako.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda hoteli pale *reception* pale wale wanaokupokea wanapewa mafunzo maalum ya kuweza kuwapokea wateja na wewe mwenyewe utaridhika kwa huduma unayoipata ya maneno tu. Sasa na hawa madaktari wetu lazima wapewe lugha za kuwapoza wale wagonjwa, sio kumtolea mtu maneno ya kijeuri yanamvunja moyo, kama ni mgonjwa wa *pressure* basi inaongezeka, kama ni mgonjwa wa sukari, unaweza ukauwa. Sasa hili tutaendelea kulisema kwa sababu linaendelea kutokea.

Jambo jengine nimewahi kusema na nitaendelea kusema, kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inatumiwa na ndugu zetu wengi Wazanzibari, ukifika ule wakati wa kuangalia wagonjwa pale saa saba, hebu nenda ukaangalie yale makundi ambayo yanapanda mule kuenea katika wodi tofauti za wagonjwa.

Sasa naendelea kusema kwamba miundombinu ya hospitali ile ni ya zamani mno kiasi ambacho huo wakati iliyojengwa ilikuwa inahudumia watu wachache sana, zile ngazi za kupandia pale zilikuwa zinatosha wakati huo, hata ikitokea *emergency* watu walioko kule juu kwa wakati huo wangeweza kuzitumia ngazi zile tatu kwa kushuka na wakawahi kutoka. Leo *population* imeongezeka wanaokwenda kuangalia wagonjwa wao pale ni wengi, lakini miundombinu ile ile haijaongezeka.

Sasa Mwenyezi Mungu atusaidie sana lisije likatokea balaa wakati ule watu wanatizama wagonjwa lakini watakufa wengi. Naiomba sana wizara na sio wizara tu, Serikali nzima ijipange namna ya kuboresha miundombinu ya hospitali kama ikitokea *emergency* watu waweze kuepuka hatari.

Mhe. Mheshimiwa, ni hatari sana, tusione halijatokea ikawa sisi kazi yetu Wazanzibari ni kujifunza baada ya jambo kutokea, hebu tujikinge, wakati tunao wa kujikinga. Kwa hivyo, wizara iombe serikalini na iandae mpango maalum wa kuhakikisha kwamba wanaweka ngazi za kutosha za kutokea watu pale likija likitokea tatizo.

Jengine ambalo kwa kweli rafiki yangu Mhe. Makame Mshimba, jana alisema mpaka akatoka machozi ni ukosefu wa kuwa na *DNA Machine*. Hili ni tatizo sugu Zanzibar, mimi najua kuna ukwasi wa fedha serikalini, lakini watoto wetu wanadhalilishwa katika nchi hii katika kiwango cha kutisha. Sasa ukienda katika Ofisi ya *DPP* anakwambia hatuwezi kuthibitisha kesi kwa sababu hatuna *DNA Machine* na sijambo la kuweka uporo miezi sita lile, ni jambo likitokea lichunguzwe pale pale, *within twenty four hours* lijulikane ukweli wake. Kwa hivyo, Serikali ijipange.

Mhe. Makame Mshimba, alisema jana kwamba tulipotaka kununua meli tuliona haja ya kununua meli, tulijipanga tukapunguza bajeti za hapa na pale, tukafanya hivi, mwisho wake sasa meli tunayo keshokutwa itakuja. Hivyo hii *DNA Machine* ina ughali kiasi gani ya kwamba mpaka leo tuache tu watoto wetu wanadhalilishwa katika nchi hii na ushahidi haupatikani na kwa sababu ushahidi haupatikani watu wanaendelea kudhalilisha watoto, mpaka lini?

Kwa hivyo, naomba iwe ni *concern* maalum sasa ya Serikali kuhakikisha hata kama ni chombo, hiki ikiwa Serikali haina pesa hebu pigeni *donation* shilingi ngapi twambieni tutatoa. Wawakilishi watachangia, Wabunge, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi tuchangeni, ndio nchi ya kinyonge inavyokwenda tutafanya nini, lakini hatuwezi kuendelea kuacha watoto wetu wakiteswa namna hii haiwezekani, lazima tutafute ufumbuzi. Hilo jengine.

La mwisho, ni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imekuwa ni mtindo siku hizi masuala ya sekondari ya juu na masuala ya vyuo wenzetu wa Tanzania Bara au Baraza la Mitihani wanakuwa wanatubadilshia kibao katikati ya safari. Mwaka juzi walianza kufuta masomo ya

Dini ya Kiislamu na ilikuwa vijana washajipanga kwa ajili ya kuwa ndio *combinations* zao wanasoma wakaanza kuyatoa, tukapiga makelele wee, wakayarudisha.

Mwaka huu kuna matokeo mengine yametokea kuwa wanafunzi wa *'A' Level* wamefutiwa *combinations* zao na hata baadhi ya vyuo vikuu kuna tatizo hilo. Wewe ushasoma mwaka mzima halafu unakuja kubadilishiwa *combinations* katikati ukaambiwa sasa acha hii anza kusoma hii mwaka mzima ushaupoteza. Sasa hii si nzuri na inatutia hasara kila siku na ndio maana tukawa tunasema kwa nini Wazanzibari hatui na Baraza letu la Mitihani, siku zote tutaendelea kuwa na Baraza la Mitihani la Watanganyika wakatufanya wanavyotaka kwa sababu gani?

Maana yake tuna uhakika ni mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba Wazanzibari wanawafelisha kila siku.

Kwa hivyo, mimi bado kama Mzanzibari halisi naendelea kusema Baraza la Mitihani halifai kabisa kuwa jambo la kufuata tuwe na letu. Maana kuna madai kwamba ukiuliza wanakwambia hao *NECTA* sijui, wanakwambia walitoa habari mapema, lakini wizara yenyewe haikulifanyia kazi, hebu tupeni ufafanuzi Wizara ya Elimu.

Kwa sababu hivi sasa wanafunzi wanaosoma *Form V* juzi wamepewa taarifa kuna *combinations* ya Kiingereza, Kiswahili na *Geography* wameifuta, wamesema Kiingereza ni lugha, Kiswahili ni lugha, *Geography* si lugha itoke pale ikae Kiarabu, mwaka mzima tayari huu wanasoma *Geography*, ukiwahoji wanakwambia tuliwaambia zamani Wizara ya Elimu hawakutaka kurekebisha. Hebu tupeni ufumbuzi Wizara ya Elimu hivi ndivyo ilivyokuwa au ni watu wanatushitukizia halafu wanatafuta sababu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja.

**Mhe. Raya Suleiman Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, hata sitaki kuchukua muda wako mkubwa. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwenye kutujaalia tukaja hapa salama na tukaweza kurejea tena.

Mhe. Mwenyekiti, nije kidogo katika Wizara ya Afya, kwanza niwapongeze mawaziri wote waliosoma ripoti zao pamoja na wenye viti. Mimi sitosema kuwa Mnazi Mmoja tukaikalia kuwa ni chafu, Mheshimiw,a mahospitali yote ni machafu watendaji hawako *serious* na kazi zao. Kwa sababu sehemu kama zile zilizokuwa zinaingia watu kutoka sehemu mbali mbali, mnataka watu makini wa kuweza kusimamia ule usafi na mle mkawa mko salama. Watu hawana roho ya usalama wa maradhi ya kuambukiza kwa sababu watu ni wengi wanaoingia katika hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitazungumza kidogo hapo Mnazi Mmoja kwanza nitazungumza hospitali yetu ya viungo. Nawashukuru madaktari wote waliopo na nashukuru pia mawaziri wetu. Kila siku tunalalamikia hospitali za viungo walemavu kuweza kupata watu makini wa kuweza kutufanyia mambo na kutuboreshea hali zetu kwa viungo na upimaji na kupata hospitali ambazo tuweze kupata madaktari makini wa kuweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kila siku mimi huwa nalilalamikia jambo hili kwa sababu tofauti ya mtu kwa mtu, tofauti za watu walemavu ni tofauti ya kiungo pengine jicho, mkono au mguu. Sasa

mazingira ndio yaliyokuwa yanatufanya watu wenye ulemavu tupate dhiki sana katika maofisi mbali mbali. Nashukuru lakini juzi nilipokwenda hospitali kile chombo nilichokuwa nikikipigania sana kilinipandisha juu ghorofa ya pili kule. Kwa hivyo, nawapongeza sana mawaziri na watendaji wote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilikwenda pale kidogo nilisikitika, kuna mama aliyeandikiwa operesheni na operesheni wake ulikuwa ni saa moja na nusu, nafika pale mimi saa tatu mama yule operesheni hajapata na daktari alikuwa keshamuweka ndani akamtoa na akaambiwa hapana vifaa. Hospitali kama ile kubwa kwa nini visiwepo vifaa vya kufanyia operesheni. Akaweza kupiga simu akaja dada yake akaandikiwa vifaa kwenda kuvinunua nje, ikiwa ni kuvinunua kwa nini hospitali isiweke vifaa yale malipo yakenda pale na kila siku sisi tunapiga kelele humu jamani, mambo mengine yatatoa muda wa mtu hata haujafika.

Kwa mfano wewe umeshafika pale unaumwa umeshaandikiwa operesheni unaambiwa hapana ganzi, hapana dawa, hapana mabendeji ya kufungwa, yale yanayonunuliwa yanapatikana wapi ukishaandikiwa pale. Hili ni jambo nalo vile vile linatushangaza na tunaomba Serikali yetu, mawaziri na watendaji wote *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awawezeshe wajitahidi haya yaondoke.

Halafu nitakuja Hospitali ya Chake Chake. Hospitali hii tunaitumia watu wengi ni kungo kwa sababu iko *centre,* kubeba watu sehemu mbali mbali wakija pale. Kwa mfano wanaopata rufaa Micheweni wanakuja pale, wanaopata rufaa kutoka Wete wanakuja pale pale wanahamishiwa Mkoani, lakini sasa Mkoani hakuna huduma kwa sababu kunajengwa.

Linalosikitisha Chake Chake kwa nini ikiwa hapana daktari kwa huduma za akinamama au za upasuaji wasitoe taarifa kama vile ukiwa umeme unazimwa au maji hakuna wakenda pale kinamama, kinamama wanafika pale wanasumbuliwa na uchungu, hali ni mbaya ni nzito ndio anapigwa *transfer* pengine kenda usiku au asubuhi mpaka saa sita za mchana wanamuondoa pale wanasema apelekwe Wete, mama akifika njiani anakufa.

Hili ni jambo la kusikitisha sana, tunaomba sana Serikali kupitia kwa mawaziri na watendaji wote hili walione, ikiwa huduma pahala hapana itolewe ripoti mapema watu wajue nikitoka hapa na mgonjwa wangu naelekea sehemu iliyokuwa ina huduma.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wizara hii hapa wanaweka baadhi tu ya maskuli yenye matatizo. Mheshimiwa, matatizo katika skuli zote yamo maana tunatembea. Wanafunzi kukosa walimu wa sayansi, vikalio hakuna yaani wanafunzi wanakaa chini, ni madarasa mengi na skuli nyingi kadhia hii ipo.

Halafu mimi nitazungumza katika skuli zetu muna watu ambao wamejumuishwa katika elimu mjumuisho, tunaomba walimu wende na wakati kwa wale watoto wanaopelekwa mule. Kwa sababu wale watoto sio wa kawaida wengine, ukimuona ni mtoto wa kawaida, lakini ana maumbile tofauti na wale watu waliomo mule.

Sasa mwalimu ukiwa mkali unamtolea ukali mtoto kama yule kitu gani atakachoondoka nacho pale, tangu hapo hiyo elimu mjumuisho kweli tumeitaka lakini kwa kiasi kikubwa haina mantiki

kwa watu wenye ulemavu, baadhi yao hawafahamiani na walimu, walimu ni kidogo wa kusomesha katika fani ile na hapa mara moja vile vile nilisema, kukichongwa madawati ya kukalia basi kuwe na vikalio maalum kwa watoto wale wengine wana tabu kuingia katika madeski yale.

Hayo niliyasema hapa, tukenda kilio ni hicho, watoto hawana vigari kama wataingia na vigari vyao, ukienda mtoto anasota chini, anayekwenda kwa tumbo anatembelea chini, hivyo hivyo na walimu wote kila mmoja wakati neno lile si lake halimuumizi, tuna shida.

Tunaomba wizara ifikirie kupitia serikalini kwa haya matatizo madogo madogo yaliyomo na *Inshaallah* tutakapofanikiwa Mwenyezi Mungu atujaalie tutaweza, lakini kwa kujipanga. Kwa sababu ikiwa neno hunalo rohoni na hapa huwezi ukalifikiria na ukaweza kuondoa matatizo yake.

Mhe. Mwenyekiti, nije Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Hapa nitakuja kwa udhalilishaji tu sina mambo makubwa. Udhalilishaji wa kijinsia ni mwingi na hasa watoto wenye ulemavu na kesi zinakwama zinaambiwa kuwa hazina ufumbuzi kwa kuwa hapana ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, upatikane ushahidi gani, ushamkuta mtu anakudhalilishia mwanao au katokea mtu kamkuta pale pale kwa sababu gani asipelekwe hospitali ukapatikana ushahidi. Kwa sababu tuliambiwa watoto wakikutwa vile wasikoshwe wakikoshwa ushahidi unapotea, lakini watoto wanakutwa na wakipelekwa lakini badala yake hapana ushahidi. Walemavu wengine wanaweza kujieleza na wanaweza wakatoa mfano pengine hata mtu akajulikana.

Kwa mfano, kabakwa na ikiwa mtu ni bubu ukimpeleka Mahakamani anakuonesha na kuweza kukwambia kwa ishara, unaweza ukampeleka pale mtu ukamgeuza na huyu, siku ukamuweka na huyu, anaweza akatoa ushahidi na akapatikana, lakini kesi zile hazijulikani zinamalizia wapi.

Naomba Serikali iwe makini sana katika kupeleka kesi basi kesi inaanzia polisi. Polisi wasitufichie kesi kwa sababu hawa watoto ni wetu shirika ni ndugu zao, ni mama zao, ni watu wote hawa, tukisema wadhalilike tena wanadhalilishwa kike na kiume. Ushahidi tunao na kesi tunazo wenyewe tunafuatilia na kesi hizi haziendi pahala popote. Utasikia watu wanakwenda kusema kuwa watu hawa kesi zao zifutwe, watu wanakamatwa wakatiwa ndani kwa ushahidi badala yake watu wana pesa zao wanawatoa na kwa sababu gani atolewe na ushahidi umeshakwenda?

Mara moja nilitoa mfano mtu alimuona mwenyewe, alikwenda kisimani Mkoani anarudi pale akamuona mtoto wa fulani yule anatoka mwangu na mimi nina mtoto mgonjwa na alipokwenda mtoto keshamuhujumu, yule mtoto alikimbizwa. Wakati mwengine hawa wanaoendesha kesi ndio wanaotudhalilisha, tunaomba waweze kuwa makini kesi hizi zitakapopelekwe kuzichukulia hatua haya madudu yasiyotosheka Mwenyezi Mungu ayalani, wanawake wote waliokuwemo, wewe mtoto kasongomana unamuona vipi yule; wanawake wote waliomo unampenda yule?

Sasa ikiwa unampenda yule kwa nini huji kunipokea mzigo, ukiwa unampenda njoo unipokee mzigo nitakuozesha, tutashirikiana tutamlea, lakini unakuja kumuhujumu, unaniwekea licha ya yule mgonjwa unampa mashaka pengine ujauzito na mimba unaniongezea tena dhiki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaiomba wizara hili ilione na wale watakaopelekewa kesi hizi tunaomba wasitufichie kesi zetu kwa pesa ndogo ndogo zinazotokea. Mwenyezi Mungu awajaalie washinde Maswahaba wote wawakanyagie wawashindilie watu hawa wanaotufanyia visa kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia ripoti hii ya utekeleza wa maagizo na maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia machache tu katika yale ambayo yamejitokeza ili kumsaidia Mhe. Waziri wangu kabla hajamaliza yote ambayo yamezungumzwa. Mimi nataka nigusie suala ambalo limechangiwa na wachangiaji wengi ambalo alilianza mchangiaji wa kwanza Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wachangiaji wengine ambao walichangia, ni kuhusu suala zima la kodi inayotoleshwa ya usafiri wa bandari.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo alizungumza Mhe. Ismail Jussa, kuwa mpaka hivi sasa pesa ambayo tumeipata Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni shilingi 700 bilioni katika shilingi 200 bilioni ambazo ziliidhinishwa. Samahani Mhe. Mwenyekiti, Baraza liliidhinisha shilingi bilioni mbili kutoka kwenye Mfuko wa Bandari kwa ajili ya kutatua matatizo ya madawati.

Hata hivyo, wizara mpaka hivi sasa pesa ilizopata ni shilingi 700 milioni kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Suala hili linatokana na Wizara ya Fedha kutokuingiza fedha ambazo zinakusanywa na wizara yangu inapewa asilimia 50 tu ya makusanyo hayo ambayo yanakusanywa.

Mhe. Mwenyekiti, iwapo utaratibu huu unaoendelea wa wizara kupewa asilimia 50 ya makusanyo ambayo yanakusanywa, utaendelea na hatorekebishwa basi wizara haitoweza kufikia lengo lake ambalo lilikusidiwa na Baraza la Wawakilishi ambalo lilipitisha hapa kama wizara ipate bilioni mbili kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo alilizungumza Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Mussa Ali Hassan, ni kuhusu uharibifu ambao umetokea katika Skuli zetu za *World Bank,* ni kweli kuna tatizo la mapaa kuwa yanavuja kwa baadhi ya skuli hizi mpya, tatizo ambalo limetokea ni tatizo la kiufundi yule *designer* ambaye ali-*design* mapaa haya na bahati mbaya sana wizara haikungundua tatizo hili mpaka mbapo muda ule ambao tunaekeana na Mkandarasi ulikuwa tayari umepita, baada ya kunyesha mvua kubwa ndio tukaona kama zile skuli zetu zinavuja.

Mpaka hivi sasa wizara imefanya tathmini ya mapaa ya skuli ambayo yanavuja na kiasi cha fedha ambazo kinahitajika kwa matengenezo ya mapaa hayo, lakini vile vile wizara itafuata

ushauri ambao waliozungumza Waheshimiwa wa kufikiria kazi hizi za majenzi kuwatumia makandarasi wetu wa ndani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme limetokea kwa sababu kwanza wizara huu mradi ulikuwa ni mradi wa kwanza ambao ulikuwa ni mkubwa katika Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, tukaona zile tenda tuzikagawe kwa makampuni mbali mbali ambayo yaliomba. Lakini nataka nikiri kama ni funzo na tutakuwa na tahadhari kubwa wakati tunapotoa tenda hizi ili kuona ni nani hasa anapaswa na zaidi tutazingatia wazalendo ambao kwa kweli wapo na wana viwango vizuri ambavyo wameonesha katika skuli hizi walizofanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia, lilijitokeza suala ambalo Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Mwanajuma Mdachi, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Mohameda Haji na Mhe. Makame Mshimba, walilizungumza kwa nguvu zao zote kuhusu suala la walimu wetu wale 159 ambao mpaka sasa hizi hawajalipwa pesa zao za mshahara ambazo walitakiwa walipwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili juzi nililijibu katika suala ambalo liliulizwa hapa Barazani na mpaka hivi sasa hatuna majibu ya nyongeza zaidi ya kusema kama tunaomba na nyie Baraza mtusaidie kwa sababu wizara iliandikia Utumishi na Utumishi waliidhinisha kwa barua kupeleka kwa katibu Mkuu kwa Wizara ya Fedha na wizara pia mara tatu tumewakumbusha wenzetu wa fedha, lakini mpaka hivi sasa hakuna jawabu ambayo tumeipata.

Kwa hivyo, hili suala niseme kama letu kama wizara kwa sababu tuna haki ya kuwasimamia walimu wetu kuhakikisha kama hizi pesa zinapatikana. Lakini niseme kama haliko kiutendaji tena katika mikono yetu tunazidi kuwasiliana na wezetu wa Wizara ya Fedha ili tuone ni namna gani ambavyo watalichukulia hatua na walimu hawa ambao wamesubiri kwa kipindi kirefu wanapata haki yao kama ambavyo inawastahili kupata.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo lilichangiwa na Wawakilishi wengi ambao walichangia wizara yetu ni suala zima la uingizaji wa fedha katika Bodi ya Mikopo. Tatizo hili ni kweli lipo na linasababisha na mambo makuu mawili:

(1)Ni kucheleweshwa kuingizwa kwa fedha za bajeti kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, tunakumbuka hapa kama tulipitisha bajeti ya bilioni 9.3. Lakini mpaka sasa hivi pesa ambayo tumepata ni bilioni 3.4 na pesa zilizopatikana tumelipa ada ya mwaka mzima na posho kwa wanafunzi 206 ambao wako nje ya nchi na ni sawa na milioni mia tisa na tisini na tatu.

Kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa, hapa kama wanafunzo walioko nje kama iwapo tunachelewa kuwalipia vyuo na kuwapa posho wanapata dhiki kubwa ya maisha katika vyuo au nchi ambazo wanasoma. Ni kweli na Bodi iliona hili, kwa hivyo, ikaona hizi pesa kidogo ambazo tumezaipata basi kipaumbele kwanza tuwafikirie hawa wanafunzi 206 ambao wako vyuo vya nje.

Fedha ambazo zimesalia ni bilioni 2.4 zimetumika ada na posho ya wanafunzi wa Vyuo vya Tanzania ikiwa pamoja na Vyuo vitatu vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, bado tuna deni kubwa hususan katika vyuo vyetu vya Zanzibar na tumejaribu kwa kidogo ambacho tunacho kupunguza angalau posho kidogo kwa wanafunzi ambao wako Bara na wale ambao tunao Zanzibar. Lakini pia lilijitokeza suala la vipi madeni ya nyuma ambayo tuliyoyakopesha.

Mhe. Mwenyekiti, tumeanza kufuatilia urejeshaji wa madeni kuanzia mwaka 2013 na mpaka hivi sasa karibu bilioni 25 tumeanza kuzikusanya na katika pesa hizo ni sawa na 5% tu bado asilimia ni ndogo, lakini bodi ilipitisha matumizi ya milioni mia saba na hamsini kwa ajili ya kusaidia haya madeni ambayo tunayo katika vyuo vyetu. Juhudi zaidi zinachukuliwa kwa bodi kufuatilia fedha hizi za Serikali ambazo zina haki ya kurudishwa katika mfuko wa bodi ili zisaidie watoto wetu wengine waweze kusoma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kuwaomba Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu Wawakilishi waliochukuwa mikopo hii ni watoto wetu ndugu zetu ni wapiga kura wetu tunao majimboni mwetu, watusaidie uhamasishaji ili pesa zile zirudishwe na baadae ziweze kusaidia kwa wanafunzi wetu wengine ili yale madeni ambayo tunayo tuweze kuyalipa na wanafunzi wetu wapate utulivu mzuri wa kusoma.

Mhe. Mwenyeti, nakushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Kaimu Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumuwakilisha Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, kutoa majibu ya hoja zilizojitokeza kutokana na michango ya Wajumbe katika kuchangia maelezo ya utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii yaliyotolewa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhia naomba kuwashukuru na kuwatambua Waheshimiwa wote waliochangia kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Pia, napenda kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru wale wote waliotupongeza kwa kazi nzuri ilifanywa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto. Tunapenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba maoni na ushauri ulitolewa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni muhimu sana kwetu na tunaichukuwa na tutaifanyia kazi ili kuleta ufanisi wa utendaji kwa manufaa ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Daima tutaendelea kushirikiana na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambazo zinatusaidia sana katika kuhakikisha kazi zetu zinakwenda vizuri kama vile zilizpangwa kwa manufaa na faida kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa nitoe ufafanuzi juu ya hoja za Wajumbe zilizojitokeza kuhusana na utekelezaji wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto za kutokuwepo kwa *DNA machine* hapa Zanzibar ni kweli suala la upatikani ya kipimo cha *DNA machine* nilikuwa changamoto kubwa na linaathiri sana katika shughuli zetu za kupambana na udhalilishaji za Wanawake na Watoto hasa katika suala la kupata ushahidi ambao unahitajika kumtia mtu hatiani kwa yule anaetenda makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa Wanawake na Wanawake ambao umeonesha kukithiri hapa Zanzibar.

Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba Serikali haijapuuza suala hilo...

**Mhe. Mwenyekiti:** Haya kuhusu utaratibu.

**UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Tunahitaji sana hii taarifa ya Kamati ya Utekelezaji hii ya Wanawake na Watoto na kwa kuwa na sauti ya Mhe. Waziri imekuwa ndogo kiasi ambacho tunapata shida sana huku katika mabenchi ya nyuma, tunaomba sana Mhe. Mwenyekiti, umuombe kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu umuombe Mhe. Waziri aongeze kidogo kusudi na sisi wakaazi wa mabechi ya nyuma tuweze kusikia na kufahamu. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa Mjumbe Mhe. Waziri amekusikia na atalirekebisha hilo. Mhe. Waziri tuendelee.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala la upatikanaji wa kipimo cha *DNA machine* hapa Zanzibar limekuwa na changamoto kubwa na linaathiri sana katika shughuli zetu za kupambana na udhalilishaji wa wanawake na watoto hasa katika suala la kupata ushahidi ambao unahitajika kumtia mtu hatiani na yule anaetenda makosa ya ubakaji na udhalilishaji wa Wanawake na Watoto ambao umeonyesha kukithiri hapa Zanzibar.

Nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba Serikali haijalipuuza suala hilo na ina mkakati madhubuti wa kulitafutia ufumbuzi suala hilo la kuwepo kwa *DNA machine* Zanzibar. Matumaini yetu baada ya kukamilika kwa mazungumzo na wenzetu tunaoshirikiana katika mapambano haya ya udhalilishaji suala la *DNA machine* litapatiwa ufumbuzi unaofaa.

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusu kesi za udhalilishaji. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Kamati ya Mawaziri inayoshughulikia masuala ya udhalilishaji wa Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Vyombo vya Sheria ikiwemo Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahakama imeanza mkakati ya pamoja na kuishughulikia kesi za udhalilishaji ziende na kutolea hukumu stahiki kwa wale waliotenda vitendo vya ubakaji na udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

Tunachokiomba kwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kushirikiana na wizara katika kampeni kubwa iliyoanzishwa ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji. Tunaomba wananchi washiriki

kikamilifu na kutoa ushahidi katika vitendo vyote vya udhalilishaji vinavyofanywa katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Suala la kuzika maiti zisizo na mwenyewe. Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto inaomba kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tutaendelea kulishughulikia suala hili kwa kuwa ni jukumu letu.

Mhe. Mwenyekiti, Suala la Afisi ya Idara ya Ushirika na Idara ya Mikopo. Ningependa kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, Afisi za Idara nilizozitaja hapo juu Serikali imezita kipaumbele cha hali ya juu kutokana na umuhimu wake wa utoaji wa huduma kwa wananchi. Idara ya Vyama vya Ushirika tayari Serikali imetupatia jengo liliopo eneo la Mazizini Mjini Unguja ambalo tayari limeshafanyiwa ukarabati mkubwa wa kisasa na lipo katika hatua za mwisho za matengenezo hayo. Matumaini yetu mjenzi wa jengo hilo atatuakabidhi jengo hilo hivi karibuni katika mwaka huu wa fedha.

Kuhusu jengo la Idara ya Mikopo kama nilivyosema katika taarifa ya utekelezaji ni kwamba ni kwamba upo katika mpango wa ujenzi wa Afisi kuu ya Mwanakwerekwe ambapo ukikamilika idara hiyo itahamishiwa katika idara hiyo itahamishiwa katika jengo hilo la Mwanakwerekwe.

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusu suala la Mikopo. Utekelezaji wa suala la mikopo katika Baraza lako tukufu umejitokeza baadhi ya Wajumbe waliousifu utekelezaji wake na wapo wengine waliooneshа suala hili kuwa halitambulikani na kazi inayofanywa ni kwa upendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nieeleze kidogo niwaeleweshe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wote waelewe kuhusu mikopo ya Mfuko wa Uwezeshaji Zanzibar na taratibu zake.

Kwanza kutambulikana Mfuko unatambulikana na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwani waliakuwa katika uchangiaji na wengi walishiriki katika uzinduzi wake. Mfuko umetoa mikopo katika Shehia 305 kati ya Shehia 339 za Unguja na Pemba zilizopo na masheha wamepatiwa muongozo wa mikopo.

Waheshimiwa, Wakuu wa Mikoa wote watano wamepatiwa orodha ya wananchi wote waliopatiwa mikopo shughuli zilizoombewa mikopo na idadi ya fedhaa wazilizopatiwa. Wakuu wa Wilaya wote 10 wamepatiwa orodha ya wananchi wote katika Wilaya zao waliopatiwa mikopo. Aidha, Wakuu wa Wilaya wameopatiwa nakala za Muongozo wa utoaji wa mikopo.

Utoaji wa Mikopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ni Mkoa wa pili ya Mikoa mitano iliyopatiwa fedha nyingi ukiongozwa na Mkoa wa Mjini Magharibi, kati ya shilingi milioni mia saba arubaini na nane laki nane na hamsini zilizotolewa kuanzia Julai 2014 hadi Machi 2015, milioni mia moja na thamanini na tisa zilitolewa Mkoa wa Kazini Unguja.

Aidha, Mkoa wa Kaskazini Unguja unazo shilingi milioni mia moja za JK na AK kati ya hizo shilingi arubaini milioni ziko Jimbo la Kitope katika kijiji cha Kinduni. Vile vile, Jimbo la

Kitope kupitia Shehia ya Mahonda ina wateja 43 wenye mikopo wa uwezeshaji wenye thamani ya shilingi milioni thalathini na mbili.

Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na unafanya shughuli zake kama kawaida tena kwa uwazi, masheha wote wa mikoa yote wanaujua na Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge wanaujua pia. Kwani muongozo unatutaka tushirikiane na watu hao na tumekuwa tukifanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa mara nyengine kwa kunipa fursa hii ya kumuakilisha Waziri. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa tunamwita Waziri wa Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru *Allah* kwa kutujaalia uhai na uzima na *toufiq* ya kukutana hapa.

La pili, naomba nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuja kutoa majumuisho madogo kuhusiana na michango mbali mbali iliyotolewa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuhusiana na ripoti ya Kamati na shughuli za Baraza kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tumepata Wajumbe kumi na tatu, karibu wote waliochangia waliweza kuchangia kwa njia moja au nyengine kwa Wizara ya Afya. Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali
3. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Salma Mussa Bilal
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Ashura Sharif Ali
8. Mhe. Hassan Hamad Omar
9. Mhe. Mohamed Haji Khalid
10. Mhe. Kazija Khamis Kona
11. Mhe. Abdi Mosi Kombo
12. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
13. Mhe. Raya Suleiman Hamad

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumze kwa uchache sana kuhusiana na mada kubwa iliyozungumzwa kwanza na wengi au karibu wote ni kuhusiana na Hospitali ya Mnazi Mmoja.
Mhe. Mwenyekiti, kwa Zanzibar Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kongwe lakini ndiyo hospitali kubwa yao inayokwenda katika hali ya rufaa kwa hapa Unguja na Pemba. Sasa hospitali hii ukongwe wake na majengo yake lazima yaendane sambamba na miundombinu ambayo inayowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali hii ni sawa na lile tangazo la dawa. Kuna baadhi ya matangazo ya dawa katika redio utaambiwa ukiumwa na kichwa tumia *panadol*, ukiumwa na kifua dawa fulani, lakini maradhi yakizidi au maumivu yakizidi muone daktari. Sasa hospitali hii ni kuwa tangazo lake ni kwamba mambo yakizidi nenda Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, ni hospitali inayopokea wagonjwa wote wa Unguja na Pemba. Hospitali kwa sababu ni ya Serikali haina njia ya kukataa mgonjwa yeyote atakayekwenda; akenda asubuhi, jioni au usiku. Sasa kuna wakati inazidiwa na kutokana na ukubwa wa hospitali na hali ya wagonjwa wanaopokewa. Kwa hivyo, baadhi ya huduma zinakosekana katika baadhi kipindi kutokana na uzito wa yale mambo ambayo yaliopo.

Na kama tunavyojua sasa hivi wengi tunakubali kwamba ama sisi binadamu tumebadilika tunakuwa na maradhi mengi au mambo ambayo tunayokwenda nayo yamekuwa ni mengi zaidi.

Kwa hivyo, hospitali haiwezi ikamkataa mtu. Sisi zamani tulikuwa tukisema mava ni sehemu ambayo hairudi mtu. Kwa hivyo, baadhi ya watu wanasema mtu kapelekwa mavani, maana hakuna mava hata moja iliyopelekwa ukisema maiti hakuna nafasi atazikwa na mwenzake, lakini harudishwi maiti kwamba mava imejaa. Sasa na Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hivyo hivyo.

Kwa hivyo, Wajumbe wengi wamechangia huduma kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini tujue kwamba ni sehemu ambayo mgonjwa yeyote atakapotoka atapelekwa Mnazi Mmoja. Kama munajua Waheshimiwa pengine mumepeleka wagonjwa wenu akizidiwa Hospitali ya *Al-Rahma* ni hospitali ya binafsi, anapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Sasa lazima hii itakuwa na changamoto nyingi.

Lakini suala la pili ambalo bahati nzuri mimi nawashukuru sana Wajumbe watatu wako; Mhe. Mohamed Haji Khalid, Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Abdalla Mohamed Ali. Hawa waliunga mkono kwamba tusitegemee huduma nzuri za kuendelea ikiwa kile kinachotolewa ni kidogo. Lakini huduma zipo na kila kitu kipo.
Kuhusu suala la hospitali wenyewe ambalo lilisemwa ndiyo kongwe kabisa. Imefanyiwa matengenezo ya mwisho makubwa mwaka 1996 na Serikali ya Abu Dhabi. Sasa kila kitu kilichopo pale kiliekwa wakati huo. Ziada inayokuja ni ziada ya misaada tu. La kwanza hilo.

La pili, kumetokezea utanuaji wa hospitali. Jengo lililofunguliwa karibuni. Utanuzi wa Hospitali ya Macho, utanuzi Hospitali ya Viungo na majengo mengine yalifanywa hivi karibuni likiwemo la *ENT* ambalo zamani lilikuwa ni kitengo kidogo, sasa ni karibu *unit* kubwa yenye jengo lake na kila kitu chake, huu upasuaji wa nini, matatizo ya masikio, koo na pua. Kwa hivyo, ile hospitali yenyewe inakua na huduma zake zinatarajiwa zikuwe vile vile. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti inakuwa lazima hamuwezi kwenda sambamba.

Kwa hivyo, tunakubali sisi kwamba baadhi ya sehemu hali hairidhishi wala hakuna mtu atakayesema kwamba vitanda vilivyopo vinamridhisha, haviridhishi. Lakini je, hali ya uchumi ilivyo, bora mgonjwa kupokewa au ikawa hapana kitanda.

Suala lililozungumzwa jengine ambalo hili tunalichukua na tunalifanyia kazi ni kuhusu suala la lugha za wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, hili tunalichukua na

tunakwenda nalo ni suala ambalo hakuna linalompendezesha mtu yeyote anayekwenda kutafuta huduma pahali, anataraji apewe lugha nzuri na lugha inayoridhisha. Hivyo, hili tunalichukua.

Kuhusu hiyo hiyo Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhusu *mortuary*. Kweli *mortuary* ni ndogo ina uwezo wa kuchukua maiti nne tu, lakini bado inafanya kazi na upo utaratibu wa kujengwa jengo zaidi linalohusu hilo *mortuary*. Kwa ujumla hivi sasa kuna mpango ambao ushafanyiwa *Feasibility Studies* ya matengenezo ya Hospitali yote ya Mnazi Mmoja kwa kupitia Benki ya Kiislamu ya *BADEA*. Kwa hivyo, mpango humo upo katika *pipe line* na *Inshaallah* ukifanikiwa hali itabadilika.

Lakini la mwisho kabla sijaondoka kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja, juzi hapa nilipokuwa nikijibu swali nilisema kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kwamba ni ya rufaa, lakini ardhi iliopo pale ni ndogo kiasi cha kwamba hairuhusu kufanya maongezeko ya baadhi ya majengo na huduma nyengine. Ndiyo maana Serikali wenyewe imetenga eneo la Binguni kwa ajili ya kujenga hospitali nyengine ya rufaa ambayo itakuwa ni ya kisasa na majengo yatakayoridhisha kwa kila mmoja.

Lakini bado tuna wajibu wa kuishughulikia ile tuliyonayo, haina maana kwamba huko tutajenga lakini ile tuliyonayo tutaiacha yaani tuna wajibu wa kuishughulikia tuliyonayo na kila siku tunaongeza juhudi katika kuona hali ilivyo.

Ilinganishwa hapa na kesi iliyotokea juzi ya makaro. Kama ilivyosemwa kwamba makaro yale yalifumka siku ya Jumamosi lakini Jumapili tayari yameshafanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, lile ni jambo ambalo bahati mbaya tu kwamba wale waliokuwepo na kamera zao wakaliona lakini lilichukua *only twenty four hours* kurekebishwa, tena kwa sababu ilikuwa ni *weekend,* haikuchukua muda wote. Kwa hivyo, lile ni jambo la kawaida ambalo linaweza likatokezea popote.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ununuzi wa mashine ya *DNA*. Waheshimiwa, Serikali hasa kama kuna Wizara ya Afya, Wizara ya Habari na kuna Wizara nyengine zinaendeshwa kwa pamoja. Sasa hichi chombo pahali pake siyo lazima kiwe hospitali tu, kinaweza kuwa pahali pengine kwa sababu hichi chombo duniani si zaidi ya kutumika kwamba hospitali ni chombo ambacho kinaweza kutumika kwa kuchunguza kesi za kiharamia, kesi ambazo ni *criminal,* yaani zinaitwa za mauwaji, za nini. Kwa hivyo, hichi chombo kinaweza kikatumika kwa matumizi mengi sana kumjua aliye mhalifu, kumjua nani.

Sasa kutokana na hali tunayokwenda nayo na bajeti finyu ndiyo maana wizara tatu sasa zinashirikiana kutafuta chombo hichi. Na mpango huo tayari umeshandikwa kila kitu, Wizara ya Katiba na Sheria chini ya *DPP,* Wizara ya Wanawake na Watoto kutokana na kesi za watoto na Wizara ya Afya kutokana na utaalamu.

Chombo hichi kikishakupatikana tayari mazungumzo yashafanyika na pahali pameshatafutwa kuweka Mkemia Mkuu ambapo utaalamu upo. Kwa sababu huwezi kuleta chombo ukawa hakuna utaalamu. Sasa hiyo mashine ambayo ilizungumzwa hapa kwamba ilikwenda kule hospitali ni chombo cha mwanzo cha kufanya kazi ya kuondoa hiyo *DNA machine* katika

kiwiliwili cha binadamu ili kikafanyiwe uchunguzi, nacho hakifanyi kazi. Bahati kwamba katika Wizara ya Afya kuna kitabu kinachoeleza muongozo wa kutoa misaada.

Kwa hivyo, mtu yeyote anayeleta msaada wake hasa wa vifaa hauwezi kupokelewa mpaka uweze kutosheleza mahitaji ya kile miongozo iliyoekwa mule, kwamba kwanza kiwe na wataalamu wa hapa, kiwe kinaweza kutumika, kiwe hakina athari kwa jamii ya hapa. Kwa hivyo, hicho sicho chombo cha *DNA*, ni chombo cha kutoa hiyo *sample* ya nini ikapatikana hiyo *DNA*.

Hivyo, Wizara imeridhika na mpango huo, kwa sababu Wizara itakuwa inakitumia, Polisi watakuwa wanakitumia, Ofisi ya *DPP* watakuwa wanakitumia na yeyote ambaye katika Serikali ambaye ana shida na kupata *DNA* atakuwa anakitumia hicho chombo. Sasa siyo lazima kinunuliwe na Wizara ya Afya, ni chombo ambacho kinahitajika kwa nchi nzima hapa Zanzibar, kwa ajili ya uchunguzi wa kesi za uhalifu.

Sasa ikiwa bajeti ni ndogo, halafu sisi tukanunue chombo hicho au Wizara ya Afya ikanunue chombo hicho, wagonjwa wote wasitibiwe kwa sababu ya kununua chombo hicho, hiyo *risk* hiyo haiwezi kuchukuliwa na Wizara ya Afya. Wizara ya Afya itakwenda kutokana na ile bajeti ambayo imepangiwa. Sasa ilipoonekana kwamba kuna utaratibu ambao unawezekana kukinunua hicho chombo bila ya ku-*involve* bajeti ya Wizara ya Afya, Wizara ya Afya inashirikiana kikamilifu na vyombo hivyo vyengine kuona kwamba chombo hicho kinanunuliwa na kitatumiwa kwa ipasavyo chini ya utaratibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali. Mkemia Mkuu ambaye yeye yupo chini ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali mbili ya Mwembeladu na ya Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu zote ni sehemu ya hospitali ya Mnazi Mmoja kwa mujibu wa utaratibu wa Wizara ya Afya. Kwa hivyo, huduma zote ambazo zinakosekana kule tatizo ni lile moja ambalo tunasema na Wizara inajua hali ilivyo katika Hospitali ya Kidongo Chekundu na *phase* ya mwanzo alipatikana mfadhili akajenga jengo ambalo mpaka sasa limeshaanza kutumika kwa ajili ya kuendesha ile hospitali, kwa ajili ya kuweka madawa na utoaji wa huduma za mtu anayekwenda na kurudi, siyo wale waliolazwa. Tatizo zaidi lipo kwenye wale waliolazwa na huduma zao. Kwa hivyo, kutokana na hali ilivyo bado mazungumzo yanaendelea kupata ufadhili wa kuweza kujenga ile wodi. Hakuna anayeridhika na hali ile.

Mhe. Mwenyekiti, ndiyo maana tukasema kwamba juzi mimi katika kujibu swali kwamba *WHO, minimum per capital health expenditure* ya mtu ni *sixty dollars*. Hiyo ni *minimum* kwa ajili ya kuweka ile nini yenyewe. Lakini sisi tunapata *twenty nine dollars* ambayo ni *less than fifty percent, what are you expecting* katika hali hiyo? Kwa hivyo, cha kufanya zaidi ni kunyanyua bajeti ya Wizara ya Afya na kuweka vipa umbele vilivyotakiwa.

Suala la Kitengo cha *HIV* katika Hospitali ya Mwembeladu. Jibu lake ni kwamba lile jengo siyo jengo jipya, ni jengo la zamani na haya maradhi yamekuja karibuni. Kwa hivyo, katika kuona kwamba ile huduma inatolewa ikatafutiwa nafasi, lakini Wizara inakubaliana na hoja ya Wawakilishi kwamba panatakiwa stara zaidi na inalifanyia kazi kikamilifu ili kwa siku za mbele, labda katika bajeti ijayo tuweze kupata pahali pengine ambapo patatoa stara zaidi kuliko pale. Lakini ile haja ilipotokezea ndiyo ikaona haina nafasi isipokuwa iwekwe pale katika nyuma ya jengo linalotoa huduma ya uzazi.

Liliulizwa vile vile au lilichangiwa kuhusu Hospitali ya Makunduchi. Hospitali ya Makunduchi kulikuwa na changamoto za wafanyakazi na hili ndilo tatizo ambalo tulilizungumzwa kwa ujumla, kwamba baadhi ya hospitali zilizopo Unguja na karibu zote za Pemba zina ukosefu mkubwa wa wafanyakazi katika ngazi ya ma-*nurses*, *clinical officers* na wengineo. Hilo tunalijua na ni mtihani mkubwa.

Kwa hivyo, mkazo mkubwa unatolewa sasa hivi kwa wale wafanyakazi wanaoajiriwa wapya kupelekwa katika maeneo ambayo tayari yana ukosefu ule ili kujaza zile nafasi. Hivyo, wale watakaopata ajira mpya sasa hivi, wataona kwamba wanaekewa *conditions* ya kwamba ajira ipo lakini ipo ya hospitali au mahali fulani ya kufanyia kazi, badala ya kuajiri kwa ujumla ujumla kwamba wewe umepewa ajira katika Wizara ya Afya, aah! utaajiriwa kwa mujibu wa maeneo ambayo yana ukosefu.

Kwa sababu kama hatukwenda hivyo itakuwa baadhi ya maeneo siku zote yana ukosefu mkubwa wa wafanyakazi na maeneo ya mjini ikiwa hii Hospitali ya Mnazi Mmoja utaiona kwamba ina wafanyakazi wengi na wengineo. Kwa hivyo, huo ndiyo mkakati ambao upo wa kuona kwamba baadhi ya sehemu zinapata wafanyakazi wa kutosha.

Upungufu wa nyumba za daktari. Kama tulivyosema kwamba Wizara ya Afya katika kuipunguzia mzigo Hospitli ya Mnazi Mmoja na katika kuona kwamba huduma za afya zinatolewa kikamilifu nje ya mjini, imeanza utaratibu wa kuzipandisha daraja. Nashukuru uongozi uliopita wa Mhe. Juma Duni na Mhe. Dk. Sira, kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kuona kwamba Hospitali ya Makunduchi na Hospitali ya Kivunge zimeanza kupelekwa daraja ya kuwa ni hospitali za wilaya na sasa imeanza Hospitali ya Micheweni kupandishwa daraja kuwa hospitali ya wilaya.

Sasa hii ikifika kiwango cha kukamilika itakuwa wagonjwa wengi sasa wanamaliza shughuli zao katika hospitali hizi badala ya ku-*stock* katika hospitali ya Mnazi Mmoja na hapo ndipo itakapokuwa hospitali ya rufaa kweli, kwa sababu mgonjwa anapotoka anatizamwa *address* yake. Je, kapitia hospitali iliyokaribu yake na kapewa cheti cha rufaa, halafu tena atashughulikiwa kikamilifu. Si hivyo, itabidi ahangaike kupita chochoro hii na hii. Lakini kwa sasa kwa sababu bado haijawa rasmi, wanapokelewa moja kwa moja kama hospitali nyengine.

Vile vile, Hospitali ya Micheweni ambayo imetengana na wenzake inapandishwa cheo kuwa hospitali ya rufaa, imeshaanza kufanyiwa utanuzi ili iende katika hospitali ya wilaya.

Hospitali ya Vitongoji kama ilivyoulizwa hapa bado hospitali ile kwa sababu mbili; Kwanza *record* yake haioneshi kwamba wagonjwa wengi wanakwenda katika hospitali ya Vitongoji. Lakini la pili, kuna hospitali ya Chake Chake ambayo iko karibu na hospitali ya Vitongoji ambapo wengi wanaelekea kule. Kwa hivyo, hospitali ya Vitongoji itasubiri kwanza kuona hali itakavyokwenda ya kibajeti katika miaka ijayo itaendelea kuwa hospitali ya *Cottage*.

Kuhusu huduma ya Hospitali ya Chake Chake kama ambavyo Mhe. Bi Raya, alivyosisitiza, hata mimi binafsi nimepata malalamiko hayo na tayari tumeshaanza kufanya utafiti wa kina kuhusu namna gani ya hospitali ya Chake Chake inavyolalamikiwa katika utoaji wa huduma. Kwa

hivyo, hili suala liko katika meza na *Inshaallah* baada ya muda tutajua ni kitu gani. Lakini moja katika tatizo kubwa ambalo kama nilivyolisema ni ukosefu wa wafanyakazi waliokuwa na ujuzi, yaani madaktari na wengineo ambao wanahitajika kuwepo.

Hoja ya uzio katika Hospitali ya Makunduchi nilisema ni ukosefu wa bajeti, *ambulance*. Ni bahati mbaya kwamba mwaka mmoja uliopita Hospitali ya Makunduchi ilipewa *ambulance* lakini ilipata *exident*, *beyond repair.* Kwa hivyo, mpaka sasa hivi kuna ukosefu huo, lakini bado jitihada zinafanywa ili kuweza kupata mbadala wa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoani inatoa huduma kwa sababu huduma zote zimehamishwa katika majengo makuu mawili; Moja ikiwemo *theatre* imehamishwa katika jengo la holi la umoja ni nguvu na nyengine imehamishiwa katika jengo la *ZSTC* Mkoani. Kwa hivyo, Hospitali ya Mkoani pamoja na kwamba inajengwa mpya, lakini huduma zake zipo mpaka zile huduma za *theatre* za operesheni zipo. Hivi karibuni tuliwapelekea mashine mpya ya kufanyia nusu kaputi, sijui ndio inaitwa nini.

Kwa hivyo, hospitali ya Mkoani inafanyakazi Mhe. Bi Raya, pamoja na kuwa inajengwa mpya, lakini ile iliyokuwepo inafanyakazi, ina madaktari na wanakwenda. *X-Ray* ilikuwa haijafanyakazi kwa sababu ya tatizo la umeme. Leo nimepata taarifa kwmaba tatizo lile la umeme limeshatatuliwa na kwa hivyo, kuanzia jana hivi imeanza kufanyakazi *X-Ray* kwa ajili ya wagonjwa wengine.

Kwa hivyo, bado tumo katika kushughulikia pamoja na kwamba hospitali inajengwa lakini *functions* zinakwenda kama kawaida. Hatuiwachi mkono kwa sababu ni hospitali ambayo iko pahali muhimu, kwa sababu pale mbali ya kuhudumia watu wa katika maeneo mbali mbali, lakini kuna vyombo vya usafiri vinafika pale na pengine mtu kaumwa ndani ya meli moja kwa moja au anafika pale anaumwa anapelekwa hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kwa ufupi Wizara ya Afya iko makini, inajua hizi kero zilizomo, lakini imekubwa na ukwasi wa fedha, uhaba wa wafanyakazi wa ngazi ya kati. Bahati nzuri sasa hivi tunao madaktari waliokuwa wataendelea wa kutosha, kwa sababu mwaka 2014 tulipata waliohitimu 38 kutoka chuo walichosomesha hawa madaktari wa Cuba na wengine wanapatikana kutoka nje.

Madhumuni makubwa ya Wizara ya Afya baada ya kuja hawa madaktari na kumaliza *internship* yao, ni kuwapeleka katika vyuo tofauti kufanya *specialization*, kwa sababu wataalamu wetu wanatuambia kwamba madaktari wazuri ni wale ambao tayari wameshapata *specialization*. Tuwe na madaktari wa maradhi ya kike, tuwe na madaktari wa moyo, tuwe na madaktari wa masikio na koo, tuwe na madaktari hawa wa mifupa ambao ni muhimu, kwa sababu *exidents* zimeongezeka na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kwa hayo machache na kwa heshima na taadhima naomba radhi sana kwa yote ambayo pengine kwa njia moja au nyengine nimelisahau, lakini nimejitahidi ili kuona kwamba Wizara ya Afya inajali sana mapendekezo ya Kamati na inayashughulikia kikamilifu. Kwa sababu yale mapendekezo ndio kazi yetu yenyewe, sasa tukiyashughulikia ndio tutakuwa tumo kazini.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nitowe majumuisho kwa waraka nilioutoa leo hivi asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru wachangiaji wote 13 waliochangia waraka wangu, wametoa maoni mazuri, michango mizuri na naahidi kwamba yale ya kutekelezwa nitayatekeleza na yale ya kawaida tutaendelea nayo kama kawaida yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu niwataje Waheshimiwa Wajumbe waliochangia hotuba yangu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Ashura Sharif Ali
6. Mhe. Hassan Hamad Omar
7. Mhe. Mussa Ali Hassan
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
10. Mhe. Kazija Khamis Kona
11. Mhe. Abdi Mosi Kombo
12. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
13. Mhe. Raya Suleiman Hamad

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru tena wajumbe hawa wote waliochangia hotuba yangu na sasa naomba kutoa majumuisho. Lakini pia namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wangu kwa mchango aliotoa na majumuisho aliyosaidia katika kuweka sawa mambo mengi na sasa hivi nitajitahidi kuchangia yale ambayo yeye ameniachia mimi na yale ambayo yeye kayachangia waliochangia wanisamehe sana sitoyachangia tena, ila kwa lile la muhimu ambalo bahati mbaya mwenyewe hayupo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ningependa kidogo kugusia mawili au matatu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa, alitaka nimuelezee kwa hakika takwimu za waliopata mikopo na sio Mhe. Ismail Jussa tu, wengi waliochangia katika suala hili waliuliza hilo. Kwa hivyo, nikimjibu Mhe. Ismail Jussa, naomba sana wajumbe wengine waliochangia suala hili na wao wawe nimeshawajibu.

Mhe. Mwenyekiti, toka mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2014/2015 takwimu zifuatazo ndizo tulizozikusanya za mikopo na waliomba mikopo. Idadi ya wanafunzi walioomba mikopo mwaka 2011/2012 ni 1,002. Mwaka 2012/2013 ni 3,400. Mwaka 2013/2014 ni 4,900 na mwaka huu tunaokwenda nao 2014/2015 tayari tumeshapokea maombi 5,005. Nilipokuwa nikichangia katika hotuba yangu nilisema kwamba kwa bahati nzuri wala sitaki kusema kwa bahati mbaya, kwa bahati nzuri idadi ya waombaji inaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, tulianza 2011/2012 tulianza na wanafunzi walioomba mikopo ni 1,002, wakati hivi sasa mwaka 2014/2015 wanafunzi walioomba mikopo ni 5,005 na jumla ya wanafunzi waliokopeshwa mwaka 2011/2012 ni 1,090 na mwaka 2012/2013 ni 2,027, mwaka 2013/2014 ni 2,828 na tunategemea kuwapa mikopo wanafunzi 3,822.

Jumla ya fedha tulizotumia. Mwaka 2011/2012 tumetenga shilingi bilioni 4 na tumekopesha shilingi bilioni 4. Mwaka 2012/2013 tumetenga shilingi bilioni 8,300,000,000 na tumekopesha bilioni 7, 700,000,000. Mwaka uliofuatia wa 2013/2014 tumetenga shilingi bilioni 9,100,000,000 na tumekopesha bilioni 6,300,000,000 na mwaka huu tunategemea kutenga bilioni 9,300,000,000 na tunaweza kukopesha bilioni 3, 400,000,000.

Hizi ni takwimu ambazo ningependa nizitowe hapa ili kuonesha kwamba idadi ya pesa tunazozitoa ni nyingi, idadi ya wananchi wanaotaka mikopo ni wengi na wanaongezeka kila mwaka na tunajitahidi sana sana kukopesha ili wananchi wetu wa Zanzibar waweze kupata elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwa Mhe. Saleh Nassor Juma, maswali yake ya wale walimu 159 yameshajibiwa. Ningependa nilijibu hili swali la kuwapatia walimu wa chuoni angalau posho la shingili 20,000, ili wapate motisha na waweze kusomesha.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kulijibu swali hili kama lilivyojibiwa kwamba utaratibu wa kiserikali hawendi namna hiyo kwamba walimu wa chuoni walipwe posho la kawaida la shilingi 20,000. Kama Waziri wa Elimu idhini, ningependa sana kufanya hivyo, ningependa sana kuwafanyia hivyo walimu wa vyuoni kwa msaada na jukumu kubwa walilonalo. Lakini Baraza hili litanihoji siku moja ulipata wapi idhini hiyo. Kwa hivyo, walimu wa chuoni tunawachangia kutoka kwenye mifuko yetu tunapoweza, tunawachangia kuhudumia maulidi yao tunapoweza, lakini kwa mfuko wa Serikali kidogo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba, maswali yako mengi yamejibiwa. Maswali yako kuhusu kilio chako cha ufinyu wa bajeti kimetokea wapi, bajeti finyu imetokea wapi na kadhalika limeshajibiwa. Lakini naomba kuongezea suala moja kwamba ulipendekeza mikopo hii. Kwanza Wawakilishi wajulishwe na wajuwe, lakini ipelekwe kwa Wawakilishi ili na wao majimbo yao wapate faida hizo katika kuhudumia majimbo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba, ningependa sana kufanya hivyo, kwa sababu na mimi ningepata sehemu yangu ya kupeleka katika Jimbo la Donge na Jimbo la Donge kuna wanafunzi wanaopasi kwenda Chuo Kikuu, kwa hivyo, tungeweza kufanya hivy,o basi mimi ningefurahia na nikapata kasma yangu tukafanya hivyo, lakini tulichokifanya hatutoi mikopo hii kwa kupitia majimbo hapana, tunatoa mikopo hii kwa masharti kwamba anayetaka kukopa amepata kuingia Chuo Kikuu ile *admission letter* anayo, yaani amepata la kwanza. Na kama amepata basi la pili maana yake amepasi ametimiza hizo *credits au distinctions* zinazotakiwa.

Kwa hiviyo, la tatu Mzanzibari huyu, kwa sababu sasa hivi tuna mikopo miwili tuna mikopo ya Mzanzibari tuna mikopo ya kutoka Tanzania Bara Wizara ya Elimu na Ufundi ya Jamhuri ya Muungano, tunajaribu kadiri iwezekanavyo wanaopata mikopo kwa Jamhuri ya Muungano hawawezi kupewa mikopo ya Zanzibar tunawatoa kabisa, kwa sababu haturuhusu mtu mmoja

achukue mikopo miwili kwa sababu itamuwiya vigumu baadae kuja kuilipa mikopo kwa pesa hizo mikopo miwili.

Kwa hivyo, hizo ni taratibu tunazozitumia ziko wazi kabisa, lakini hata hivyo tuko tayari kupokea wazo jengine lolote tufanye nini ili kuboresha utaratibu huu wa kutoa mikopo kwa walimu wetu, kama nilivyokwisha kutoa *figure* hapa bahati nzuri idadi ya tunaokopesha imeongezeka na fedha tunazozikopesha zinaongezeka.

Kwa hivyo, nahisi hatufanyi vibaya ingawa na idadi ya watu ambao hatuwezi kuwapa mikopo nayo inaongezeka kutokana na pesa chache tulizopewa za kuwakopesha.

Mhe. Ashura wa viti maalum ameuliza masuala mengi kidogo na mengine Mhe. Naibu Waziri, ameshayajibu na yeye pia alizungumza posho la shilingi elfu ishirini kwa walimu wa vyuo, limeshajibiwa hili na mimi nimeshaongezea kulijibu.

Mhe. Hassan Hamad Omar,  simuoni kwa bahati mbaya hayupo lakini ningependa anisikie kwamba ni kweli tumerikodi kwa makosa yule mwalimu tuliyempeleka Kojani wa Sayansi, tulizipata nafasi mbili za kuajiri walimu wa Sayansi kwa bahati mbaya yuole mmoja tuliyedhamiria kumpeleka Kojani hatukumpata na tukampata huyu mwengine ambaye anasomesha masomo ya *Arts*.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Hassan Hamad Omar, huyu ni Naibu Mwenyekiti wangu wa Kamati anistahamilie na anivumilie, nitahakikisha *intake* nyengine yoyote inayokuja kwa ajili ya walimu nitafanya kila jitihada kumpatia mwalimu kama si mmoja wawili kwenda kusomesha Kojani, namnasihi na namuomba akawape habari watu wa Kojani, tutakapompeleka mwalimu wa Kojani wasimkatae kwa sababu kule ni mbali kumejitenga sana, kwa hivyo, kama tulivyopeleka walimu Micheweni wakakataliwa wakaondoka wakarudi mjini basi huyo wa Kojani tutakapomleta jitahidini sana sana kumpokea.

Mhe. Mohammed Haji Khalid, madai yako ya madawati ni yale yale kama kawaida fedha tulizotiliwa ni chache mno nataka nilizungumze kidogo hili la madawati. Kutokana na kodi ya wanaosafiri tulikubaliana katika Serikali yetu  kwamba tuwatoze wananchi kodi hii tuwaongezee *tax* ya shilingi elfu moja angalau, fedha hizi zote zikikusanywa ziingie katika ujenzi wa madawati.

Kwenye bajeti ya mwaka jana ikakubalika na ikapitishwa hapa Barazani kwamba mfuko wa madawati kutokana na kodi utakuwa bilioni mbili, bilioni mbili, kwa bahati mbaya kabisa pesa hivi hazipatikani kwa wakati na tulipata mara moja mwaka jana karibu ya bajeti tukatiliwa nafikiri shilingi milioni saba mpaka hivi leo hatukuzipata pesa hizo hata shilingi moja.

Kwa hivyo, mchango wa madawati unapatikana kila siku kwa sababu kila siku watu wanasafiri lakini pesa hizi zinakwenda Wizara ya Fedha, kwa bahati mbaya tumeshazungumza na kuandika na kuongea, lakini bado sijakata tamaa tuna robo ya mwisho, nitahakikisha angalau pesa zaidi kidogo tunazipata ili kukamilisha hili lengo tulilopewa, vyenginevyo, haitawezekana kuwachongea madawati walimu wote wanaoingia katika maskuli.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Mohammed, amesikitika sana mpaka akaahidi kwamba tukifika kwenye bajeti mwaka huu atatubana sana sana kutokana na watu kutikupata pesa zao tokea Oktoba miaka miwili iliyopita. Sitaki nizungume sana kutokana na hili kwa sababu mimi nimeshalifikisha mwisho, nimeshalipitisha kwenye bajeti limepita, nimeliomba katika Tume ya Utumishi, Tume ya Utumishi imeiandikia Wizara ya Fedha kwamba hawa wanastahiki walipwe pesa zao hata kama walikawia kutoa taarifa za vyeti vyao, lakini sasa taarifa zimekamilika, ombi la Wizara ya Elimu tumeshalipata na sisi tunathibitisha kwamba watu hawa sasa walipwe pesa zao.

Mhe. Abdalla Mohammed nakumba na nakunasihi sana tushirikiane mimi na wewe kuzidi kuwahimiza wenzetu watutilie hizi fedha, lakini tusifike pahala Mheshimiwa mzee wangu ukawa mgumu kunipitishia bajeti yangu, ukikataa kunipitishia bajeti yangu maana yake umekataa nisiwasomeshe wanafunzi wazaliwa wananchi wetu. Kwa hivyo, nafikiri kwa namna ninavyokujua na utu uzima wako hutokuwa mkaidi kiasi hicho.

Lakini nataka nikuhakikishie mimi bado sijakata tamaa, walimu hawa watapata fedha zao kabla ya kumalizika bajeti hii na mimi mwenyewe nitakuwa sasa kiguu njiani kwenda kuzidai pesa zao walimu hao, maana kama kuna watu tunawaonea machungu, najua wapo walimu wengi sana, mimi ni mmoja, mwalimu anafanya kazi kubwa sana yenye thamani kubwa sana ya kutusomeshea watoto wetu. Leo mwalimu anadai posho lake, anadai mshahara wake mwaka nenda mwaka rudi hajazipata mpaka leo, nakuomba sana tustahamiliane na *Inshaalla* tutafanikiwa.

Mhe. Kazija Khamis Kona na wewe hili la walimu ulilizungumza na Mhe. Naibu Waziri, ameshalitolea ufafanuzi, umezungumza kuhusu skuli za msingi kwamba hazina vitabu vya kusomea na wao karibu watafanya mitihani, nataka nikuhakikishie kutoka *STD* 1 mpaka *STD* 4 walimu wa msingi wana vitabu vya kutosha na bado havijamalizika kule ghalani kwetu vingaliko na wanavyo vya kutosha, walimu wa *STD* 5 mpaka *STD* 6 tuko mbioni kuwamalizia, kuwachapishia vitabu vyao na kuwanunulia vitabu vyao. Nataka nikuhakikishie bajeti hii haitamalizika na wao watapata vitabu vyao kila mwanafunzi kitabu chake mwenyewe.

Mhe. Abdi Mosi Kombo, umezungumza kama walivyozungumza wengine kwamba elimu mbadala hakuna walimu wa kutosha ni kweli, tuko mbioni kunatafuta walimu wengine. Nakuoneni mnapiga kofi kwa sababu nasema tuko mbioni, hizi mbio za kweli kweli hizi, hizi mbio za kupiga hatua kweli kweli na nina hakika tumeshapeleka barua utumishi Serikalini kuomba ajira ya walimu, tunao walimu wengi sana ambao hawajaajiriwa na wameshahitimu, lakini sisi si waajiri lazima tupeleke utumishi.

Utumishi hawezi kukupa ruhusa ya kuajiri kama hatuna mshahara wa kuwalipa, kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu pesa zao zipo, hawa walimu tunatarajia kuwaajiri, barua tumeshaandika na barua tumeshakumbusha na hivi karibuni tukishamaliza shughuli hizi tu bajeti, nimeagana na Kamishna wa ruhusa ya kuajiri nitakutana nae na tutaipitia tena kwa mara ya mwisho *lists* zote niliyompa ya wananchi walimu waliomaliza kusoma, kusomeshwa, kusoma kupasi, tuna walimu wenye *Certificates*, tuna walimu wenye Diploma, tuna walimu mpaka wenye *Degree*.

Kwa bahati nzuri hatuna walimu wenye *Degrees* za Sayansi ambao hawajaajiriwa kama hao Wawakilishi wenzangu mnao mnawajua katika Majimbo yenu jamani tuleteeni kwa haraka sana, mwalimu yoyote mwenye *Degree* ya Sayansi mleteni kwa haraka sana, walimu wengine tutafuata utaratibu huu, lakini nitafanya mkutano makusudi na Tume ya Utumishi Serikali hivi karibuni tukishamaliza shughuli hizi za Baraza ili tuweze...sio kulimaliza lakini angalau kulipunguza sana hili suala la kutoajiri hizi ndio mbio ambazo nasema nakwenda.

Mhe. Abdi Mosi Kombo, umenivunja nguvu kidogo uliponitajia suala la Pwani Mchangani, kwani suala hili si tumeshalizungumza mimi na wewe, suala hili mimi na wewe tushalizungumza tena juzi kishindo cha jana na tukakubaliana kama ni kulizungumza Barazani hapa ili tupate umaarufu na wananchi wetu watujue kwamba tunagombania basi hilo ni zuri ni sawa nakubaliana na wewe. Lakini hili tumeshalizungumza na nitalitekeleza kama tulivyolizungumza.

Mchangiaji wa mwisho Mhe. Raya Suleiman Hamad, umetushauri na umetuomba tuzungumze na walimu wetu ili wale watu wenye ulemavu wazungumze nao pole pole wasiwakaripie sana, wasiwakaripie kabisa, lakini wazungumze nao pole pole kiungwana ili hawa wenye ulemavu tusije tukawapa shutuma mbili kwa pamoja, shutuma moja ana ulemavu masikini ya mungu lakini la pili anajuta kwa nini kaja pale skuli kwa sababu ya maneno machafu anayopewa.

Nitasema nao sana sana walimu wetu hawa na tukimbaini mwalimu ambaye anafanya hivyo moja kwa moja tumuondoshe, moja kwa moja tutamuondosha na tutaweka mwelimu mwengine. Kwa bahati nzuri nimepata Mkurugenzi mpya yule mama aliyekuwepo pale ameshastaafu, nimepata Mkurugenzi mpya kijana, yuko tayari kufanya kazi kwa nguvu zake zote, kwa hivyo, *Inshaalla* hili tutalitekeleza.

Umezungumza na umezungumza mapema siku mbali mbali katika Baraza hili kwamba tujaribu watu walemavu tuwatengenezee viti vyao maalum, kwa sababu viti vya kawaida hawawezi kuvitumia kuingia na kukaa, nimelipokea kumbusho hilo na nimelipokea kwa mikono miwili, tutafanya kazi hiyo kadiri iwezekanavyo ili tuweze kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nakushukuru sana kwa kunivumilia na kunipa ruhusa nichangie nitoe ufafanuzi wa hoja zilizozungumzwa na Wawakilishi hapa, nimejitahidi kama niwezavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kama mimi na Naibu Waziri wangu tumelikosea au tumesahau hoja yoyote iliyotolewa hapa hatukuijibu, tunaomba radhi, lakini tujaribu kama tuwezavyo kuyasawazisha yote yaliyozungumzwa hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Mwenyekiti na mimi awali ya yote kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto nachukuwa nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuajalia jioni hii kuwepo hapa katika kuendeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Lakini pia, nachukuwa nafasi hii ya kukushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa majumuisho juu ya yaliyochangiwa na Wajumbe mbali mbali juu ya hoja yetu iliyokuwepo mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nianze maneno yangu ya majumuisho kwa ku-*qourt* maneno ya Mtume (*SAW*). Mtume (*SAW*) anasema kwamba; "*Qulukum Rag'hiyn wa Qulukun Masuulun Gh'anraiyyatih"* kwamba nyote ni wachunga na nyote mtaulizwa juu mliowachunga.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba niwatambue wale wote waliochangia ripoti yetu.

| | | |
|---|---|---|
| (1) | Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | - Mwakilishi wa Jimbo la Kitope |
| (2) | Mhe.Mohammedraza Hassanali | - Jimbo la Uzini |
| (3) | Mhe. Ismail Jussa Ladhu | - Jimbo la Mji Mkongwe |
| (4) | Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | - Viti Maalum |
| (5) | Mhe. Salma Mussa Bilali | - Viti Maalum |
| (6) | Mhe. Saleh Nassor Juma | - Jimbo la Wawi |
| (7) | Mhe. Ashura Sharif Ali | - Viti Maalum |
| (8) | Mhe. Hassan Hamad Omar | - Jimbo la Kojani |
| (9) | Mhe. Mussa Ali Hassan | - Jimbo la Koani |
| (10) | Mhe. Mohammed Haji Khalid | - Jimbo la Mtambile |
| (11) | Mhe. Abdalla Mohammed Ali | - Jimbo la Mkoani |
| (12) | Mhe. Kazina Khamis Kona | - Viti Maalum |
| (13) | Mhe. Abdi Mosi Kombo | - Jimbo la Matemwe |
| (14) | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | - Jimbo la Chonga |
| (15) | Mhe. Raya Suleiman Hamad | - Viti Maalum |

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza wale waliochangia ripoti yetu kwa namna moja au nyengine wamefanya kazi nzuri sana na sisi kama Wajumbe wa Kamati kwa naiba ya Kamati yangu nasema kwamba tumepata faraja kubwa juu ya michango yao ambayo wamechangia hapa kuipelea mbele Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwapongeza wachangiaji niseme kwamba niwapongeze tena na Waheshimiwa Mawaziri na wao kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo zimeulizwa na Wajumbe wa Baraza lako leo tokea asubuhi mpaka jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mtoa maelezo ya kwanza ya ufafanuzi ni Mhe. Naibu Waziri wa Elimu Mhe. Zahra Ali Hamad, Mhe. Sira Ubwa Mamboya Kaimu Waziri wa uwezeshaji, Mhe, Rashid Seif Suleiman Waziri wa Afya na Waziri wa mwisho alietoa majumuisho katika wizara yake ni Mhe. Ali Juma Shamuhuna.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wote walitoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali ambazo ziliulizwa na Wajumbe ambao walikuwa wakitaka ufafanuzi juu za wizara zao zilizohusika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hii inasimamia wizara tatu; Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara ya Uwezeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, yaliyojitokeza kwa wingi katika Wizara ya Afya; kwanza ni upungufu wa watendaji katika Hospitali zetu na vituo vya afya mfano kama chumba cha *ICU* kongwe na wodi ya mifupa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mtendaji mmoja tu na kila chumba katika hivi vilikuwa vinahitajika watendani wasiopungua watano.

Lakini suala jengine ambalo lilichukuwa nafasi kubwa katika Wizara ya Afya ni suala zima la usafi ambao unahitajika sana katika vituo vya afya na hasa katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ambayo Hospitali ile ndio kioo cha Hospitali zetu zote za Zanzibar. Haya yanahitajika kwamba Serikali ifanye juhudi za makusudi ili matatizo haya yaondoke.

Mhe. Mwenyekiti, tukenda katika Wizara ya Elimu mambo ambayo yalichukua nafasi kubwa; kwanza ni kodi ya Bandari ambayo ilihusikana na mchango wa madawati. Suala hili linahitaji Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tulifanyieni kazi kwa nguvu zote. Kwa sababu Naibu Waziri na Waziri wameleta maelezo, kwamba changamoto kubwa ipo Wizira ya Fedha. Ni juu yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hili kulifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba tatizo la madawati linaondoka katika maskuli yetu na mchango huu unatumika katika mahitajio yale yalikusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ambacho kimejitokeza ni malipo ya walimu 159 waliokatwa mishahara yao. Suala hili limechangiwa na wajumbe wengi. Tunaiyomba Serikali pamoja na mbio zake zote basi iyende mbio kweli kweli, lakini walimu hawa walipwe haki yao.

Lakini jengine ni Bodi ya Mikopo ijitahidi sana kuwapa wanafunzi mikopo yao kwa wakati ili waweze kukidhi haja.

Jengine ambalo limezungumziwa katika Wizara ya Elimu ni maeneo ya Wizara na skuli zipatiwe hati miliki. Zile skuli ambazo hazijapatiwa hati miliki na yale maeneo ya wizara ambayo hayajapatiwa hati miliki basi vile vile wizara ijitahidi kushirikiana na wizara husika ili zipatiwe hati miliki.

Jengine ambalo limejitokeza ni tatizo zima la mwalimu wa Sayansi katika skuli ya Kojani.

Mhe. Mwenyekiti, mwalimu aliyeajiriwa siye aliyekusudiwa, lakini nampongeza mwalimu huyu kwa kupata ajira. Tunaiomba wizara kama alivyosema Mhe. Waziri afanye juhudi ya kutosha ili mwalimu huyu aajiriwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia hapa katika majumuisho yangu niende katika Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Suala zima ambalo limechukua nafasi kubwa mpaka Mhe. Makame Mshimba, lilikuwa limlize au lilimdondosha machozi ni udhalilishaji wa watoto ambao umechukua nafasi kubwa. Kwa hivyo, mashine ya *DNA* inunuliwe ili tupate kuwapatia ushahidi wale ambao wanakwenda kutoa ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu Idara ya Mikopo wapatiwe Ofisi, kwa sababu inaonekana kwamba wanakuwa na eneo ambalo halitoshi.Jengine ambalo linahusiana na Wizara hii ni

shamba lile la vijana Tunguu pamoja na Mbuzini Pemba yaimarishwe ili vijana wajisikie kwamba na wao wanafanya kazi vizuri.

Jengine ambalo nalizungumza hapa ni kesi za udhalilishaji zichukuliwe hatua bila ya kuchelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo na kwa maelezo hayo nirudie maneno yafuatayo ili nifunge mjadala wangu. Iwapo Serikali imelenga kuimarisha afya nchini kukuza ustawi wa jamii na kuwaendeleza wananchi wake kielimi ni lazima Wizara hizi zipatiwe fedha zake za bajeti kama zinavyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Ufinyu wa bajeti kila siku tukisema tu kwamba ufinyu wa bajeti, sasa wizara hizi zitakosa kufanya mambo yao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho, nakushukuru na nawashukuru Wawakilishi wote. Naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaoafiki kupokea ripoti hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto, wanyooshe mikono, wale wasioafiki, walioafiki wameshinda.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

## TAAFIRA YA SERIKALI

### Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza Yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Mwaka 2013/2014.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kazi zetu tulizonazo mpaka sasa hivi hazijamalizika. Lakini tukiangalia muda naona ni mdogo sana. Sasa na tayari hapa kuna baadhi ya Wajumbe wameleta vi-*memo*, kwamba kazi iliyofanyika leo ni kubwa sana akiwemo Mhe. Makame Mshimba. Sasa tumuombe basi Mwanasheria Mkuu atusaidie kutumia ile Kanuni yetu ya muda ili tuweze kuahirisha shughuli zetu hadi kesho asubuhi saa 3:00 ili tuweze kuendelea na shughuli hizo. Mhe. Mwanasheria Mkuu, karibu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nitowe hoja ya kutenga kando Kanuni ya muda ya 23 ili tuahirishe kikao hichi hadi kesho siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokata waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kukushukuruni sana kutokana na mashirikiano ambayo mmenipatia tokea asubuhi, hadi sasa hivi na hatimaye tukaweza kumaliza shughuli zetu kwa kiwango ambacho tumefikia kwa leo.

Baada ya maelekezo hayo sasa nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 20/03/2015 saa 3:00 za asubuhi. Naomba kuahirisha.

*(Saa 1:30 Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 20/03/2015 saa 3:00 za asubuhi)*